FOR ANSWERS SMS OR WHATSAPP 0723981225

# MARUDIO K.C.S.E KNEC 1995 – 2014
# KISWAHILI
# KARATASI 102/2

# MASWALI NA USAHIHISHO

**102 1B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT/ NOV 1995**
**2 ½ HOURS**

**Jibu maswali yote**

**1. UFAHAMU**
**Soma Makala yatuatayo kisha ujibu maswali**
Ama kweli maisha ya vijana wa kisasa yanatofautiana na kuhitilafiana pakubwa na yale ya wazee wao. Sio katika mavazi, lugha, mienendo, mitazamo, mawazo tu bali pia katika kipengele kingine chochote utakachofikiria. Yote haya ni vielezo vya jinsi kizazi cha leo kinavyoishi katika ulimwengu ambao ni kivuli tu cha ule wa vizazi vilivyotangulia. Baadhi ya watu wameieleza hali hii kuwa maisha sio jiwe. Kwao basi, si ajabu katu kuwaona vijana wakizungumza lugha yao ya kipekee au wakivaa nguo zinazobana ajabu na kudhirisha bayana maungo yao badala ya kuyasitiri.

Hata hivyo, watu wengi wameonelea kwamba hali ya maisha ya vijana wa leo maasia yanayotokana na utundu na hata ukatili wao. Upande huu umetoa rai kwamba kizazi hiki kisingepotoka kama tu kingezingatia na kustahi utamaduni wa wahenga wao ambamo wazazi wao ndimo walimokulia. Wanazidi kufafanua kuwa nyendo hizi za miaka ya nyuma zilithamini sana amali kama waminifu, heshima kwa wazee ama wakuu, bidii, ushirikiano, ukarimu, unyenyekevu, hadhari katika kila jambo, utiifu na pia kujitegemea. Yote haya yamesahaulika ama tuseme yamepuuzwa katika utamaduni wa kisasa."

Swali lilozuka sasa ni je tunapaswa kuwahukumu vijana wa leo kwa kutumia vigezo au masharti gani? Tuwapige darubini kwa kutegemea hali ilivyo hivi leo duniani ama tuwapime kwa mujibu wa jinsi maisha ya baba na babu zao yalivyokuwa. Jibu la swali hili ni gumu na sharti lifafanuliwe kwa makini lisije likaegemea upande wowote.

Mathalan, ni jambo lisilopingika kuwa maisha ni utaratibu unaothirika na hivyo kubadilika daima. Angalia kwa mfano jinsi maendeleo ya elimu, sayansi, mawasiliano na hata ufundi yalivyoyageuza maisha siku hizi. Yamkini vijana wa barani Afrika wakaona na hata kuzungumza wa wenzao kutoka Uropa, Asia na Marekani bila hata kunyanyuka hapa kwao nyumbani. Athari ya filamu, video, vitabu, magazeti, majarida n.k haikadiriki. Haya kwa kiasi yamewafanya vijana hata kupevuka kabla ya wakati wao. Isitoshe, mambo haya yameweza kuwazuzua na kuwaaminisha kuwa yale wanayojifunza ni kweli. Matokeo yamekuwa ni wao kuudunisha utamaduni wao wa asili na kuupapia ule wa wageni waliowaathiri. Tusisahau kuwa ujana ni tembo la mnazi na rahisi kwao kubadili mawazo.

Lakini hatuwezi kuwasamehe vijana wanaokosa akili razini kwa kupotoshwa na kuchacharika na yote, wanayoyapokea kutokea ugenini na hivyo kuanza kudhalilisha utamaduni wa Waafrika. Hata hivyo, badala ya kuwakashifu wanapopotea njia amakuwapongeza wanapotenda yale

tunayoyategemea tu, ni wajibu mkubwa wa wazazi kuwaongoza na kuwasaidia vijana kuwa na uwezo mkubwa na kufanya uteuzi mwafaka katika maisha yao.

**Maswali**

(a) Kulingana na mwandishi, kundi linalodai kuwa maisha sio jiwe' lina maoni gani? ( alama 2)

(b) Kulingana na taarifa uliyoisoma ni jinsi gani vijana wa kisasa wangeziepuka athari mbaya? ( alama 2)

(c) Kwa mujibu wa taarifa hii, utamaduni wa Kiafrika una manufaa. Yataje ( alama 4)

(d) Mwandishi anaposema mambo haya yameweza kuwazuzua na kuwaaminisha vijana kuwa yale wanayojifunza ni kweli anamaanisha nini? ( alama 4)

(e) Mbali na wazazi, ni makundi gani mengine ya watu ambayo yanapaswa kutoa mawaidha kwa vijana? ( alama 3)

(f) Kwa maoni yako vijana wanapaswa kufanya uteuzi wa namna gani katika mvutano huu wa tamaduni? ( alama 2)

(g) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika makala

(i) Maasia

(ii) Razini ( alama 2)

(h) Andika methali moja ambayo inaafiki taarifa hii ( alama 1)

## 2. MUHTASARI

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Ili kupiga vita propaganda za wakoloni mambo leo katika vyuo vikuu vyetu, inafaa kutumia Kiswahili kufundisha masomo yote. Jambo hili ni la lazima na linawezekana kabisa, ingawa lina matatizo yake. Jambo linalotakiwa kufanya ni kuchukua wananchi wenye elimu ya juu wakatafsiri fikra za wazalendo katika Kiswahili. Kwa njia hiyo, lugha ya wanachuo itakuwa ndiyo lugha ile ile ya umma

Ni jambo la kuepukwa kuwa na lugha mbili ambazo zinasaidia kuwatenga na umma. Wasomi wetu watakuwa wamekaribia umma kwa kutumia lugha iliyozoeleka na umma wenyewe. Jambo linalotutinga ni hili: mara nyingi wasomi wengine waliozoea kutakadamu lugha ya Kiingereza wanapojaribu kuwaeleza watu wengine jambo la kieleimu au kitaalamu, hushindwa kabisa. Wao huchanganya sana maneno ya Kiingereza na Kishwahili hata kufikia kiasi ambacho mtu wa kawaida haelewi chochote.

Kwa kuwa wakoloni mamboleo wameelewa kwamba lugha ni kioo cha kuchujia utamaduni, miaka ya hivi karibuni wamejifunza kwa dhati kuliko wakati mwingine kupigania ufundishaji wa lugha zao, hususa, Kifaransi na Kiingereza. Wakati huo wao wanatoa porojo kuwa kugha ya Kiswahili haifai na kwamba ni lugha ya watumwa. Kwa mfano, utaona katika maandishi mngi kila wanapoorodhesha lugha kuu za dunia. Kiswahili hakionyeshwi katika hizo.

Badala yake wanakiweka kwenye kiwango sawa na Kiganda, Kikikuyu, Kinyamwezi na lugha kadha wa kadha za kikabila. Hiyo ni harakati kubwa ya kudanganya umma na kukivua Kiswahili hadhi yake ilhali lugha hii inatumiwa na zaidi ya watu milioni mia moja wanaosambaa katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kwa kutumia hila hii, wao wanasadikisha watu wengi ili wachukulie Kiswahili kama lugha nyimgine ya kikabila. Ndiposa hawa wakoloni mamboleo wanawashawisha baadhi ya watumiaji wa Kiswahili wastawishe lugha za makabila mabalimbali na kuonyesha

kwamba umaarufu wa lugha hizo ni sawa na Kiswahili. Hayo bila shaka ni mawazo. Ukweli ulioko ni kwamba mawazo kama haya yawezi keundeleza ukabila. Hata hivyo sharti kueleweka kwamba kusema hivyo si kudhalilisha umuhimu wa kukuza lugha za kikabila. Tusemacho ni kuwa ukuzaji wa lugha hizo ungekuwa na kusidi moja kuu ambalo ni kustawisha Kiswahili kufika ngazi za kimataifa.

Swali ambalo ni muhimu kujiuliza ni hili: Wakoloni - mamboleo wanatuonaje tunapokazania Kiswahili? Je, wanaona ni faida kwao au kwetu? Jambo muhimu zaidi ni kutamba jinsi Kiswahili kinavyotuwezesha kuungana na kuwa kitu kimoja. Ni dhahiri kwamba wakoloni mamboleo hawafurahili wanapoona kishahili kikituunganisha. Machoni mwao Kiswahili ni ishara mojawapo ya kujikomboa kwetu kutokana na minyororo yao. Hivi si kusema kwamba hapupaswi kujifunza kiingereza, Kifaranza au Kijerumani, la hasha. Tunachosema ni kwamba tutumie Kiswahili ambacho ni kioo cha utamaduni wetu.

**Maswali**

(a) Mwandishi amesema nini kuhusu utengano kati ya umma wa wasomi?
( Maneno 30 – 40) ( alama 4)

(b) Eleza pingamizi zilizowekwa na wakoloni- mamboleo ili kudunisha Kiswahili (maneno 40 – 50) ( alama 8)

(c) Kulingana na mwandishi ni sababu gani zinazofanya wakoloni mamboleo kupinga maendeleo ya Kiswahili? (maneno 25- 30) ( alama 8)

**MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Akifisha kifungu kifuatacho
"Baba Wafua, ona Barua iliyotoka kwa mwanao. Hata hati haisomeki" "lo" baba watoto akamaka. Hii barua kweli imetoka kwa mwanangu Wafua. "Waniuliza mimi?" Mama akamjibu "Tazama maandishi na anwani basi. Shule ya Msingi ya Barungani S.L.P 128 Vuga."
( alama 5)

(b) (i) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi
Uwanja mwingineo umechimbuliwa kuongeza ule wa zamani ( alama 1)

(ii) Unda jina kutokana na kivumishi hiki ( alama 1)
Refu

(iii) Tunga sentensi moja ukitumia – ki – ya masharti ( alama 1)

(c) (i) Zifuatazo ni sehemu gani za mwili
(i) Kisugudi
(ii) Nguyu ( alama 2)

(ii) Andika maneno mengine yenye maana sawa na
(i) Damu ( alama 2)
(ii) Jura

(d) Tumia kitenzi KAA inavyofaa kujazia nafasi zilizoachwa
Onyango alipofika mkutanoni alikosa mahali pa………………..
Watu walikuwa wamejaa na hapakuwa na kiti hata kimoja cha ( alama 2)

(e) (i) Fafanua maana ya methali: Waso haya wana mji wao ( alama 1)
(ii) Tunasema kifurushi cha kalamu

………………………….. ya ndizi ( alama 1)

(f) (i) Tunga Sentensi tano kuonyesha matumizi matano tofauti ya neno KWA ( alama 1)

(ii) Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi

(a) Minghairi ya

(b) Maadam ( alama 2)

(ii) Ni mbinu gani za lugha zinazotumiwa katika sentensi hizi?

(a) Juma si simba wetu hapa kijijini

(b) Juma ni shujaa kama simba ( alama 2)

(g) Sentensi ifuatayo ina maana mbili totauti. Zieleze

Huyu amekuja kutuliza ( alama 2)

(h) Andika sentensi tatu kuonyesha maana tatu tofauti za neno KINA( alama 3)

(i) Eleza tofauti ya semi mbili zilizopigwa mstari

(a) Kevoga hana muhali; ikiwa hawezi kukufanyia jambo atakwambia

(b) Kevogo hana muhula; hivi sasa amekuambia hawezi kukufanyia jambo hili ( alama 2)

(j) Tofautisha maana

(a) Ningekuwa na uwezo ningesafiri kwenda ng'ambo

(b) Ningalikuwa na uwezo ningalisafiri kwenda ng'ambo ( alama 2)

(I) Yaandike maneno yafuatayo katika ufupi wake

A. (i) Shangazi zako

(ii) Mama zako ( alama 2)

B. Unda jina moja kutokana na majina yoyote mawili ya Kiswahili sanifu ( alama 1)

**102/B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT/NOV 1996**
**2 ½ HOURS**

**1. UFAHAMU**
***Soma makala yafuatayo Kisha Ujibu Maswali***
Zamani sana na hata hivi karibu watu wengi kote duniani walikuwa wakiamini kuwa kuna ardhi na mbingu tu basi. Imani hii ilijikita katika mantiki inayosema kwamba ardhi au dunia ipo katikati ya maumbile yote na isitoshe, ni tambarare.

Juu ya ardhi ni mbingu ambayo imejaa vimulimuli vidogovidogo sana viitwavyo nyota. Baina ya vimulimuli vipo viwili vikubwa viitwavyo mwezi na jua. Hivi viwili japo ni vikubwa kuliko vingine, bado ni vidogo kuliko ardhi.

Hii ndiyo imani iliyoutawala ulimwengu kwa miaka na miaka, na ikawa imekita mizizi. Lakini jinsi wanajimu walivyozidi kuelimika, waligundua kwamba ukweli wa mambo umejitenga kando kabisa na imani hii
Ukweli ni kwamba zima tulionalo la rangi ya samawati nusumviringo juu ya paa zetu za vichwa ni kubwa sana tena. Na si kubwa tu bali lazidi kupanuka. Katika bwaka hili lipanukalo kila uchao mna galaksi nyingi ajabu zisizokadirika. Ndani ya kila galaksi mna nyota mamilioni na mamilioni, malaki na kanui. Imejulikana kuwa nyota hizo japo huonekana kama vimulimuli vidogo sana usiku usiku ni kubwa ajabu. Kadiria mwenyewe! Jua letu ni nyota kubwa sana. Ukubwa wake umezidi wa dunia mara nyingi sana, zaidi ya elfu moja! Basi fikiria juu ya ukubwa wote huo. Imegunduliwa ya kwamba jua ni nyota ndogo sana ikilinganishwa na zingine zilizo katika galaksi yetu tu, licha ya galaksi nyinginezo zilizoko katika bwaka.
Na haya sio maajabu peke yake. Wataalam wamevumbua mengi ya kushangaza zaidi. Mathalan, imekuja kufahamika kuwa jua letu ambalo ni nyota, lina sayari tisa zinazolizunguka. Baadhi ya sayari hizi ni Arthi yetu. Zaibaki, Zuhura, Mirihi, na mshitara baina ya tisa jumla. Baadhi ya sayari hizi zina visayari vidogo vinavyozizunguka. Visayari hivi ndivyo viitwavyo miezi. Ardhi yetu ina mwezi miwili ilhali Mshitara ina kumi na miwili! Sayari hizi zote na visayari vyao, au vitoto ukipenda, havitoi mwanga. Nuru ya mwezi na nuru ya hizo sayari zinazolizunguka jua letu inatokana na jua lenyewe. Kwa hakika ni mmeremeto tu unaotufikia sisi kupitia sayari hizi kutoka kwa nyota hii yetu iitwayo JUA.
Kama wasemavyo washahili ya Mungu ni mengi. Taswira tuliyo nayo katika maelezo haya yaonyesha jinsi ambavyo mwanadamu licha ya kuwa na akili nyingi, bado hajawahi kuigusia siri kamili ya mungu. Lakini kwa ufupi twaweza kusema hivi. Ikiwa katika bwaka lote kuna galaksi nyingi, bila shaka kwa vile jua ni nyota basi zimo sayari nyingi ajabu zinazozunguka kila nyota au jua kama zipasavyo kuitwa. Kwa vile katika mfumo- jua imo sayari moja yenye viumbe vyenye uhai, binadamu wakiwemo, basi bila shaka katika mifumo- jua mingine katika galaksi yetu zipo sayari zinazofanana na ardhi hii yetu, ambazo sina viumbe vilivyo hai- penginepo watu pia! Wanona maajabu? Na katika magalaksi mengine je? *Mambo pengine ni yayo hayo*! Kwa hivyo huenda ikawa peke yetu katika bwaka hili; labda tuna viumbe wenzetu ambao hatutakutana nao katika uhai wetu kwa sababu uwezo wetu wa kimaumbile, na vile kisayansi ni hatifu. Lakini, kwa vile mwenye kupanga maajabu hayo yote, yaani Mwenyezi Mungu ni huyo mmoja basi huenda sote tukakutana Ahera.Mungu ni mkubwa

(a) Kulingana na habari hii, taja mambo manne ambayo ni imani potovu
( alama 4)

(b) Kwa kusema " ukweli wa mambo umejitenga kando" Mwandishi anamaanisha nini? ( alama 2)

(c) Taja sifa zozote nne za maumbile ya anga zinazopatikana katika habari hii ( alama 4)

(d) Taja vitu viwili vipatikanavyo katika galaksi ( alama 2)

(e) Taja sayari mbili ambazo ni kubwa kuliko ardhi ( alama 2)

(f) Ni ithibati gani iliyotolewa kuonyesha kuwa nyota sio vijataa vidogo? ( alama 1)

(g) Bainisha nuru aina mbili tuzionazo angani ( alama 2)

(h) (i) Ni neno gani lenye maana sawa na "anga" ama "upeo" katika habari hii? ( alama 1)

(ii) Andika neno moja ambalo lina maana sawa na paa kama lilivyotumiwa katika taarifa ( alama 1)

(i) Mwandishi anaposema kuwa katika magalaksi mengine "mambo pengine ni yayo hayo" anamaanisha nii? ( alama 1)

**UFUPISHO**

**2. Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali**

Mababu walituachia msemo maarufu kuwa " Kuzaa sio kazi. Kazi kubwa ni kulea." Busara iliyomo katika methali hii inatupambazukia peupe pindi tukianza kuchunguza maisha ya vijana wa siku hizi katika jamii zote, hasa zile za Afrika. Kwa upande mmoja, maisha ya vijana hawa yanaonyesha cheche ya matumaini kwa maisha ya siku za usoni kwa sifa zao za mori na kupenda kujaribu na kushika mambo upesi kama sumaku. Lakini kwa upande wa pili, tunashuhudia upotevu wa kimawazo na hulka ambayo ndiyo kipingamizi cha kuendelea kwao kama raia wa kutegemewa. Kuwanyeshea vijana lawama na kashifa za kila aina hakufai wala hakufui dafu katika juhudi za kuwaongoza na kuwalea. Kwa hili hatuna budi kusadiki, "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo." Basi hivyo badala ya kuwashambulia vijana wenyewe. Tutafanya hivyo kwa imani kuwa "mwiba uchomeako ndiko utokeako." Kiini cha matatizo ya vijana wa leo ni namna ya mwongozo na vielezo wanavyopokea kutoka kwa wazazi, waalimu, viongozi wa kijamii wakiwemo pia wale wa medhehebu tofauti na hasa kutokana na vyombo tofauti vya habari: vitabu majarida, filamu, magazeti na kadhalika.

Jamii ina haki gani kuwashtumu vijana iwapo mzazi, tangu utotoni mwao amewahubiria maji na huku mwenyewe anakunywa mvinyo? Kama fasihi na maandishi mengine wanayoyabugia vijana yamejazwa amali, picha, jazanda na taswira zinazohimidi ugeni na kutweza Uafrika, tutashangazwa na nini pale vijana watakapoanza kupania zile zile amali za ugenini? Iwapo jamii na mazingira wanamokulia vijana yanatukuza kitu kuliko utu. Hatupaswi kupepesa macho na kukonyeza tunapowaona vijana wakihalifu sheria zote kwa tamaa ya kujinufaisha binafsi.

Ni hoja isiyopingika kuwa kulea sio tu kulisha na kuvisha au kumpeleka mtoto shuleni sharti itambulike wazi wazi kuwa sehemu kubwa ya elimu na mwongozo unaoathiri mienendo ya jijana na watoto haitokani na yale waambiwayo bali hasa yote wanaoyashuhudia kwa macho na hisia zao.

(a) Katika aya ya kwanza, maisha ya vijana wa kisasa yameelezwaje? ( alama 6)

(b) Kwa nini vijana hawapaswi kulaumiwa kulingana na mwandishi Maneno 30 – 35 ( alama 8)

(c) Eleza sifa za malezi bora ( alama 6)
(Maneno 20 – 25)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Sahihisha makosa yaliyomo katika sentensi mbili zifuatazo
- (i) Bei za vitu zimepanda juu sana siku hizi
- (ii) Weka mizigo kwa gari ( alama 2)

(b) Eleza maana ya sentensi hizi
- (i) Mikono yao imeshikana
- (ii) Mikono yao imeshikamana ( alama 2)

(c) Andika sentensi zifuatazo ukitumia kinyume cha neno lililoandikwa kwa herufi za Mlazo
- (i) Usijaribu *kupaaza* sauti unapoimba
- (ii) Huyu ni mtu *mwenye busara*
- (iii) Binadamu hawezi *kumuumbua* mwenzake

(d) Fafanua maana za misemo ifuatayo kwa kuitungia sentensi
- (i) Kula uyundo ( alama 2)
- (ii) Kula uhondo (alama 2)
- (iii) Kula mori ( alama 2)

(e) Akifisha kifungu kifuatacho
Bwana mwenyekiti wetu wa leo wazazi wote na hata wanafunzi leo ni siku muhimu je mngependa niwafahamishe msaada tuliopokea kutoka kwa wizara ya elimu
( alama 4)

(f) Eleza kazi ifanywayo na
- (i) Mhariri
- (ii) Jasusi ( alama 4)

(g) Tunasema: Mtoto huyu mzuri anapendeza
Ukitumia majina yafuatayo kamilisha sentensi ukifuata mfano ulio hapo juu

- (i) Ngome ( alama 1)
- (ii) Mitume ( alama 1)
- (iii) Heshima ( alama 1)
- (iv) Ng'ombe ( alama 1)
- (v) Vilema ( alama 1)

(h) Kutokana na vitenzi tunaweza kuunda majina na pia kutokana na majina tunaweza kuunda vitenzi. Mfano

| **Jina** | **Kitendo** |
|---|---|
| Mwuzaji | Uza |
| Mauzo | Uza |
| Wimbo | Imba |

**Sasa kamilisha:**

| | **Jina** | **Kitenzi** | |
|---|---|---|---|
| (i) | Mnanda | | |
| (ii) | Kikomo | | |
| (iii) | | Ruhusa | |
| (iv) | | ashiki | |
| (v) | | husudu | ( alama 5) |

(i) Andika katika msemo halisi
Mvulana alimwambia baba yake kuwa alitaka kwenda sokoni
(alama 2)

(ii) Andika katika msemo wa taarifa
"Nitakuwa nikija hapa kila siku kukuona", Kamau alimwambia shangazi yake

(j) Eleza matumizi ya 'Po' katika sentensi hii ( alama 2)
Nilipofika nilimwona pale alipokuwa amesimama

(k) Mtu akicheza mchezo mahali Fulani tunaweza kusema alichezea hapo
Ukifuata mfano huu, tumia vitenzi vilivyoko katika mabao kukamilisha
( alama 2)

(i) Ali hapo (la)

(ii) Ali hapo (fa)

(iii) Ali hapo (oa) ( alama 3)

**102 1B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT/NOV. 1997**
**2 ½ HOURS**
**JIBU MASWALI YOTE**

**1. UFAHAMU**
***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali***
Binadamu kwa wakati huu amemaka kwa sababu amechafua mazingira yake pasipo tahadhari. Mathalani insiya amejaza gesi za sumu zitokazo viwandani na hata kuchafua mito kutokana na maji machafu kutoka viwanda hivyo. Takataka zinazotupwa ovyo ovyo zinarundikana kila mahali. Isitoshe miti inakatwa vivyo hivyo bila simile. Matokeo ya haya yote ni kwa mfano tunapata mvua ya asidi ambayo huhasiri mimea. Aidha nao ukanda wa ozoni unaotukinga dhidi ya miali hatari kutoka kwa jua umeharibiwa tayari na hivyo kuongeza joto duniani. Sehemu nyingi zimeanza kugeuka na kuwa jangwa huku sehemu zingine zikifurika kwa maji ya mito na mvua. Maji haya yameanza kumeza visiwa vingi vilivyo baharini. Kutokana na madhara haya, binadamu sasa anatapatapa ili kutafuta makao kwingine kwenye salama. Ndiposa siku hizi nadhari za binadamu zimeelekezwa katika mawanda mengine nje kabisa ya kisayari hiki kidogo kiitwacho dunia.

Kwa miaka mingi sasa binadamu amekuwa akitafakari uwekano wa kuishi katika sayari nyingine. Hii ndiyo sababu mwaka wa 1969 waamerika walimkanyagisha binadamu wa kwanza kabisa mwezini. Lengo lilikuwa ni kutalii na kuchunguza uwekano wa binadamu kuishi huko ili wale watakaoweza wahamie huko, hata mimea. Mwezini ni vumbi tupu lisiloota chochote. Kipatikanacho kwa wingi sana ni madini tu ambayo hayawezi kufaidi binadamu kwa lolote.

Sayari nyingine alizozitalii binadamu ni Zuhura, Mirihi, Mushtara na tuseme karibu zote zinazolizunguka jua. Kilichogunduliwa ni kuwa upo uwezekano wa sayari kama Zuhura na pengine Mirihi kuwa na mvua, lakini nyingi mno isiyoweza kuruhusus mimea kukua. Sit u, zuhuria inasemekna kuwa joto sana wakati wa mchana ilhali Mirihi ni baridi sana siku zote; baridi kiasi cha kuuwa binadamu na wanyama hawawezi kuishi huko. Mushtara yasemekana kuwa joto ajabu, ambapo hizo sayari nyingine zina joto sana au zina baridi sana. Habari hii imemfunga binadamu katika jela ya kijisayari chake kiki hiki kiitwacho dunia anachokichafua uchao.

Je, binadamu amekata tama? Hata kidogo! Ndio mwanzo anajaribu sana kuzikata pingu alizofunzwa na maumbile. Vipi? Amejaribu kuchunguza uwezekano wa kuihama ardhi na kuishi baharini, kwa sababu bahari inazidi ardhi mara tatu kwa ukubwa. Na ni vipi binadamu anadhani anaweza kuishi baharini mahali ambapo hakuumbwa aishi humo kama samaki?
Jawabu ni kuwa angefanya hivyo kwa kutumia maarifa yake.

Binadamu anaamini kabisa kuwa ana uwezo wa kujenga miji mikubwa mikubwa humo humo baharini… mikubwa zaidi yah ii tuliyo nayo ardhini. Anaamini ya kuwa anaweza kuitawala bahari kiasi alichitawala ardhi, na hivyo basi kufanya bahari impe makao na kumlisha bila ya kuyabadilisha maumbile yake. Na iwapo hili halitawezekana basi, ikiwajibika, abadilishe maumbile yake kwa kujiunda mashavu kwa mfano, ili avute pumzi ndani ya maji

Njia ya pili ya kuepukana na pingu za maumbile ni kuishi angani. Hii ina maana ya kujenga miji iliyoelea angani, kama madungu vile. Na kwa vile anga haina kikomo, binadamu atakuwa amejipatia visayari vyake visivyo idadi ingani!

Njia ya tatu ni kubadilisha umbo lake ili asihasirike na joto wala baridi. Binadamu wa kisasa anaamini kuwa inawezekana kumuunda upya mtu katika maabara badala ya katika mamba.
Mtu huyu wa maabra, aitwaye 'cyborg' kwa lugha ya Kiingereza, anaweza kuwa na chuma ndani badala ya mifupa, na mwili wa kawaida wa udongo na maji nje.

Kiunde huyu atakuwa hadhuriki ovyo ovyo kama binadamu wa sasa aliyeumbwa kwa chumvi, maji na protini. Au bora zaidi, binadamu mpya wa maabarani aundwe kwa zebaki. Binadamu huyu wa zebaki hafi wala hakatikikatiki. Na iwapo atakatika vipande vipande, basi kama zebaki hivyo vitaundika tena upya na kumrudishia umbo la awali kamili.

Njia nyingine ya kuepukana na uangamizi ni kutumia viunde vyake vya electroniki kama vile tarakilishi yaani kompyuta, na mitambo mingine kama iyo. Binadamu anaamini kwamba uwezo wa vyombo hivi utakapokamilishwa, basi vitamsaidia kwa lolote lile.

**Maswali**

(a) Inasemekana kwamba binadamu anakichafua hiki kisayari chake kila uchao. Kwa kutumia mifano mitatu, eleza vile binadamu amechafua mazingira yake. (alama 3)

(b) Kwa nini ongezeko la joto limeleta jangwa duniani wa wakati huo huo likaleta mafuriko? ( alama 3)

(c) Eleza sababu mbili zinazomfanya binadamu kuhangaika na kutafuta makao kwingine ( alama 2)

(d) Ni mambo gani yanayomfunga binadamu katika ardhi. Taja mawili ( alama 2)

(e) Unadhani ni kwa nini madini mengi yaliyoko mwezini hayaletwi duniani. Taja na ufafanue sababu mbili ( alama 4)

(f) Kulingana na aya mbili za mwisho, eleza jambo ambalo binadamu anajaribu kukwepa ( alama 2)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu ( alama 4)

  (i) Mashavu
  (ii) Madungu
  (iii) Asihasirike
  (iv) Kiunde

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali***

Vijana wengi wake kwa waume, walikuwa ndio tu wakamilishe shughuli ya kusajiliwa chuoni. Walikuwa bado nadhari zao zimetekwa na ugeni, hawajapata starehe akilini mwao wala kujisikia wamekaribia kama kwao nyumbani. Kwa hakika mazingira yale mapya yalikuwa yanawapa kiwewe kidogo au tuseme hata woga kiasi. Kusema kweli, kwa wakati ule walikuwa hawajui ni maisha ya namna gani yanayowasubiri mahali pale. Hawakuweza kukadiria kwa uyakinifu wowowtw iwapo makaazi yao pale ya miaka mine mizama kuanzia wakati ule, yangekuwa ya utulivu na raha au pengine yangeondokea kuwa ya roho juu juu na matatizo chungu mzima.

Wamsubiri mkuu wa Chuo aingie wamsikize atakalosema, kisha ndipo waweze kubashiri vyema mkondo wa maisha yao utakavyokuwa. Lakini jinsi walivyosubiri Mkuu wa chuo aingie ukumbini ndivyo wayo wayo lao lilivyozidi kuwacheza shere. Waliwaza: Ugeni jamani kweli ni taabu. Mawazo mengi yaliwapitia bongoni mwao. Wakawa kinywa ukumbi mzima, kama kwamba

wamekuja mazishini badala ya kuja kusoma. Waliwaza na kuwazua. Waliona au pengine walidhani kuwa hapa kila kitu ni tofauti.

Wanafunzi hawa waliona tofauti nyingi kati ya mambo pale chuoni na yale waliyokuwa wameyazoea. Kwa mfano, mwalimu mkuu hapa hakuitwa ‘ headmaster’ kama kule katika shule za msingi na vile shule za upili aliitwa ‘ vice – chancellor’ Nyumba za kulala hazikuitwa ‘dormitory’ au ‘mabweni’, kama walivyozoea, bali ziliitwa ‘ halls’ kwa sababu sio kumbi za aina yoyote ile, bali ni nyumba hasa, zenye vyumba vya kulala, kama walivyozoea kita walipokiwa shule zao za upili huko, bali hapa wenyewe wenyeji waliita kwa majina mengine kabisa! Mara University, mara zutafindaki, mara Ndaki kwa ufupi, mara Jamahiri ya na kadhalika na kadhalika! Waliwaza: kweli mahali hapa wenyewe wenyeji waliita kwa majina mengine kabisa! Mara kumzubaisha mtu hadi kufikia kiwango cha kuonekana kama zuzu! Hata hivyo hawakuvunjika moyo, bali walipiga moyo konde wakanena kimoyomoyo: Potelea mbali! Ukiyavulia nguo, yaoge! Walikuwa wamo katika hali ya kurandaranda katika ulimwengu wa mawazo pale katika ulimwengu wao mpya, ulimwengu mwingine kabisa usioafanana hata chembe na ule waliouzoea, mkuu wa chuo alipoingia.

Kuingia mkuu wa chuo wote walisimama kwa pamoja na kwa mijiko, wamekauka kama askari katika gwaride. Kuona hivyo, mkuu wa chuo akwaashiria wakae tu, bila kujisumbua. Kicheko kikawatoka bila kukosa adabu na heshima, kasha wakakaa kwa makini ndio mwanzo wakajisikia wamepoa.

Kuona kuwa sasa wametulia na wamestarehe. Mkuu wa chuo akaanza kwa kuwaamkua kisha akawajulisha kwa wakuu wote wa vitivo mbali mbali na idara mbali mbali waliokuwa wamekaa pale jukwani alipo yeye upande huu na huu.

Kufikia hapo, alaka ikawa imeungwa baina ya wenyeji na wageni wao. Kila mtu akaona mambo yamesibu tena; huo bila shaka ni mwanzo mwema, na kama ilivyosemwa na wenye busara, siku njema huonekana asubuhi. Hii, Kwa wote ndiyo asubuhi tu, bali ni asubuhi njema, si haba.

**JIBU KILA SWALI**

(a) Ukirejelea aya ya kwanza na ya pili, eleza wasiwasi wanafunzi waliokuwa nao wakati wakisubiri (maneno 45- 55) ( alama 7)

(b) Ni mambo gani mageni wanafunzi hawakuyazoea yanayoelezwa katika kifungu (maneno 25 – 30) ( alama 3)

(c) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za mwisho kwa kutumia maneno yako mwenyewe. Tumia maneno 40 -45 ( alama 10)

## 3. MATUMIZI YA LUGHA

**Jibu maswali yafuatayo kulingana na maagizo**

(a) Andika katika msemo wa taarifa
Mzazi: Kesho nataka ufike nyumbani mapema, unasikia?
Mtoto: Nitajaribu, lakini mwalimu alisema tutafanya mtihani jioni ( alama 4)

(b) Badilisha katika udogo kasha uukanushe udogo huo
(i) Guu lake limepona baada ya kuumwa na jibwa la jijini ( alama 2)

(ii) Nyumba yenyewe ilijengwa bondeni karibu na mto ( alama 2)

(c) Andika katika kauli ya kutendesha

(i) Nataka upike chakula hiki vizuri ( alama 1)

(ii) Toa ushuru wa forodhani

(d) Sahihisha bila kubadilisha maana:

(i) Usikuje hapa kwetu kwani sitakuwamo ( alama 1)

(ii) Basi la shule imeharibika moshi nyingi inatokea dirishani na maji inatiririka ovyo ( alama 2)

(e) Bila kubadilisha maana, andika sentensi zifuatazo ukitumia kirejeleo cha ngeli kifaacho

(i) Nyumbu alishinda farasi kukimbia ( alama 1)

(ii) Milango yote yajifunga ovyo, nenda uakafunge ( alama 1)

(iii) Hamisi amekata nyasi vizuri ( alama 1)

(iv) Jiwe lile liliangukia matunda ( alama 1)

(f) (i) Eleza maana ya misemo ifuatayo kwa kuitungia sentensi moja moja

Kuramba kisogo ( alama 2)

Kuzunguka mbuyu ( alama 2)

(ii) Andika methali nyingine ambayo maana yake ni kinyume cha Riziki kama ajali huitambui ijapo

(g) Eleza matumizi manne tofauti ya – na ( alama 4)

(h) (I) Eleza maana mbili mbili zinazotokana na sentensi zifuatazo

(i) Mtoto alitimua mbio, kuona nyoka ( alama 2)

(ii) Juma alifagia chakula ( alama 2)

(iii) Sisikii vizuri ( alama 2)

(II) Mahali palipohamwa panaitwa ( alama 1)

(i) Tunga sentensi ya neno moja ambayo ina visehemu vifuatavyo vya sarufi

- Kiima
- Wakati
- Kirejeleo
- Kiswahili kitendwa
- Kitenzi ( alama 5)

(j) Bila kunyambua, andika maneno mawili ambayo yanatokana na shina moja na neno: imani ( alama 2)

**102 1B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT/NOV. 1998**
**2 ½ HOURS**

**1. UFAHAMU**
***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata***

Kuna sayansi mpya inayoitwa "cloning" kwa lugha ya Kiingereza. Pengine kwa sasa tuite "kutumbisha." Sayansi hii tayari imeleta mapinduzi makubkwa katika uzalishaji mimea na uvunani. Imesemekana ya kwamba, ghairi ya wivu na kijicho baina ya jamii mbalimbali ulimwenguni, aina hii ya sayanzi ina uwezo na kuangamiza kabisa janga la njaa katika sayari hii yetu. Kivipi? Rahisi kabisa. Ni kwamba mbegu moja tu ya aina yoyote ya mmea, baada ya kuneemeshwa vyumba vyake vidogo ambavyo ndivyo hasa msingi wa uhai vinaweza kunyunyiziwa dawa maalum ili vitawanyike mara hata mamilioni na kuwa mimea kamili…. Mamilioni!

Sayansi hii tarari inatumiwa kukuza viazi na vyakula vingine. Hii ina maana ya kwamba mashamba makubwa si muhimu siku hizi, yaani vyakula vingi kabisa vinaweza kukuzwa mahali padogo sana. Kwa hivyo hivi karibuni tu, kutakuwa hakuna haja ya kupigania mashamba.

Vyema. Hebu sasa tuangalie zilizokwishapigishwa hii sayansi ya "kutumbisha" na mahali binadamu alipofika kimaendeleo kwa sababu ya hatua hizo. Jambo la kwanza sayansi hii tayari imeshatumiwa kuzalishia wanyama wengi, wengi sana wadogo wadogo kwa lengo la kuendeleza mbele utafiti. Kufikia sasa, wanyama hawa waliotengenezwa na binadamu katika maabara yake bado wanahifadhiwa mumo humo walimotengenezwa. Hii ni hatua kubwa na binadamu anastakili pongezi kwa jinsi anayotumia akili yake kuvumbua ibura hizi zote.

Hata hivyo imesemwa kwamba *kuchamba kwingi ni kuondoa mavi*. Binadamu kama ijulikanavyo, anajaribu sana jujitakasa kwa kujitenga mbali sana na asili yake ya unyama ili aufikie ubinadamu mkamilifu. Hapana ubaya hapo. Lakini tukirudi nyuma tunakuta ya kwamba binadamu sasa aneingia tama kubwa sana kuliko wakati wowote ule. Tamaa hii imeletwa na ujuzi wake katika sayansi hii ya "kutumbisha." Sasa binadamu ana jua vizuri sana kwamba kwa vile ana ujuzi wa kutengeza panya na hata kondoo katika maabara basi hata ujuzi wa kutengeneza binadamu pia anao! Na hapo ndipo tatizo lilipo. Swali hi hili: Je, ujuzi huu utatufikisha wapi? Na kikomo chake kitakuwaje?

Binadamu sasa ujuzi wake unamtia wasiwasi. Wataalam wa sayansi hii wamejiuliza mara nyingi nini kitakachotokea ujuzi huu utakapomilikiwa na mwenda wazimu mweledi." Watu kadha wa kadha, miongoni mwao wakiwa wanasiasa wamejiuliza mara zisizohesabika swali hili: kama Hitler angekuwa na ujuzi huu, angekuwa na lazima gani ya kuwaulia mbali wayahudi milioni sita wasiokuwa na hitia isipokuwa na nywele nyeusi na hawakuwa weupe sana kama wazungu? Hitler aliamini ya kwamba *"mtu mzuri"* ni mwenye pua ya upanga (kama mzungu), macho ya buluu nywele rangi ya dhahabu na mwenye kimo cha futi sita au zaidi kidogo. Hivyo lengo lake lilikuwa ni kubuni taifa la watu wazuri pekee ambao mwisho watautawala ulimwengu na kuenea duniani kote. Katika mpango wake, watu weusi wote wangefaa kuangamizwa tu ili watoe nafasi kwa watu aliowaona yeye kuwa bora.

Sasa baada ya sayansi hili ya "kutumbisha" kuvumbuliwa, wataalam wametishika sana. Wamewaza jinsi ambavyo Hitler angeweza kufanya kama angekuwa mjuzi wa taaluma hiyo.

Kitisho hiki kimezidi kuwatwanga wataalam na wasiokuwa wataalam hivi majuzi tu ilipogunduliwa maiti ya msichana wa miaka kumi na mine huko milima ya Andes, Amerika ya kusini. Msichana huyo alikuwa ametolewa kafara miaka karne tano zilizo pita lakini hakuoza kwa sababu ya baridi kali ya barafu milimani.

Kwa sababu ya dukuduku la uvumbuzi ambalo haliishi dhana za kiajabu ubongo wa binadamu, wataalamu wa "kuchezea" maumbile walipomwona msichana huyo maiti, upesi upesi wakampima. Walipofanya hivyo wakagundua ya kwamba mayai yake ni timamu kabisa wala hayajaharibiwa na mpito wa karne. Papo hapo wengine wakajiwa na wazo la kuyatoa mayai hayo na kuyahifadhi kwenye mabara. Tamaa ikazidi zaidi ya zaidi. Baadhi ya wataalamu wakajiwa na wazo la "kuyaneemesha" mayai hayo na mbegu za uzazui za wanaume. Kwa lengo gani? Kuunda watoto amabo mama yao alikufa zamani za kale ili waonekane watakuwa watu wa aina gani!

Sasa fikiria mwenyewe! Watoto hawa wa maabara wakiwa weledi zaidi ya binadamu yeyote yeyote wa kisasa lakini watiifu kama mbwa na paka itakuwaje? Hakuna atakayefikiria "*kutumbisha*" ili tuwe na vijitumwa vyetu vipenzi majumbani mwetu vinavyofanana nasi badala ya paka na mbwa wasiovishwa nguo?

(a) Andika kichwa kifaacho kwa nakala hii ( alama 1)

(b) Kutumia sayansi ya "kutumbisha" kunaweza kumsaidia binadamu kuangamiza mabaa gani mawili yanayomkabili sasa? ( alama 2)

(c) Unadhani ni kwa nini wanyama waliozalishwa kwa kutumia sayansi hii bado wamo maabarani? ( alama 3

(d) Fafanua methali "kuchamba kwingi nikuondoka na mavi" kulingana na muktadha wa habari hii

(e) Kuna ubaya gani kutumbisha watu? ( alama 4)

(f) Mwandishi anaonekana kutishwa sana na uwezekano wa sayansi ya kutumbisha kuishia mikononi mwa "wendawazimu weledi" kwani kuna hatari gani? ( alama 4)

(g) Eleza kwa ukamilifu matatizo yanayoweza kuukumba ulimwengu iwapo mayai ya msichana wa Andes yatatumbishwa ( alama 4)

**MUHTASARI**

***2. Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata***

Lugha ya Kiswahili ni lugha iliyoendelea sana. Leo hii lugha hii inasema na watu wote nchini Tanzania, Rwanda na Burundi, inasemwa na watu wote nchini Kenya. Nchini Uganda, Zaire, Malawi, msumbiji, Zambia, Somalia, Bukini (Madagascar) na Ngazija (Comoro), inasemwa na asilimia kubwa za wananchi wa huko. Aidha lugha hii ina wasemaji si haba katika kisiwa cha Sokta na nchini Oman.

Fauka ya maendeleo haya, Kiswahili kinatumika kwa minajili ya matangazo ya habari katika idhaa nyingi za mashirika ya habari ulimwenguni. Nchi zenye idhara za Kiswahili ni kama vile hizi zetu za Afrika ya Mashariki na kati, Afrika ya kusini, Nigeria, Ghana, Uingereza, ( shirika la B.B.C) Marekani ( shirika la V.O.A), Ujerumani ( shirika la Radio Deutch Welle, Cologue), Urusi ( Radio Moscow), China, India na kadhalika.

Maendeleo mengine yanapatikana katika upande wa elimu, Marekani peke yake, kuna vyuo zaidi ya mia moja vinavyofundisha Kiswahili kama lugha muhimu ya kigeni. Huko Uingereza vyuo kama London, Carmbridge na Oxford vinafundisha lugha hii. Nci nyingine ambazo zina vyuo vinavyofunza lugha ya Kiswahili ni kama vile Japan, Korea, Ghana, Nigeria na kadhalika

Kweli Kiswahili kimeendelea jamani. Lakini je, kilianza vipi? Na ilikuwaje kikaweza kupiga hatua hizi zote?
Kiswahili kilianza kuzungumzwa na kabila dogo la watu waliokuwa wakiitwa wangozi. Watu hawa walikuwa wakiishi mahali palipoitwa shumgwaya. Shungata ni nchi ya zamani iliyokuwa eneo lililoko katika nchi katika nchi mbili jirani ambazo siku hizi ni Kenya na Somalia. Kabila hili la wangozi iliishi irani na makabila mengine kama vile wajikenda, wapokomo, Wamalakote ( au Waelwana) na Wangazija ( kabla hawajahamia visiwa vya Ngazija) Lugha ya wangozi siku hizo, ambayo ndiyo mzazi wa Kiswahili cha leo, ilijulikana kwa jina kingozi. Kama ilivyosemwa hapo awali, kingozi kilisemwa na watu wachache sana.

Je lugha hii ilikuwaje mpaka ikapata maendeleo haya makubwa tunayoyashuhudia siku hizi? Ama kwa hakika, Kiswahili ni lugha iliyobahatika tu. Inaweza kusemwa kwamba lugha hii ilipendelewa na mazingira na historia.

Jambo la kwanza, wageni waliotoka mashariki ya kati kifukia hizi janibu zetu Afrika ya mashariki walikaribishwa vizuri na hawa wangozi. Wakaingilia wageni na wenyeji kindakindaki, kidini, kitawala, kibiashara na kitamaduni kwa jumla. Punde si punde wangozi, ambao baadaye walijulikana kama waswahili na wageni hawa, wakaelimika katika dini (ya kiisilamu), biashara na mambo ya utawala aina mpya. Lugha yao nayo ikapanuka pale ilipochukua msamiati ya kigeni hususan wa Kiarabu na Kiajemi na kuufanya uwe wake, ili kueleza kwa rahisi zaidi mambo haya mageni katika taaluma za dini, biashara, siasa na hata sayansi kama vile unajimu. Wakati huo, lugha ya Wangozi sasa ikaitwa Kiswahili wala sio kiangozi. Tatizo hapa ni kuwa kwa vile Kiswahili kilichukua msamiati mwingi wa kigeni ili kuelezea taaluma hizi mpya, baadaye kimekujashukiwa kwamba ni lugha ya kigeni ilhali ni lugha ya Kiafrika asilia, na kitovu chake ni nchi mpya za kiafrika ziitwazo Kenya na Somalia hii leo.

(a) Thibitisha kuwa Kiswahili kimekuwa lugha ya kimaitaifa ( maneno 35 – 40) ( alama 6)
(b) Eleza kwa ufupi asili ya Kiswahili hadi kuja kwa wageni ( maneno 20 – 25) ( alama 4)
(c) Ukitumia maneno yako mwenyewe, eleza ujumbe uliomo katika aya ya mwisho ( alama 10)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Akifisha kifungu hiki:
Nilopomwendea aliniangalia kisha akaniambia siamini kuwa ni wewe uliyeandika insha hii. ( alama 3)

(b) Onyesha kielezi, kivumishi, kitenzi na jina katika sentensi:

Watu wane walipeperushwa juu kwa juu na upepo mkali ( alama 4)

(c) Taja madini mawili ambayo yametukuzwa zaidi, moja kwa thamani yake ya kifedha na nyingine kwa kutengeneza vyuma vigumu kuliko madini mengine ( alama 2)

(d) Tumia viunganishi vingine badala ya vile vilivyotumiwa katika sentensi hizi:
(i) Anayetafuta hachoki hata akichoka keshapata ( alama 1)
(ii) Ngonjeeni hadi washiriki wote wafike ( alama 1)

(e) Watu wafuatao wanafanya kazi gani ( alama 2)
(i) Mhasibu
(ii) Mhazili

(f) Tumia kiulizio – pi – kukamilisha
(i) Ni mitume ………………………. Aliowataja? ( alama 1)
(ii) Ni kiziwi ………………………. . Aliyemwona akipita?( alama 1)

(g) Eleza tofauti mbili muhimu za kimaumbile kati ya wanyama ( alama 4)
(i) Kifaru
(ii) Nyati

(h) Tunatumia viashiria vya kuthibitisha kwa mfano kitabu kiki hiki. Sasa kamilisha
Ni mbwa …………………….. aliyekula chakula cha mtoto ( alama 1)

(i) Tumia semi hizi katika sentensi kuonyesha maana:
(i) Kuchokoachokoa maneno ( alama 2)
(ii) Kumeza shibiri ( alama 2)

(j) Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia kirejeshi ( kihusiano) cha ngeli cha mwisho
Mwanafunzi anayefanikiwa maishani ni yule anayesoma kwa bidii na pia anayetii wakuu wake ( alama 2)

(k) Tunga sentensi mbili zinazobainisha tofauti kati ya:
(i) Goma
(ii) Koma ( alama 2)

(l) Jaza viambishi vifaavyo katika sentensi zifuatazo:
(i) Ukuta ----------enyewe una nyufa nyingi lakini fundi …… ote anaweza Kuukarabati ( alama 2)
(ii) Maji yalizoa changarawe …….. ote na vitu ……. Ingine……o ufuoni mwa bahari. ( alama 2)

(m)(a) Eleza matumizi ya
(i) Isije ikawa
(ii) Huenda ikawa ( alama 2)
(b) Tunga sentensi za kuonyesha matumizi hayo ( alama 2)

(n) Onyesha maana mbili tofauti za neno ‘hapa’ (alama 2)

(o) Andika maswali mawili ambayo hayahitaji majibu ya moja kwa moja (alama 2)

**102 1B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT./NOV. 1999**
**SAA: 2 ½**

**UFAHAMU**
**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamaake-kuu.

Yeye hatarajii kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia watoto, na daima dawamu kuwa '<u>mwendani wa jikoni</u>' akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. <u>Akanyangapo mume naye papo huutia wayo wake.</u>

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, historia, jiografia, hesabu, sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya. Akataka kuwa mwalimu, akawa. Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandishi, madereva wa magari, mawakili, mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi. Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa <u>hateswi akafyata ulimi</u>. Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali 'mahali pake' katika jamii alipotengewa na wanaume wenye mawazo ya kihafidhina yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake, iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha <u>ukutani.</u>

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanamume wa 'kisasa', ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama mshirika sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya <u>aushi.</u>

**MASWALI:**

a) Msemo 'mwendani wa vijungu jiko' unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii? (alama 2)

b) Jamii imemfanya mwanamke kuwa hayawani wa mizigo. Fafanua (alama 2)

c) Eleza maana ya 'akanyagapo mume papo huutia wayo wake.' (alama 2)

d) Zungumzia maswala ya ndoa na elimu huku ukilinganisha mwanamke wa kiasili na wa kisasa. (alama4)

e) Mwanamume wa kisasa anamwonaje mwanamke wa kisasa? (alama 2)

f) Taja mifano minne ya 'mawazo ya kihafidhina. (alama 4)

g) Eleza maana ya:
   (i) Akafyata ulimu…………………………………………
   (ii) Ukatani…………………………………………………….
   (iii) Taasubi za kiume……………………………………….
   (iv) Aushi……………………..……………………………..
(alama 4)

2. **MUHTASARI**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Siku hiyo nilipitia mahali hapo kama nilivyokuwa nikimuona siku hizi zote, mwaka nenda mwaka rudi. Nilisimama huku nikishangaa kwa mara nyingine tena.

Nilikuwa najitayarisha kujiendea na hamsini zangu mtu huyo alipojipinda kwa mbali sana. Kwa hakika nilidhani macho yangu yananihadaa. Nikafikicha macho yangu nikitumia nishati yote iliyomo mwilini mwangu ili niyatoe matongo ambayo nilituhumu kwamba ni akili yangu tu iliyokuwa imeniadaa, nikaamua kuendelea na safari yangu kwenda kujitafutia riziki.

Hatua ya kwanza na ya pili, moyo haukunipa. Sauti katika kilindi cha moyo wangu ikanisihi na kunitafadhalisha nitazame nyuma. Kutupa jicho nyuma, nikamnasa mtu huyo akeguka! Nikashtuka sana! Jambo la kwanza nildhani macho yangu yameingiwa na kitu kilichoyafanya kuona mambo yasiyokuwepo. Pili, nilidhani iwapo niliyoyaona yana msingi wowote, basi huenda ama nina wazimu, au yule mtu ni mzuka, hasa kwa vile ilionekana ni mimi tu nimuonaye. Nilikikuwa niko katika hali ya kufanya uamuzi kuhusu dhana zangu hizi aina aina mtu huyo alipojigeuzageuza, kisha akafunua macho! Moyo ulinienda mbio. Nilitaka kutifua vumbi ili wazimu usinizidie, lakini sikupata nafasi. Mtu yule alijizoazoa na kuketi kitako. Kisha akatokwa na maneno katika lugha iliyofanana sana na Kiswahili. Niliyaelewa aliyokuwa akisema.

Ajabu ya maajabu, mtu huyo alidai ya kwamba tangu alipolala kivulini hapo tangu jana baada ya chakula cha mchana, hakuota ndoto hata moja bali usingizi wake ulikuwa mithili ya gogo! Sasa nilikuwa na hakika kwamba ikiwa mimi sina wazimu, basi kiumbe yule aliyevaa ngozi iliyochakaa sana katika mpito wa miaka hakika ana wazimu. Nilitaka kuhakikisha, hivyo nilimkumbusha kwamba amelala mahali hapo kwa muda wa miaka mingi sana.
Kusikia hayo alianza kunikagua. Akasema nimevaa kizungu. Akanitajia tofauti nyingi baina ya vijana aliowazoea na mimi. Mwisho wa yote akauliza kama siku hiyo si tarehe kumi na nane mwezi wa pili mwaka wa 1897. Nikadhani anafanya mzaha kwa hivyo nikacheka.
Nilipoona kicheko changu kinamuudhi, nikamwambia siku hiyo ni tarehe kumu na nane mwezi wa pili mwaka wa 1997. Nilipoona ameshangaa kwa dhati, nikagundua ukweli.

Alikuwa amelala kwa karne nzima!.

**MASWALI**

a) Eleza hoja nne muhimu zinazojitokeza katika aya tatu za mwanzo.
(Maneno 75-85) (alama 12)

b) Kwa maneno yako mwenyewe, fupisha aya mbili za mwisho bila kubadilisha maana.
(Tumia maneno 40-50) (alama 8)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

A:

a) Jaza kiambishi kifaacho:
Ume__________ ona kalamu nyekundu ziliz_______potea?
(alama 2)

b) Andika kwa umoja
Tumewaondoleeni matatizo yenu, yafaa mtushukuru. (alama 2)

c) Nyambua vitnzi vifuatavyo ili kupata majina (nomino) mawili mawili tofauti:
(i) Kumbuka
(ii) Shona
(iii) Cheka

d) Ondoa- amba-bila kubadilisha maana. (alama 6)
(i) Kuimba ambako kulisifika siku nyingi sasa kunatia shaka
(alama 1)
(ii) Mibuni ambayo hupandwa wakati wa mvua hustawi
(alama 1)

e) Sahihisha:
Siku hizi mahitaji imezidi na pesa haitoshi (alama 1)

f) Akifisha:
Sijaona kitabu kizuri kama hiki utaniazima siku ngapi bashiri alimuliza sijaona.
(alama 4)

g) Eleza maana mbili za sentensi:
Jua nisemalo ni muhimu kwetu. (alama 2)

h) Kiambishi- U-hutambulisha majina yote ya ngeli ya U (umoja). Hata hivyo baadhi majina hay huchukua viambishi tofauti tofauti katika wingi. Orodhesha majina ma kama hayo, kisha uonyeshe viambilshi hivyo tofauti vya ngeli (Katika umoja na Wingi)

**B:**

(a) (i) andika methali nyingine yenye maana sawa na
Mwenya kelele hana neno. (alama 2)

(ii) Eleza maana ya misemo:
I Hana mwiko
II Ametia mbugi miguuni (alama 2)

b) Tunga sentensi mbili kuonyesha tofauti kati ya:
   (i) Tega
   (ii) Tenga (alama 2)

c) Eleza maana mbili kuonyesha tofauti kati ya;
   (i) Rudi
   (ii) Funza (alama 2)

d) Jumba la kuhifadhi vitu vya kale ili watu wavitazame huitwa
   (alama 2)

e) Andika kwa tarakimu;
   Nusu kuongeza sudusi ni sawa na thuluthi mbili (alama 2)

f) Jaza kiungo cha mwili kifaacho:
   i) ……………………ya jicho hurekebisha kiasi cha mwanga uingiao kwenye jicho. (alama 1)
   ii) Saa hufungiliwa kwenye………………..cha mkono (alama 1)

g. i) Mjukuu ni wa babu; mpwa ni wa…………………. (alama 1)
   ii) Tunachunga unga, tunapeta…………………….. (alama 1)

**102 1B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT./NOV.2000**
**SAA: 2 ½**

**1. UFAHAMU**
**Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali**
Nchi nyingi za ulimwengu unaoendelea, au ule uliokuwa ukiitwa ulimwengu wa ta zimegawika sehemu mbili mbili. Sehemu hizi zinazidi kutoshabihiana kila uchao zinatengana kiasi cha kukaribia kupigwa mfano wa masafa ya ardhi na mbingu. Seher zenyewe ni mijini na mashabani. Sehemu hizi, hasa ukizitia katika mizani ya hali na jia za watu za maisha, zimetofautiana mno. Kiasi cha tofauti hizi ni kikubwa hadi kuonekana kama kwamba hazina uhusiano kamwe, mithili ya nchi mbili tofauti.

Hebu sasa tuzingatie yale yana yozifanya sehemu hizi kukosa kufanana. Hapa tutawajibika kuzizingatia tofauti zilizo bayana baina ya watu wa shamba na wa mijini, hasa kufungamana na jinsi wanavyoyaendesha maisha yao.

Jambo lililo wazi ni kwamba watu wa mashambani hawajapiga hatua ya maana kuhusu jinsi wanavyuotakikana kuishi katika karne ya ishirini. Watu hawa bado wanaishi kama walivyoishi mababu zao. Hawahisi halahala ya jambo lolote. Mategemeo yao ni shamba; usubiriwe msimu mzuri wa mvua, watu walime, *Mungu* akineemeshe kilimo, wavune mavuno mema, Chakula kikiwa tayari, wale, walale, siku nyingine warudie mkondo uo huo wa kuendesha maisha yao.

Watu hawa maisha yao yamepangika mikondo mitatu tu: kuzaliwa, kuoa au kuolewa, na kufa. Zaidi ya mikondo hii, maisha ya *viumbe* hawa hayana mabadiliko makubwa.
Mabadiliko haypendelewi sana huko mashambani. Huko, wanaume ni mabwana, *wanawake ni mfano wa vijakazi na watoto hawana tofauti kubea na watwana*. Mwanume akikohoa, mkewe akimbilie kulikokoholewa, na watoto watetemeke. Wanawake wa shamba na watoto hawana haki hata ya kunena, wala hawajui haki ni nini.

Kwa upande mwingine, mijini kuna viwanda, kuna majumba, kuna magari na kuna vyombo vingi sana vya maendeleo ya kisiku izi. *Watu wa mijini ni watu wa ulimwengu kote*, wala si watu wa mji mmoja tu. Watu wa mji wowote ulimwenguni huweza kuwasiliana na wenzao wa miji mingine kokote kule ulimwenguni kwa njia ya runinga. Pia, kwa watu wa mjini, kuona kiumbe kidogo kabisa kisichoweza kuonekana kwa macho si ibura hata. Kiumbe cha namna hiyo huonekana kupitia mangala. Na kwa wale walioondokea kuwa wanajimu wa kisasa, kuziona sayari na thurea zilizoko mbali sana nasi kupitia ningala ni jabo la kawaida sana.

Watu wa mjini huwa na mabadiliko mengi sana katika maisha yao, wala sio mikondo aina tatu tu. Kwa mfano, wanawake wa mijini hawakubali tena kuonewa na wanaume. Wanajua vyema sana maslahi yao na wameiweka menke yao mbele; yaani mahali pao katika jamii, wakiwa wao ni wanawake. Kupigania haki sawa na wanaume bila kulegeza kamba. Huku kupambana kimaisha kama wapambanavyo wanaume na kufanikiwa kufanya kazi za kusikika kam vile uwakili, udaktari, uhandisi, urubani na nyinginezo zilizokuwa zikifanywa na wanaume tu. Wanawake wengine hata ni maprofesa! *Kweli watu wa mijini wameendelea.*

a) Toa maelezo kuhusu tofauti zinazosemekana ni bayana baina ya maisha ya watu wa shamba nay ale ya watu wa mijini. (alama 2)

b) Rejelea "Mungu" katika aya ya tatu na neon "viumbe" katika aya ya nne. Bainisha uhusiano uliopo baina ya manen haya mawili, hasa ukizingatia jinsi yavyotumiwa katika habari. Je matumizi haya yankupa hisia gani?
(alama 4)

c) Unadhani mwandishi ana maana gani anaposema ya kwamba huko mashambani "wanawake ni mfano wa vijakazi, na watoto hawana tofauti kubwa na watwana?"
(alama 4)

d) Orodhesha vifaa vyovyote vitano vilivyotajwa katika taarifa hii, kisha ueleze umuhimu wa kila kimoja wapo. (alama 5)

e) "Watu wa mijini ni watu wa ulimwengu kote" Hapa mwandishi anamaanisha nini?
(alama 2)

f) (i) Ni nini maana ya neon menke? (alama 1)
(ii) Mwandishi anamaliza taarifa yake kwa kusema "Kweli watu wa mijini wameendelea." Kwa muhtasari, ni tabia gani za wanamiji zilizomfanya kukiri hivyo.
(alama 2)

2. **Ufupisho**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Raha ni kitu gani? Je, ni kitu kizuri au kibaya? Mbona kila mutu hipigania na kama ionekanavyo, kila aionjaye hatimaye humwunguza? Au pengine wako wengine wasiooungua? Hebu basi tuzingatie wale wasemekanao huitafuta sana raha na, penginepo wakafanikiwa kuipate.

Chukua mfano wa msichana na mvulana wapendanao. Hawa wawili wanapopendana, lengo lao huwa ni kuoana na wakishaoana, waishi raha mustarehe milele na milele. Hata hivyo, jambo la kwanza ni kwamba, hata kabla hawajaoana, wanadhikika na kudhikishana kwa kutaka sana kuaminiana si mara haba wakati wakiwa wapenzi mar. Mara kadha wa kadha husameheanana kuendelea na mapenzi. Baadaye wakiwa na bahati, huona.

Mara tu wanapooana hugundua kuwa huko kuishi raha mustarehe ilikuwa ni ndoto tu ya ujana iliyotengana kabisa na uhalisia. Uhalisia unapowabinikia huwa ni kuendelea na huko kudhikishana,kutoridhishana, kutiliana shaka, kuombona mamaha na kuendelea tu.
Ama tumwangalie mwanasiasa. Huyu anapigania usiku na mchana ili awe mjumbe. Mwisho anachanguliwa, lakini afikapo bunge, anakuta hakuna anayemtambua kama bwana mkubwa. Inambainikia kwamba ubawana- Mkubwa hautegemei kuchaguliwa tu, bali unategemea mambo mengine pia, kama vile pesa nyingi, magari makibwa, sauti katika jamii na wadhamini wanotambulikana. Raha kwa mwanasiasa huyu inakuwa mithili ya mazigzi tu, "maji" uyaonayo kwa mbali wakati una kiu kali sana, kumbe si maji bali ni mmemetuko wa jua tu.

Mwingine wa kupigiwa mfano ni msomi. Huyu huanza bidii yake akiwa mdogo sana. Lengo lake huwa ni atambuliwe kote kwa uhohadri wake katika uwanja wa elimu. Basi mtu huyu husoma mpaka akaifikia daraja ya juu kabisa ya usomaji. Akapata shahada tatu: ya ukapera, ya uzamili nay a uzamifu. Akajiona yu upeoni mwa ulimwengu. Akatafuta kazi akapata. Kisha akagundua kwamba watu hawakijali sana kisomo chake. Wakamwona ni kama mwehu tu.

Fauka ya hayo wakamlumu kwa kupoteza muda wake mwingi kupekuapekua vitabu. Wakamfananisha na mtu mvivu.

Mwisho tuangalie mfano wa mwanamuziki . Huyu anahaghaika na wazo la kwamba sauti yake ikiwaonga watu, atapendwa sana na wengi na kuwazuzua wengi kama mbalamwezi au kuwaongoza kama nyota. Mtu huyu anapofikia kilele cha malengo yake hata husahau kama ni binadamu wa kawaida, akawa anaishi katika muktadha wa watu kuzirai kwa sababu ya akili kujawa pomoni na upungaji wake. Watu hutamani hata kumgusa tu. Hata hivyo, mtu huyu huishis kujisikia mkiwa pale wakati unapowadia wa kupumzika. Je, raha yote huwa imekimbilia wapi?

a) "Mapenzi ni kuvumiliana." Kwa maneno yako mwenyewe, eleza jinsi msemo huu ulivyo muhtasari mwafaka way a pili nay a tatu ya habari hii. (Maneno 30-35) (alama 8)

b) Kwa muhtasari, raha ni "asali chungu. "Fafanua dai hili huku ukirejelea mwanasiasa, msomi na mwanamuziki (maneno 45-55) (alama 12)

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

A.

a) Eleza tofauti iliyopo katika jozi hii ya sentensi. (alama 2)
Alimpatia soda ya chupa
Alimpatia soda kwa chupa.

b) Kamilisha jedwali ukifuatia mfano uliopewa (alama 4)

| | | |
|---|---|---|
| Wimbo | Mwimbaji | Uimbaji |
| Jengo | ……………. | ………. |
| Pendo | ……………. | ………. |

c) Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi; kisha ueleze ni vielezi vya aina gani (alama 4)
(i) Aliamka alfajiri
(ii) Mtu huyu ni hodari sana

d) Andika kwa msemo halisi
Yohana alisema kwamba njiani kuliwa kumenyesha sana ndio sababu tulichekelewa (alama 2)

e) Tunga sentensi moja moja ukitumia alama zifuatazo za uakifishaji
(i) Ritifaa
(ii) Parandesi
(iii) Dukuduku
(iv) Mshangao.

f) Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya vitenzi vya silabi moja katika jinsi ya kutendesha ukitumia silabi hizi (alama 3)
(i) -la
(ii) nywa
(iii) fa

g) Taja na ubainishe aina za viwakilishi katika sentensi zifuatazo (alama 4)
   (i) Ile minazi yangu niliyopalilia inakua vizuri
   (ii) Mimi ninataka kumwona mwanariadha aliyepata nishani ya dhahabu

h) Andika kwa wingi:
   (i) Uta wake ni mrefu na mkubwa sana (alama 2)
   (ii) Merikebu itayokayofika kesho itango'a nanga kesho kutwa. (alama 2)

i) Andika upya sentensi zifuatazo ukitumia neon amba
   (i) Kijiti kilichovunjika kilimwumiza Amina guu (alama 2)
   (ii) Barua zitakazoandikwa na baba kesho zitatumwa mwaka ujao.

j) Sahihisha sentensi hizi:
   (i) Bahasha ilionunuliwa jana ni kubwa na mzuri (alama 2)
   (ii) Mananasi hizi zinauzwa ghali kwa sababu zimeiva vizuri sana (alama 2)

**B:**

a) Tunawaitaje watu hawa? (alama 2)
   (i) Mtu anayebeba mizigo kwa ujira
   (ii) Mtu anayeshughulikia elemu ya nyota

b) Taja methali inayoafikiana na maelezo haya:
   i) Wengine wanapoozana na kugombana, kunao wanaofurahia kabisa hali hiyo.
   ii) Afadhali kuhudhuria huo mkutano hata kama umechelewa (alama 2)

c) Tunga sentensi tatu zikionyesha maana tatu za neon chungu (alama12)

d) Kamilisha:
   i) Bumba la ……………………..
   ii) Genge la…………………….. (alama 2)

e) Eleza maana ya:
   i) Juhudi zake hizo si chochote bali ni kutapatapa kwa mfa maji
   ii) Leo kapasua yote, hata mtama kamwagia kuku.

**102 1B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT./NOV.2001**
**SAA: 2 ½**

1. **UFAHAMU**

**Soma makala afuatayo kisha ujibu maswali yanafuata.**

Katika falme ya Pate ya enzi za kale, kulikuwa n binti Sultani aliyeitwa Mwanakishwira. Alipopata umri wa miaka kumi na mine tu, Mwanakishwira alikuwa tayari ni mrefu na mkubwa, na alionekana kuwa msichana mzima mwenye umri wa miaka kumi na minane. Alikuwa nadhifu na mzuri sana wa sura, kiasi cha kubandikwa lakabu ya malaika.

Lipendeza sana macho *fauka* ya kuwa alikuwa na akili nyingi mno. Katika umri huo, alikuwa amemaliza masomo yake yote katika madrassa iliyokuwa hapo, na aliweza kuikariri. Kurhani yote bila kigezigezi. Babake, Mfalme, aliuma videole akilia ngoa kuwa motto mwenye akili hiyo ni mke wala sio mume. Aliwaza ya kuwa kama angekuwa mvulana, angempeleleka zutafindaki ya Al-Azhar huko Misri kuendelea na masomo ya juu katika chuo hicho kisifika.

Wakati mfalme akiuma vidole kuhusu junsia ya motto wake, wanaume wengi hapo mjini walikuwa wakimeza mate. Mtu aliyememezewa mate alikuwa ni yeye huyo Mwanakishwira. Walimmezea mate kwa sababu kila mmoja wao alitaka kumwoa awe mkewe. Kumwoa Mwanakishwira kulikuwa na manufaa ya kupata mke mwenye uzuri wa shani, kama nyota, na aidha kuwa Mfalme baada ya mwenye kukikalia kuaga dunia, sababu yeye hakuwa na mrithi mwingine.

Basi ikawa ni kila mtu kujipendekeza kwa mfalme…Kila mtu bila kujali nasaba. Walijipendekeza wakwasi na mwakata pia. Mwisho Mfalme, Kwa vile alikuwa anasumbuliwa sana, na wakati huohuo aliogopa kuwa asipomwoza mapema binti yake huenda akaharibika, akaamua kuruhusu wachumba wamchumbie.

Uamuzi huu ulimshtua sana Mwanakishwira, Mshutuko aliopata ulimtia ugonjwa na kumdoofisha kabisa. Akadhoofu hadi Mfalme akaingiwa na hofu ya kuwa motto wake atakufa. Akaamua kumwuliza kinachomdhoofisha. Mwanakishwira. Mwanakishwira akasema kimdhoofishacho ni mwezi. Akipata mwezi, na nafuu pia ataipata.

Kusikia hivyo, Mfalme akatokwa na kijasho chembachemba. Akafikiria kwamba labda motto wake amemalizwa kabisa na uwele, na sasa yaweweseka tu, wala hana akili razini ya kutambua na kupanga mambo.

Hata hivyo hakuvunkika moyo kabisa. Akaamua kupata tafsiri ya kitendawili hicho kutoka kwa waheshimiwa wake hapo mjini. Ambao wote walitaka mumwoa Mwanakishwira.

Kwanza akamwendea Waziri Mkuu akamwulia tafsiri ya mwezi autakao binti yake. Waziri akasema mwezi utakikanao ni wa dhahabu. Alipoambiwa hivyo motto akzidi kudhoofu. Mfalme akakasirika sana. Akawaendea wakwasi wengine kama vile Kadhi, Mnajimu na Kadhalika. Hawa wote wakamzidisha ugonjwa binti Mfalme kwa sababu jawabu walizotoa ni kuwa mgonjwa alihitaji mwezi wa almasi, fedha na hata hatua!

Mwisho kabisa, Mfalme akamwendea Mvulana aliyeckuwa mchungaji. Huyu akamwaidhi Mfalme kwamba aulize mgonjwa aseme mwenyewe aina ya mwezi aitakayo. Jawabu hili halikumfurahisha Mfalme, japo alienda kamwuliza binti yake, kama alivyoambiwa. Alipoulizwa Mwanakishwira

akasema mwezi autakao ni kishaufu kilicho na umbo la mwezi mchanga kilichotengenezwa na chuma. Mfalme alishangaa sana, Hata hivyo akamfulia kisaufu alichokitaka mgonjwa. Alipokivaa, Mwanakishwira akapata nafuu mara moja na akaendelea na nafuu hiyo hadi akapona kabisa.

Kuona hivyo, Mfalme akawateremsha vyeo wakwasi wote humo mjini, na kuteua wengine mahali pao. Kwa upande mwingine, mchungaji akaozwa binti Mfalme na kupewa madaraka ya Waziri Mkuu. Hatimaye, Mfalme alipoaga dunia, mchungaji akawa Mfalme na Mwanakishwira akawa Malkia.

a) Zungumzia swala la meuke (yaani mahali pa mwanamke au mwanamume katika jamii) katika falme ya pate ya enzi hiyo. (alama 5)

b) i) Kwa nini Mfale iliwauliza wakwsi kwanza tafsiri ya kitendawili (alama 2)
ii) Kwa nini mfalme alishangazwa na jawabu la binti yake? (alama 2)

c) “Akili ni nywele, kila mtu ana zake” Dhihirisha jinsi methali hii inavyobainika katika hadithi hii (alama 4)

d) Ni nini maoni yako kuhusu mwanamume aliyemwoa Mwanakishwira na kwa nini alikubali kuolewa na huyo? (alama 3)

e) Eleza maana ya maneno na tamathali za semi zifuatazo (alama 4)
i) Fauka ya kuwa
ii) Akilia ngoa
iii) Uzuri wa shani
iv) Akamwaidhi

2. **UFUPISHO**

Yusufu Bin Hassan, Mfalme wa mwisho wa halali wa Mombasa, alijitayarisha kuihama himaya yake. Alikuwa amewashinda Wareno, mahasimu wake, vibaya, lakini alijua watarudi na watamwadhibu vikali. Hivyo basi, badala ya kusubiri waje wazitie baruti nyumba na kuzilipua, badala ya kungojea waje wawachinje raia wake kama kuku, badala ya kungonja ashuhudie minazi yote kisiwani na miti mingine ya manufaa kukatwa katwa na makatili hao, badala ya kujitayarisha yeye mwenyewe mji, faua ya kuikatakata miti yote ili Waareno wakija wasikute chochote cha kuvutia macho na watokomee kabisa. Alijua asipotekeleza uamuzi huo mkali, basi Wareno watakujja na hasira zote na kuadhibu waliomo na wasiokuwemo, kama walivyofanya Faza.

Unyama uliofanyika huko alikuwa ameusikia ukisimuliwa mara zisizohesabika. Katika masimulizi hayo, alikuwa amesikia ya kwamba Falme hiyo ya Faza ilipoasi utawala wa Kireno, askari wa Kireno, chini ya uongozi wa Martin Affenso de Mello, walifanya unyama hapo mjini Faza ambao ulikuwa haujawahi kutokea, hata katika mawazo. Inavyosemekana ni kwamba Wareno waliamua kuangamiza chochote chenye uhai, hata wanyama na miti na wakautimiza muradi wao. Ajabu ni kwamba, hata kasisi aliyeheshimika sana wa Kireno enzi hizo, Baba Joao dos Santos, aliunga mkono tukio hili akisema ya kwamba wafaza walistahili kuadhibiwa. Hakuna mtu hata mmoja upande wa Wareno aliyekilaani kitendo hiki cha kutisha.

Hii ndiyo sababu Mfalme Yusuf na raia wake walipowazima wareno hapo Mombasa, aliwaamuru watu wajitolee kuwashabulia kwenye vituo vyao vyote kaitika mwabao mzima wa mashariki ya Afrika. Baada ya kuamua hivyo, alienda Uarabun kutafuta silaha ili atekeleze azimio lake.

Alipopata zana za kutosha, ikiwa ni pamoja na silha na meli, alianza kupambana na wareno kuo huko Arabuni, mahali pitwapo Shihr.  Halafu alielekea mwambao wa pwani ya AFrika aliwasumbua sana maadui zake, Mwisho alikita makao yake Bukini ambako aliendelea kuwashambulia Wareno kokote walikokuwa.

a) Eleza sababu zilizomfanya Mfalme Hassan kuuangamiza mji wake, na halafu kuuhama (maneno 30-40) (alama 8)

b) Ukitumia Maneno yako mwenyewe na bila kupoteza maana, fupisha kuanzia aya ya pili hadi mwisho wa kifungu (maneo 75-80) (alama 12)

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

1. a) Kwa kutumia kirejeshi kifaacho, rekebisha sentensi ifuatayo kwa njia mbili tofauti.
   Yule ndiye mkwasi ambaye aliyenusurika. (alama 2)

   b) Andika umoja wa sentensi hizi:
      (i) Kwato za wanyama hutufaidi
      (ii) Mnataka vyeti vya kuwasaidia? (alama 2)

   c) Andika ukubwa wa
   Mwizi aliiba kikapu na ngo'mbe (alama 2)

   d) Tunga sentensi sahihi ukidhihirisha wingi wa majina yafuatayo:
      i) Ukanda
      i) Uzee

   e) Sahihisha sentensi zifuatazo bila kugeuza maana
      i) Kikombe chenye kimevunjika ni kipya (alama 1)
      ii) Nimepeana kitabu kwa mwalimu mkuu (alama 1)

   f) Tunaweza kusema katika chumba au
      i) …………………………………………………..ama
      ii) ……………………………………………………..

   g) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya kutendewa
      i) Yule Ngo'mbe alizaa ndama mkubwa jana
      ii) Mavu hawa wamemsumbua Nyatogo kwa mda mrefu.

   h) Kwa kurejea ngeli za mahali, andika sentensi tatu ukionyesha matumizi ya kila moja
      i) Andika sentensi za mseto kutokana na mbili fupi ulizopewa
      a) Mwanafunzi amesoma kwa bidii.  Mwanafunzi anataka kupita mtihani (alama 1)
      b) Leo nimerudi nyumbani. Sipendelei kuishi hapa (alama 1)

   j) Geuza sentensi hizi kutoka msemo wa taarifa hadi msemo halisi
      i) Mama alisema nichukue nafaka yetu nikauze sokoni (alama 2)

ii) Mwalimu aliomba aletewe vitabu vyake kutoka darasani (alama2)

k) Eleza maana mbili tofauti za sentensi hii:
Wenzake wamelipwa pesa zao, yeye bado amelala.

I) a) Eleza Katika sentensi maana ya misemo ifuatayo;
(i) Uso wa chuma (alama 1)
(ii) Kuramba kisogo (alama 1)

b) Andika visawe (maneno yenye maana sawa) vya maneno haya
i) Sarafu (alama 1)
ii) Kejeli (alama 1)
iii) Daktari (alama 1)

Kwa kila jozi ya maneno uliyopewa, tunga sentensi mbili kutofautisha maana.

c) i) Ini
Hini (alama 2)

d) Andika kinyume cha
i) Shari (alama 1)
ii) Oa (alama 1)

e) i) Anayefundisha mwari mambo ya unyumba hutwa (alama 1)
ii) Samaki anayejirusha kutoka majiri huitwa (alama 1)

**102 1B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT./NOV.2002**
**SAA: 2 ½**

1. **UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Kati ya viumbe wote waishio ulimwenguni, hakuna kiumbe aliyepevuka mawazo kama binadamu. Kiumbe huyu amewapiku wale wengine kwa njia nyingi, hata kuweza kuwatawala na kuwapangia maisha yao. Binadamu amekirimiwa uwezo wa kuyatawala mazingira na kukabidhiwa hekima ya kuweza *kusana* ala mbalimbali ili kuyakabili mazingira hayo. Hekima hii humwezesha kusitiri kizazi chake.

Aidha, ametunukiwa uwezo mkubwa wa kuivinjari sayari hii yetu katika ilhamu yake ya kutaka kuvumbua 'siri' za maumbile, amejasiri hata kuzitalii sayari nyingine nje ya uso wa ulimwengu huu. Si ajabu kwamba iwapo wanyama wengine wangepewa urazini wa kuongea kama yeye, wangalimwandikia tumbi la vitabu kusiuf busara yake. Sifa za ujasiri wake kamwe hazingewatoka vinywani mwao!

Hata hivyo, kuna tofauti nyingine kubwa kati ya binadamu na hayawani, Tofauti hii inaweza kumvua binadamu sifa zake zote na kuuona ukwasi wa maarifa yake kama ishare ya maangamizi ya ulimwengu. Hii ni kutokana na hasara anayosababisha katika mazingira tulivu walivyoumbiwa viumbe wote.

Uzuri wa ulimwengu tunamoishi humpendeza kila kiumbe hata yule anayemchukia binadamu kama nzi. Wote hufurahia mazingira yao; hewa safi itokayo milimani, chemichemi, mito na vijito mnamotiririka maji safi, vilele vya milima vilivyokumbatiwa na theluji daima dahari, yakiwemo mabonde na tambarare zinazohimili uhai wa viumbe wengi.

Urembo huo wa kiasili hauwezi kukamilika bila vichaka na misitu inayoipamba sayari hii huku ikileta mvua. Mapambo yote haya huendeshwea na nguvu za maumbile; nguvu ambazo hazisababishwi na kuwa hatari kwa uhai wake na ule wa viumbe wenzake kwa sababu anayaharibu maumbile kwa kiasi kikubwa kinachomtisha yeye mwenyewe. Hii ni kwa sababu gani? Sababu zipo nyingi.

Sababu mojawapo ni uchafuzi wa maji kama rasimali muhimu ya kiasili. Uchafuzi huu umewaletea viumbe na mimea maafa mengi, yakiwemo maradhi mbalimbali. Kwa kweli bila maji, uhai utatoweka duniani. Uharibifu mkubwa wa maji machafu yenye sumu hasa kutoka viwandani na kuingia kwenye mito na bahari, huwadhuru biumbe wengine ambao makao yao ni majini. Maji huleta madhara si tu kwa mimea bali hat kwa binadamu kupitia kwa ulaji wa vyakula.

Misituni rasilimali nyngine inayokimu viumbe, lakini binadamu anaiponza. Ukataji wa miti kiholela hasa kwenye sehemu za chmichemi husababisha uhaba wa mvua. Uhaba huo nao huleta kiangazi kinachokausha mimea na visima vya maji. *Mchapuko* wa ujenzi wa viwanda hasa katika nchi zilizostawi wanasayansi wanaohusika na hali za anga umesababisha taharuki na wasiwasi mwingi. Hii ni kwa sababu umenyosha kuwa ule utandu unaozuia miale ya jua kupenya moja kwa moja kweye sayari hii na juhatarisha uhai, sasa unaanza kutoweka taratibu. Hii ni kutokana na hewa chafu itokayo viwandani. Kwa kadri binadamu anavyozidi kujiimarisha kiviwanda ndivyo ambavyo mabaki yaviwanda yanavyozidi hatua hii, ni binadamu atakuwa amechangia pakubwa katika kutowesha uhai wa viumbe wote ulimwenguni.

Mikutano mingi ya kmataifa imefanywa nab ado inaendelea kufanywa kila uchao ili kutahadharisha umma wa ulimwengu dhidi ya uharibifu wa mazingira na mali asili. 'Ajenda' za mikutano hiyo hasa zinalenga nchi zilizostawi kwani hizi ndizo zinazochafua mazingira kwa kasi zaidi kuliko zile zinazostawi . Mapendekezo mengi yametolewa katika vikao hivyo ili kusuluhisha tatizo hili lakini ni hatua chache mno zinazochuliwa kurekebisha mamba.

Inatupasa sisi wenyewe kuchukua jukumu la kusafisha mazingira yetu. Tuwafunze pia watoto wetu kuhifadhi mazingira yanapochafuliwa au kuharibiwa. Tukumbuke kuwa *Mwana hufuata kisogo cha nina*.Mazingira yanpochafuliwa au kuharibiwa, afya zetu zimo hatarini, na hali hii pia ni tisho kwa viumbe wengine, hata vimatu! Kila mmoja wetu anawajibika kutunza mazingira anamoishi kwa manufaa yetu sote na kwa vizazi vijavyo.

a) Kulingana na taarifa hii, kwa nini binadamu anahesabiwa kuwa na uharibifu mkubwa kushinda wanyama wengine? (alama 4)

b) Onyesha uhusiano uliopo baina ya maendeleo ya binadamu na uharibifu wa mazingira. (alama 4)

c) Ni kwa nini mwandishi anahofia zaidi athari za miale ya jua? (alama 2)

d) Eleza kwa ufupi hasara zinazoweza kusababishwa na uharibifu wa mazingira. (alama 2)

e) taja hatua mbili ambazo mwanadamu angeweza kuchukua ili kupunguza madhara ya viwanda. (alama 2)

f) Kulingana na makala haya ni nini maana ya methali "mwana hufuata kisogo cha nina?" (alama 1)

g) Eleza maana ya
   (i) Kusana (alama 2)
   (ii) Mchapuko (alama 2)

2. **MUHTASARI**

Vipindi mbalimbali vya historia vimeshuhudia kuibuka kwa magonjwa ya ajabu. Magonjwa hayo yame wahangaisha watu na kuzishughulisha bongo za wanasayansi na madaktari katika kutafuta tiba. Mgonjwa kama vile tauni, kifua kikuu, homa ya matumbo na ndui ni baadhi ya yale yaliyotisha sana nyakati Fulani za historia ya binadamu. Magonjwa haya yaliwaua maelfu ya watu na kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu.

Hata hivyo, magonjwa hayo yaliweza kuchuzwa na kutafutiwa tiba kabla ya kumaliza kabisa kizazi cha binadamu . Lakini hii ni baada ya kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. Ulimwengu wa sasa umashuhudia janga lingine la maradhi sugu ya ukimwi. Neno "**UKIMWI"** lilitolewa katika na athari za ugonjwa huo mwilini. Neno "**UKIMWI"** humaanisha *ukosefu wa Kinga Mwilini*, ambapo herufi za maneno matatu ziliunganishwa pamoja na kuunda neno hilo.

Ugojwa huu ambao tayari umewaua mamilioni ya watu wtu kote ulimwenguni unazidi kuenea kwa kasi, mfano wa moto katika kichaka. Kutoka kasi yake ya kuua watu, ugonjwa wa **UKIMWI** umepewa majina kama vile "umee" na pia 'ugonjwa wa vijana.' Watu wengi wanaoabukizwa, virusi vya **UKIMWI** umepewa majina kama vile "umeme " na pia 'ugonjwa wa vijana. Watu wengi wanaombukizwa virusi vya **UKIMWI** ni wale walio na miaka kati ya 15 hadi 49. Kundi hili kwa kweli ndilo, linalohesabiwa kuwa na nguvu za kutunza jamii kwa njia nyingi iwapowengi katika kundi hili watakumbwa na maradhi haya, watasalia wakongwe na watoto wachanga wasioweza kujimudu.

Nchini Kenya **UKIMWI** uligunduliwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1984. Kufika mwezi wa Juni 1996, inakisiwa kuwa ugonjwa huu ulikuwa umewaua watu wapatao 65,647 nchini. Hivi sasa, imesemekana kuwa takrban watu zaidi ya 500 hufa kila siku nchini Kenya kutokana na janga hili. Aidha imethibitishwa kwamba takribani watu milioni mbili u nusu tayari watapoteza maisha yao kutokana na kuambukizwa virusi vya ugonjwa huu humu nchini. Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa.

Kutokana na kuongezeka kwa visa vya **UKIMWI**, hospitali na zahanati nyingi kote nchini zinashindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa. Kwa hivyo makundi ya kujitolea na mashirika mbalimbali yameundwa ili kuwahudumia wagonjwa wa **UKIMWI**. Baadhi ya makundi hayo hutoa tiba ya kisaikolojia pamoja na kuwapa ushauri wa hima ya kuishi, badala ya kukata tama. Wagonjwa wengi pia huishia kutibiwa nyumbani kwao.

Ugonjwa huu umeathiri jamii kwa njia nyingi. Hali ya wasiwasi na woga, ukosefu wa matumaini, ongezeko la mayatima na kuzorota kwa uchumi kutokana na kutoweka kwa kizazi chenye nguvu za kutoa, huduma kwa jamii, ni baadhi ya athari za maradhi haya.
Lakini jambo la kuzingatia ni hili, tujifunze kutokana na historia. Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba ya ugonjwa huu itapatikana. Hii ni kwa sababu tumethibitishiwa haya kutoka katika historia yetu wenyewe. Ikiwa magonjwa yaliyasababisha vifo vya wengi kutokana na ukosefu wa tiba yalitokomezwa kupitia juhudi za kimatibabu, sembuse huu ugonjwa tulio nao sasa? Huku tukijikinga kutokana na maradhi haya, tusife moyo bali tuwe na matumaini kwani subira huvutia heri.

a) Kwa kutumia maneno yako mwenyewe na bila kupoteza maana, fupisha aya nne za mwanzo (maneno 90-100) (slsms 3 kwa mtiririko) (alama 4)

b) Eleza mambo yanayoleta matumaini kwa wagonjwa wa UKIMWI kulingana na aya tatu za mwisho. (Maneno 40-50)(alama 1 kwa mtiririko) (alama 4)

## 3. MATUMIZI YA LUGHA

1. a) Eleza matumizi matatu ya KI na utunge sentensi moja kwa kila mojawapo. (alama 6)

   b) Tambulisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo, halafu uzigeuze sentensi hizo kwa wingi.
   (i) Nilisoma kitabu chake
   (ii) Umekuwa mwadilifu kupindukia
   (iii) Alishinda nishani ya dhahabu (alama 6)

   c) Akifisha sentensi hii:
   Watu wengi wamezoea kusema ajali bwana basi yakaishia hapo lakini kufanya hivyo ni sawa. (alama 3)

   d) Andika sentensi hizi kwa umoja
   i) Mafuta haya yanachuruzika sana (alama 2)
   ii) Miinuko ile ndiyo mwanzo wa milimu ya Chungu. (alama 2)

   e) Sahihisha sentensi zifuatazo (alama 2)
   i) Kile kitabu kilipasuka ni changu
   ii) Matofali haya yanatumiwa kwa ujenzi wa nyumba

g) Andika sentensi hizi upya ukitumia o-ote. (alama 3)

i) Chakula kikibaki hutupiliwa mbali
ii) Kila nyumba unayoingia unapata watoto wawili

h) Yapange majina yafuatayo katika ngeli zake (alama 3)

i) Neno
ii) Kiongozi
iii) Mate

i) Ukizingatia nenolililo katika mabano, andika sentensi hizi atika hali ya kutendeka. (alama 2)

i) Daraja hili (vuka) tu wakati wa kiangazi.
ii) Kitabu hicho (soma) ijapokuwa sura zingine sura zingine hazimo.

j) Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya (alama 2)

i) –enye
ii)-enyewe

I) a) Tunga Sentensi zitakazobainisha maana ya jozi za maneno zifuatazo: (alama4)

i) Mbari
Mbali
ii) Kaakaa
Gaagaa

b) Tumia misemo ifuatayo katika sentensi; (alama2)

i) Enda nguu
ii) Chemsha roho

c) Eleza maana mbili tofauti za (alama 2)
Rudi

d) Eleza maana ya methali
Ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni (alama 2)

**1021B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT./NOV.2003**
**SAA:2 ½**

1. **UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu mwsawali**

Utandaridhi (au globalization kwa lugha ya Kingereza) ni jinsi ya maisha inayoendelea kuutawala ulimwengu wote katika karne hii ya 21. Neno utandaridhi ni neno mseto ambalo maana yake ni utamaduni uliotanda au kuenea ardhi nzima. Mtu mtandaridhi' hivyo basi ni mtu aliyebebea kikamilifu katika utamaduni huu mpya kwa jinsi moja au nyingine.

Matandaridhi hujihusisha sana katika kutandaridhisha aina moja au nyingine ya *amara* muhimu za kitandaridhi. Hizo ni kama vile biashara za kumataifa, lugha za kimataifa, aina za mavazi zilizotokea kupendwa ulimwenguni kote, muziki wa kisiku hizi, hasa vile pop, reggae, raga, rap, ambao asili yake ya hivi majuzi ni Marekani. Muziki huo waimbaji wake hutumia, sana sana, lugha ya Kiingereza hususan kile cha Marekani na kadhalika Watandaridhi wana nyenzo zingine kadha wa kadha za kuendeshea maisha yao au kujitambulisha. Wao huwasiliana kutoka pembe moja ya duni hadi nyingine wakitumia vitumeme, yaani vyombo vitumiavyo umeme kufanya kazi vya hali ya juu, kama vile tarakilishi na simu, hata za mkono. Watu hawa hawakosi runinga sebuleni mwao, usiseme redio. Hawa husikiliza na kutazama habari za kimataifa kupitia mashirika matandaridhi ya habari kama vile BBC la uingereza CNN la marekani. Aidha watu hawa husafiri mara kwa mara kwa ndege na vyombo vingine vya kasi. *Hawa hawana mipaka*. Wale wanaohusudu utandaridhi wanaamini kindakindaki kwamba utamaduni huu wa kilimwengu umeleta *mlahaka* mwema baina ya watu binafsi, makampuni makubwa makubwa ya kimataifa na usiano bora baina ya mataifa. Watu hawa husikia wakidai ya kuwa aina hii ya utamaduni imeupigisha mbele ustaarabu wa wanadamu ulimwenguni kote. Kwa upande mwingine, *wakereketwa* wa tamaduni za kimsingi za mataifa na makabila mbalimbali ulimwenguni wanadai ya kwamba utandaridhi umeleta maangamizi makubwa ya tamaduni hizo. Kwa ajili hiyo basi, utandaridhi umeleta maangamizi makubwa ya tamaduni hizo. Kwa ajili hiyo basi, utandaridhi umesemekana kwamba unasababisha kutovuka kwa utu miongoni mwa wanadamu wote, ambao wamo mbioni kusaka pesa na kuneemesha ubinafsi. Inadaiwa pia kwamba utandaridhi umesababisha kutovuka kwa adab kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu. Huku kutovuka kwa adabu kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu. Huku kutovuka kwa adabu kwa vijana, hasa wale wa mataif yanayojaribu kuendelea, kumeleta zahama *chungu mbovu*, ikiwa ni pamoja na kuenea kwa **UKIMWI** kwa kasi ya kutisha.

a) i) Bainisha kwa kutoa maelezo kamili kwamba utandaridhi ni neno mseto. (alama 3)

ii) Tohoa maneno mawili kutokana na neon kutandaridhisha kisha ueleze maana za maneno hayo. (alama 2)

b) i) Nini maana ya 'hawa hawana mipaka?' (alama 3)

ii) Kwa nini watandaridhi wanpenda kusikiliza na kutazama habari kupitia BBC na CNN?

c) i) Eleza kikamilifu maoni ya watandaridhi kuhusu utamaduni wao (alama 3)

ii) Je, Utandaridhi unalaumiwa kwa nini katika kifungu hiki? (alama 3)

d) Msemo: " chungu mbovu" ni msemo wa kimtaani tu. Msemo sawa ni upi (alama 1)

e) Eleza maana ya maneno yafuatayo

i) Amara

ii) Mlahaka

iii) Wakereketwa (alama 3)

2. **UFUPISHO**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Ukiwa mtoto unadhani ulimwengu ni kipande kimoja cha keki kilicho kitamu mithili ya asali. Hakuna dhiki, hakuna mateso, hakuna kuhuzunika kwa aina yoyote. Neno huzuni linasikika masikioni kama neno lisiloelekea kwenye uhalisia wowote. Kwa watoto dunia imejaa raha, starehe na vicheko visivyoisha. Maisha ni ahadi njema, yenye matokeo ya kufurahisha na kustarehesha tu, sio **KUDHIKISHA NA KUHUZUNISHA.**

Huyu tunayemzumgumzia hapa ni mtoto mdogo ambaye hajajua kubainisha kitendekacho mkono wake wa kushoto na kile kinachofanyika hasa katika mkono wake wa kulia. Hata hivyo, jinsi mtoto anavyoendelea kukua na kufahamikiwa na mambo, vigambo na kadhia zinazoendelea katika mazingira yake, anabainikiwa na mengi machungu ambayo huleta huzuni, sio raha.

Hebu tuanze na nyumbani kwao mtoto. Aghalabu, watoto wote hupendwa kwao nyumbani, iwapo wazazi wao ni watu wangwana na wana nafasi ya kulea watoto wao bila taabu. Hata hivyo watoto huchapwa pale wanapokuwa watundu, jambo ambalo huwahuzunisha sana, japo ni wajibu wa wazazi sababu, kama isemwavyo, mcha mwana kulia hulia yeye. Pili, inajulikana wazi kwamba watoto wengi siku hizi huenda shule, huko shule, wao hupendelea sana kucheza kuliko kusoma. Ili wasome kama inavyotakikana, ni sharti waelekezwe barabara katika njia hiyo na walimu wao. Katika kuelekezwa huku, walimu wanaweza kulazimika kuwaadhibu, hasa wale watoto ambao huzembea na kutofanya kazi zao wanazopewa kufanya nyumbani kama kawaida ya mfumo wa shule ilivyo. Watoto ambao huzembea na kutofanya kazi zao wanazopewa kufanya nyumbani kama kawaida ya mfumo wa shule ilivyo. Watoto wa aina hii wanapotiwa adabu raha hujitenga na huzuni huwatawala.

Huzuni, hivyo basi, inaonekana ya kuwa ni uso wa pili katika maisha ya mwanadamu, uso wa kwanza ukiwa raha. Na kwa hakika wanaohuzunika si watoto peke yao. Kila mtu duniani ni sharti, katika wakati mmoja au mwingine, azongwe na huzuni. Inajulikana wazi kwamba wanadamu wote hawapendi huzuni asilani na hakika kabisa, kila binadamu huchukia huzuni na kustahabu raha. Hata hivyo, raha humjia binadamu kwa nadra sana, ilhali huzuni humvamia wakati wowote, hata akiwa humo katikati ya kustarehe. Si tu, inajulikana dhahiri shahiri kwamba hakuna mtu asiyewahi kuonja huzuni, japo wapo watu wengi kweli kweli wasiowahi kuonja raha maishani mwao.

Zingatia mtoto anaezaliwa, halafu wazazi wake wanaaga dunia, pengine katika ajali, kabla mtoto mwenyewe hajaweza kujikimu. Mtoto huyu anaishi kutegemea jamaa za wazazi wake. Watu hawa wasipokuwa na nafasi wao wenyewe kimaisha pamoja na ukarimu unaohitajika basi mtoto anateseka na kuhuzunika sana katika maisha yake yote. Ama zingatia mtoto anayetupwa na mamake kijana, aliyempata bila kupanga. Hata mtoto huyu akiokotwa na kulelewa na wahisani, maisha yake yatakuwa ya taabu, dhiki na huzuni. Au zingatia mtoto anayelelewa na mama wa kambo anayeondokea kuwa mwovu. Mtoto huyu atakayoijua ni huzuni tu. Ama zingatia mtoto ambaye babake ni mlevi na unalojua ni kurudi nyumbani kufurahia kupiga watoto wote na mama yao ndipo apate usingizi mnono. Mtoto mwenye baba wa aina hiyo atakayoijua ni huzuni tu, sir aha asilani.

2. a) Ukitumia maneno yako mwenyewe na bila kupoteza maana, fupisha aya nne za mwanzo (Maneno -100) (alama 10)

b) Ukizingatia aya ya mwisho, eleza hali mbalimbali zinazowatia watoto huzuni. (Maneno 40-45) (alama 6)

**3. MATUMIZI YA LIGHA**

a) i) Tumia viashiria vya kutilia mkazo katika sentensi zifuatazo
   i) Kibogoyo………. Ndiye anayehitaji meno ya dhahabu.
   ii) Vyakula……………mvipikavyo nyinyi, nasi twavipika
   (alama 2)

b) Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya umoja
   i) Huku kuimba kwenu kuzuri kutawapendez wageni (alama 1)
   ii) Hii miche ni mizuri sana, itatufaa (alama 2)

c) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia viunganishi vifaavyo.
   i) Chakula hiki hakina mchuzi. Hakina chumve (alama1)
   ii) Romeo aliamka. Alitazama saa yake
   Akala kiamsha kinywa mbio mbio (alama 2)

d) Ziandike upya sentensi zifuatazo kwa kufuata maagizo uliyopewa.
   i) Nimemleta paka ili aue panya wote wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani. (Anza: Panya…) (alama2)
   ii) Mbwa ambaye aliripotiwa kuwa ameibwa amepatikana katika bwawa la maji (Anza: katika bwawa…..) (alama2)

e) Andika kwa msemo halisi sentensi. Tajiri alishangaa kuwa niliweza kuubeba mzigo huo peke yangu. (alama 2)

f) Piga mstari vivumishi katika sentensi hizi
   i) Sina nguo yoyote niwezayo kuvaa (alama 1)
   ii) Mtoto mwenyeweatataileta kalamu (alama 1)

g) Andika vitensi vinavyotokana na majina haya;
   i) Mfuasi
   ii) Kifaa
   iii) Mharibifu (alama 3)

h) Kanusha
   i) Ungemwuliza vizuri angekujibu bila wasiwasi (alama )
   ii) Andika kinyume;
   Mjomba alicomeka upanga kwenye ala (alama 2)
   i) Eleza maana nne-tofauti za sentensi hii;
   Alinunua samaki na mtoto wake (alama 4)

j) Eleza tofauti baina ya sentensi hizi;
   i) Ningekuwa na pesa ningenunua shamba.
   ii) Ningelikuwa na pesa ningalinunua shamba (alama 2)

B a) Kamilisha tashbihi zifuatazo
   i) Baidika kama
   ii) Mzima kama

b) Tumia tanakali za sauti zifaazo kukamilisha sentensi hizi;
   i) Sauti ya waimbaji haikusikika tena, ilikuwa imedidima…wageni walipofika katika jukwaa.
   ii) Simba ni mnyama hodari sana, akimkamata swara humrarua
   (alama2)

c) Tunga sentensi mbili tofauti zinazobainisha maana tofauti kati ya:
   i) Nduni
   ii) Duni (alama 4)

d) i) Mdudu anayetengeneza atandu huitwa (alama 1)
   ii) Mdudu mwenye mkia ulipinda nchani ambao una sumu ni
   (alama 1)

e) Andika methali moja inayotokana na maelezo yafuatayo:
   Asiye na uwezo ataendelea kuwa bila uwezo hata akifanya bidii namna gani.
   (alama2)

**102 1B**
**KISWAHILI KARATASI 1B**
**OCT. NOV 2004**
**2 ½ HOURS**

**1. UFAHAMU**
***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***
Wahenga walisema “mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.” Hii ina maana ya kuwa ukiogopa kutumia ufito kumchapa mtoto wako, ukamdekeza atadeka na hatimaye ataharibika. Methali hii ina picha yake ambyo ni, “Ukicha mwana kulia, utalia wewe.”

Hizi ni methali zilizojaa busara kubwa. Mathalini wewe ni mzazi au mtu yeyote mzima aliyetunikiwa madaraka juu ya watoto. Lakini kila wanapokiuka uadilifu au mmoja wao anapokosea wewe unambembeleza tu, basi huwa unaizorotesha tabia yake. Mwisho, mtoto huyo anaweza kuishia kuwa mtundu.

Hata hivyo, ni sharti tujue ya kwamba tuko katika njia panda hapa. Kwa upande mmoja, zamani ilichukuliwa kwamba watoto na hata wanawake watu wazima hawana akili. Kwa ajili hiyo, iwapo mwanaume mtu mzima ana jambo la kuwaeleza, njia pekee ya kuliingiza katika “ akili” yao “ hafifu” ni kuwatwanga ili kulikongomeza jambo hili. Ukweli ni kwamba akili ya mtoto si hafifu hata. Unaweza kusema ni kama mmea, ambao usiporutubishwa kimakusudi, ukapaliliwa vyema na kustawishwa stahiki yake, basi hudhoofu” na mwishowe kufifia.

Kwa upande mwingine, mtazamo wa kisasa ni tofauti kabisa, imethibitishwa ya kwamba wanawake ni sawa kabisa katika maumbile yao wakilinganishwa na wanaume. Kwa jinsi hiyo, kweli wapo wanawake amabo hawana mwelekeo timamu kuhusu maisha. Lakini ni kweli pia kuwa wapo wanaume watu wazima mamilioni ambao hawana akili. Kadhalika, si kweli kuwa watoto wote, kwa sababu ya umri wao tu, basi hawana akili. Ama kwa kusema kweli binadamu yeyote kuwaliwa na akili zake timamu isipokuwa wale ambao kwa bahati mbaya maumbile yamewapa akili pungufu. Hili litokeapo basi tunalikubali tu. Hatuwezi kumlaumu mtu kama huyo au muumba wake. Kwa hakika huu ndio msingi wa methali. “Akili ni nywele, kila mtu ana zake.” Vinginevyo, mtazamo wa kizamani ni taasubi kogwe tu za kiume zilizopitwa na wakati.

Aidha, kwa sababu watu wote huzaliwa na akili timamu, tena hawawi watu wazimu kabla ya kuwa watoto kwanza, mtu mzima yeyote ana hali gani ya kuwadhulumu watoto na kujipambaniza na lawama za uongo dhidi ya vijana hao kwa madai kuwa hawana akili? Na je, ikiwa hawana akili, basi ndipo waonewe? Wanyanyaswe? Hili si jambo la busara. *Kurudi mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo.* Kurudi kufaako ni kwa kupeleka mbele, sio kwa kurudisha nyuma. Kurudi kuelekezako mbele ni kwa uongozi mwafaka, uongozi ambao lengo lake ni kummulikia mtoto kurunzi ilimradi kumwongoza mtoto.

Mtoto ana haki ya kuhudumiwa kwa njia yoyote ifaayo ili akue na akili yake ikomae kikamilifu. Inafaa asomeshwe, apewe malezi bora ili naye aje alee wengine kistahiki.

(a) “Mapenzi yasiyo kipimo yanaweza kuwa hatari kwa mtoto.” Eleza kikamilifu huku ukirejelea habari uliyosoma ( alama 3)

(b) Fafanua njia panda inayorejelewa na mtunzi ( alama 3)

(c) Mtoto analinganishwa na mmea katika taarifa hi, kwamba “usiporutubishwa

kimakusudi, ukapaliliwa vyema na kustawishwa stahiki yake basi hudhofu."
Tahtmini kulinganishwa huku, huku ukirejelea taarifa ( alama4)

(d) "Akili ni nywele, kila mtu ana zake." Eleza maana ya ndani ya methali hii kulingana na taarifa ( alama 4)

(e) Onyesha kwamba unaelewa maana ya:
"Kurudi mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo" ( alama 4)

(f) Eleza maana ya:
(i) Kulikongomeza ( alama 2)
(ii) Kujipambaniza

**MUHTASARI**

Maendeleo ya taifa hutegemea jinsi wananchi wanavyolitolea katika kulibingirisha gurudumu la uchumi wao. Kila mwanajamii anahitajika kujibidisha katika kazi au taaluma yake. Mzalendo yeyote yule hupata motisha ya kufanya kazi iwapo anaweza kupata ile kazi aliyokuwa akitamani.

Kumakinika katika taaluma Fulani si jambo jepesi na huchukua muda kutengeneza. Kwa mfano, ili mhazili apate staha ya uhazili sharti apitie ngazi mbali mbali. Mwanzo kabisa lazima kumpa fursa ya kujiunga na vyuo mbali mbali vya uhazili. Anapojiunga na vyuo hivyo ndipo safari inapoandaliwa. Kukamilisha safari hii inahitaji muda wa miaka mine- mitano. Anapohitimu kuwa tayari ameimudu shughuli hiyo. Hata hivyo, anatakiwa afanye mazoezi kila mara ili asisahau yanayohitajika katika taaluma hiyo. Wengi waliokwishapata ujuzi huo wa wale wenzao ambao katika masomo wana utaakamu kama wao. Ijapokuwa wote ni wahazili, viwango vyao ni tofauti na mishahara pia hutofautiana. Tofauti hapa ni daraja zao za vyeo. Baada ya kuhitimu na kupata vyeti vya uhazili ni rahisi kupata au kutopata kazi zenye ujira wa kuvutia. Anayefanikiwa ana sayari ya kujikakamua hasa kwa upande wa uzingatifu wa kazi kikamilifu na kutunza hadhi ya ofisi yake.

Kuna mashirika makubwa yanayojiweza kiuchumi, ambayo rasimali yake ni imara. Mashirika madogo huwa yana rasilmali yenye kuyumbayumba. Mashirika haya yana wahazili na wanafunzi ambao hupata mishahara duni. Wanafunzi wote hao hufanya kazi kwa kutokuwa na uhakika wa kulipwa mwisho wa mwezi. Watu kama hao hawawezi kutilia maanani kazi zao. Mashirika mengine hayana utaratibu maalum, wa kulipa mishahara kwa vile hutegemea utu wa mkurugenzi. Badhi ya wakuu hao huwa wabanizi na huwapunja wafanyi kazi wao. Hili ni swala nyeti ambalo linahitaji litatuliwe kwa kuwa na chama cha kupigania haki za wafanyikazi. Wakati wanapotafuta kazi, Wahazili wengi huwa ni wahitaji na hukubali chochote wanachopewa.

Wale waliobahatika kupata nafasi ya ajira katika kampuni kubwa za kimaataifa, mishahara huwa ni ya kutia moyo. Katika dunia hii wahazili wana vibarua vigumu, kwa sababu lazima wapate tajriba na uzoefu wa taaluma inayoendelea na shirika Fulani. Mhazili anapotumia msamiati usionda sambamba na shughuli za kiofisi hawasiti kufoka. Wavumilivu miongoni mwao hula mbivu. Hawa hawafi moyo bali hujitahidi zaidi ili wasikumbwe na kimbunga cha kufokewa. Kuna wengine ambao humwaga unga.

(a) Bila kupoteza iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya ya kwanza na ya pili ( maneno 60 – 70) Alama 2 kwa mtiririko) ( alama 8)

(b) Kwa kuzingatia aya mbili za mwisho, eleza mambo muhimu yanayoshughulika na mwandishi ( maneno 60 – 70) alama 2 kwa mtiririko) ( alama 8)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

1. (a) Andika udogo na ukubwa wa jina ngoma ( alama 2)

(b) (i) Eleza namna mbili za matumizi ya alama ifuatayo ya uakifishi (;) ( alama 2)

(ii) Tunga sentensi mbili tofauti zinazoonyesha matumizi hayo ( alama 2)

(c) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo

(i) Kazi yote ni muhimu

(ii) Kazi yoyote ni muhimu ( alama 2)

(d) Tunga sentensi mbilimbili kuonyesha matimizi mawili tofauti ya

I. Ka

II. Ndivyo ( alama 4)

(e) Tunga sentensi kuonyesha matumizi sahihi ya viunganishi hivi ( alama 2)

(i) Ingawaje

(ii) Ilhali

(f) Tambulisha kielezi, kivumishi na mnyambuliko wa kitenzi katika sentensi ifuatayo:

Msichana mrembo alikuja upesi akimkimbilia dadake ( alama 2)

(g) Andika kifungu hiki kutoka usemi wa taarifa hadi usemi halisi ( alama 4)

Watoto waliambiwa na mama yao watakaporudi nyumbani waoge. Wale, halafu waanse kusoma moja kwa moja badala ya kuharibu wakati wao kwa kutazama vipindi vya runinga. Aliwakumbusha kuwa wanaofanya maonyesho kwenye runinga tayari wamefuzu shuleni na wameajiriwa kazi

(h) (i) Taja vihusishi vitatu vinavyorejelea mahali, wakati na kiwango ( alama 3)

(ii) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kila kihusishi ( alama 3)

(i) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo

(i) Alicheza kwa bidii akawafurahisha wengi waliohudhuria tamasha hizo

Anza kwa: Kucheza ( alama 2)

(ii) Karamu hiyo ilifanya sana, kila mtu alikula chakula akatosheka

Anza kwa: chakula ( alama 2)

(j) Tunga sentensi mbili tofauti ukitumia vitenzi hivi vya silabi moja ( alama 2)

(i) Pa

(ii) La

(k) Unda vitenzi kutokana na majina haya: ( alama 2)

(i) Mtukufu

(ii) Mchumba

**LUGHA**

**KISWAHILI KARATASI 2 (102.2)**
**OKT/NOV 2005**
**SAA 2 ½**

**1. UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Nairobi , mji mkuu wa Kenya, ni jiji la maajabu na mastaajabu chungu nzima. Nadhari ya mtu anayewahi kuingia jiji hili kwa mara ya kwanza huvutiwa na huo msheheneko wa majumba ya fahari, marefu ajabu, kiasi cha minazi mitano- sita iliyounganishwa kuelekea juu mbinguni.

Jumba linalowavutia watu wengi ni lile la makongamano ya kimataifa liitwalo kwa kiingereza Kenyatta International Conference Centre. Jumba hili, hadi miaka michache ilipopita, ndilo lililokuwa refu zaidi mjini. Jumba lenyewe lina ghorofa ishirini na tisa hivi, Usipohesabu hilo pambo kama kofia kileleni mwake, linalojulikana kama mwavuli. Hata hivyo, miaka michache iliyopita jingo hili lilipitwa kwa urefu na mnara wa Nyakati ( Times Tower) Mnara huo hasa ni jumba linaloafiki lakabu yake ya kikwaruza mawingu. Jumba hili lina ghorofa zisizopungua thelathini na mbili.

Mbali na majumba haya mawili, kuna majumba mengine zaidi ya ishirini katikati ya jiji ambayo, japo mengine ni mafupi kiasi, maumbo ya kustaajabisha kweli kweli. Hebu zingatia mwenyewe jumba liitwalo "mdomo wa kengele" au bell - bottom" ambalo ni vioo vitupu, toka chini hadi juu. Fauka ya haya, umbo lake ni la kipekee ulimwenguni kote. Jumba hili lina kama miguu, kisha kiuno mithili ya kinu hivi japo si mviringo. Linapaa juu, mbali sana, likichukua umbo pana kuliko lilivyo chini. Umbo la fua pana kama kengele.

Halafu rudia barabara. Hizi hazina hesabu katikati ya jiji ni pona, tena safi sana. Magari yanayotumia barabara hizi ni kochokocho, ya kila aina na yanashindania nafasi.

Ajabu kubwa ya Nairobi hata hivyo ni idadi ya watu. Hakuna hasa anayejua idadi kamili ya watu wa Nairobi, lakini sio kupiga chuku ninaposema kwamba, hasa nyakati za kuelekea kazini asubuhi, kwenda kula chakula cha mchana, kuelekea nyumbani baada ya kazi na kuvuka barabara wakati wa msongamano, watu hukanyagana. Mtu anayesema kwamba watu wa Nairobi ni wengi kama chungu, au kama mchanga wa ufuo wa bahari, hati chumvi

Watu wa Nairobi, kwa tabia na mavazi, si kama watu wa kwingineko nchini Kenya. Watu hawa kuvalia nadhifu sana. Wanawake ni warembo ajabu na hutengeneza nywele zao mithili ya hurulaini peponi. Wengi huvaa suruali ndefu! Kucha zao na midomo yao hupata rangi maridadi sana. Huzungumza Kiswahili na kiingereza takriban wakati wote. Wanawake wengi ajabu huendesha magari yao wenyewe, jambo ambalo litakushangaza mara tu uingiapo jijini, hasa kama ulilelewa ukidhani maskani mwafaka ya wanawake ni jikoni peke yake, yaani kuzingatia ile falsafa kuwa " kuoa ni kupata jiko". Wanaume nao huvaa suti safi, maridadi na shingoni wamefunga tai stahiki yao. Wanaume hao huendesha magari ya kuyaegesha karibu na afisi zao. Huingia afisini mwao kwa maringo na madaha, huku funguo za magari yao zikining'inia vidoleni. Hawa nao husema Kiswahili na kiingereza kupitia puani, utadhani ni waingereza hasa.

Kwa upande mwingine, watoto ni nadhifu kweli hasa watoto wa shule. Hawa huvalia sare zilizofuliwa na kunyoshwa vizuri kwa pasi. Wake kwa waume, shingoni huvalia tai. Watoto wa shule Nairobi huongea Kiswahili, kiingereza na Sheng, ambayo ni "lahja" yao waliyoibuni.
"Luhya" hii ni mchanganyiko wa Kiswahili. Kiingereza na msamiati mchache wa lugha nyingine za wakenya zisemwazo jijini Nairobi na vitongoji vyake.

Kwa jumla, watu wote wa Nairobi hutembea kasi sana. Hawana hata wakati wa kutembea pole pole na kuangazaanga huku na huko. Iwapo wewe ni mgeni jijini, ukizubaa utapigwa kumbo na waendelee na hamsini zao kama vile hapakutokea jambo. Hili linapojiri, usidhani limefanywa maksudi. La, hasha ni vile tu kwamba Wanairobi hawana muda wa kupoteza.

(a) Kwa nini majumba ya jiji la Nairobi yana majina au lakabu za kiingereza? ( alama 2)

(b) (i) Baadhi ya maajabu ya Nairobi ni barabara safi, msongamano wa magari na majumba marefu. Ongezea maajabu mengine manne ( alama 4)

(ii) Watu wa Nairobi wanajipenda kweli kweli. Fafanua ( alama 4)

(c) (i) Je, unadhani watu wa Nairobi kweli hukanyagana? Eleza ni kwa nini msimulizi ametoa maelezo hayo ( alama 2)

(ii) Unafikiri ni kwa nini hasa wanawake wa Nairobi wanaonekana nadhifu? ( alama 3)

(d) Kwa nini neno “lahja” limewekwa alama za mtajo? ( alama 1)

(e) Eleza maana ya maneno na tamathali za usemi zifuatazo: ( alama 4)

(i) Nadhari

(ii) Linaloafiki

(iii) Kikwaruza mawingu

(iv) Waendelee na hamsini zao

**2. UFUPISHO**

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo lilolowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesi mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hii. Hata hivyo, fanaka haijapatikana wala haielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi la dhana ya “ujambazi” tena “wa kimataifa”. Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi wan chi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambazi ni balaa kweli, tena belua, lakini huo ni wa huko, wala hauwezi kuwagusa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni watakaburi hao, ujambazi ni wa watu “washenzi” wasiostaarabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi pekee wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa madawa ya kulevya uliosababishwa na vinyangarika kutoka nchi hizo maaluni za “ ulimwengu wa tatu”. Kulingana na wastaarabu wan chi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusagwasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu ya kuwa ujambazi wa kimataifa. Hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilipoelekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako! Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo, wanarekani kudhai kwamba ingewezekana taifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kuishambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya aina yeyote ile ya uchokozi kutoka pembe lolote la dunia.

Hakuna ulimwengu mzima, aliyeamini kuwa marekani ingeeza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio marekani pekee.

Mintarafu hiyo, marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusherehekea. Kwa nahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara- pacha ya Newyork na lile la Pentagon, uti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ilizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa ni majambazi wa kimataifa.

(a) Bila bubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza ( maneno 65 – 75)
Matayarisho
Nakala safi (alama 10, 2 za utiririko)

(b) Ukizingira aya, tatu za mwisho, fafanua fikira za watu wa mambo yote yaliyotokea
Baada ya Septemba tarehe 11, 2001 (maneno 65 – 75) (alama 10, 2 za utiririko)
Matayarisho
Nakala safi

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Bainisha aina ya vivumishi katika sentensi hii ( alama 2)
Nyumba yangu ni maridadi

(b) Kamilisha jedwali

| Kufanya | Kufanyia | Kufanywa |
|---|---|---|
| Kula | | |
| Kuunga | | |

( alama 4)

(c) Eleza matumizi ya kwa katika sentensi hii
Aliimba kwa sauti tamu (alama 1)

(d) Andika kwa wingi (alama 1)
Pahala hapa ni pake

(e) Eleza matumizi ya na katika sentensi:
Halima na Asha wanasaidiana ( alama 3)

(f) Huku ukitoa mifano, fafanua miundo mitatu ya majina katika ngeli ya JI-MA ( alama 6)

(g) Onyesha (i) Kielezi (ii) kitenzi katika sentensi ( alama 2)
Mvua ilinyesha mfululizo

(h) Kanusha sentensi hii:
Tumechukua nguo chache kuuza ( alama 2)

(i) Tumia – ndi pamoja na viashiria vya ngeli kujaza mapengo
(i) Wewe ____________ ninayekutafuta
(ii) Nyinyi ____________ mnaoongoza

(j) Andika sentensi hii upya kwa kufuata maagizo
(i) Nilikuwa nimejitayarisha vizuri kwa hivyo sikuona ugumu wo wote katika safari yangu.
Anza: safari ( alama 2)

(k) Geuza vitenzi hivi view majina
(i) Shukuru ( alama 1)
(ii) Enda ( alama 1)

(l) Eleza maana mbili tofauti za sentensi hii
Mamake Juma na Mariamu walitutembelea ( alama 2)

II (a) Eleza maana ya:
(i) Sina pa kuuweka uso wangu ( alama 1)
(ii) Ana mkono wa buli ( alama 1)

(b) Jaza jedwali

| Kiume | Kike |
|---|---|
| Mjakazi | |
| Jogoo | |
| Fahali | |

( alama 3)

(c) (i) Kati ya madini haya taja yale yanayopatikana baharini

| | |
|---|---|
| Zinduna | Zebaki |
| Lulu | Ambari |
| Yakuti | Marumaru |

(alama 3)

(ii) Haya ni magonjwa gani?
I Matubwitubwi
II Tetewanga ( alama 2)

(iii) Mbuni huzaa matunda gani? ( alama 1)

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI**
**LUGHA**
**OCT/NOV 2006**

**1. UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za Kulitadarukia tatizo la umaskini ambao unakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaoyakabili mataifa yanayoendelea. Unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakitpiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yalo yaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umaskinin huu ni anuwai mathalan, ufusadi, uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemea mvua isiyotabarika, idadi ya watu inayoupik uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini unaoathiri nchi Fulani una athari pan asana. Uvunigu unaotokana na umaskini unaweza kuweza kuwa mboji ambako matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburai madeni mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umaskini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharural ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa huishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza masikini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yazingatie uhalishi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

a) Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea? (alama 4)

b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)

c) Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la umaskini?

d) Mfumo wa soko huru una mathara gani kwa mataifa machanga? (alama 2)

e) Ukirejea kifungu, eleza maana ya:
   i) Kulitadarukia

ii) Kuatika
iii) Kuyaburai madeni

2. **MUHTASARI**

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalokumba ulimwengu wa sasa , hasa katika nchi zinazozoendelea. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo ilivyo katika nchi nyingi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika nyanja mbalimbali za jamii. Zipo sababu nyingi zinazowasukuma watoto kutafuta ajira barani Afrika kwa mfano, familia nyingi huishi maisha ya ufukara hivi kwamba hushindwa kuyatimiza mahitaji muhimu hususan kwa watoto. Kapanda kwa gharama ya maisha kunazidisha viwango vya umaskini. Ukosefu wa lishe pia huwafanya watotto kutoroka nyumbani kutfuta ajira. Janga la **UKIMWI** limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoshia kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. **UKIMWI** umezifanya nyingi pia kuwaondoa watoto shule ili waweze kuajriwa kwa lengo la kuanzisha pato la familia hizo. Watoto wengine hutoroka makwao kwa sababu ya maonevu. Maonevu haya ni kama vile kupigwa, kutukanawa kila wakati, kunyanyaswa kijinsia na kadhalika. Huko nje hutaabishwa kimwili na kiakili. Hufanyishwa kazi za sulubu zenye malipo duni au wasilipwe kabisa. Hili huwasononeshe na kuathiri afya yao.

Uundaji wa Umoja wa Afrika hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kama vile ajura ya watoto, kuzorota kwa miundo msingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia haki za watoto, nchi za Afrika hazina budi kuzingatia masharti yalivyowekwa na Umuja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi nyingi za Afrika ziliidhinisha mkataba wa marsharti hayo ikiwemo inchi ya Kenya. Nchi hizi basi lazima zishughulikie haki za watoto kupitia sheria za nchi. Watoto ni rasilimali muhimu na ndio tumaini la kuwepo kwa kizazi cha binadamu.

a) Eleza mambo yote muhimu anaazungumzia mwandishi katika aya ya kwanza
(maneno 45-50) (alama 7, 1 ya utiririko)
Matayarisho
Jibu

b) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwisho (maneno 50-55)
(alama 8, 1 ya utiririko)
Matayarisho
Jibu

3 **MATUMIZI YA LUGHA**

a) Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya ngeli ya I – I (alama 1)

b) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mchoro wa matawi:
Mkulima mzembe amepata hasara (alama 4)

c) Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi: Alimchezea (alama 3)

d) Taja sauti mbili zinazotamkiwa midomoni (alama 2)

e) Kanusha sentensi ifuatayo:
Ningalikuwa na pesa ningalinunua nyumba (alama 2)

f) Kitenzi fumbata kiko katika hali (kauli) ya (alama 1)

g) Tunga sentensi ukitumia kielezi cha
   i) Wakati (alama 1)
   ii) Mahali (alama 1)

h) Andika sentenzi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa (alama 1)
   i) Mhunzi mrefu alishinda tuzo (Anza kw: tuzo… (alama 1)
   ii) Mwanafunzi huyu anasoma Kifaransa. (Anza kwa kiashiria kisisitizi)

i) Sentensi hizi ni za aina gani?
   i) Lonare anatembea kwa kasi. (alama 1)
   ii) Halima anaandika hali Ekomwa anasoma (alama 1)

j) Tunga sentensi moja ukitumia neon "seuze" (alama 1)

k) Bainisha Kirai Nomino na Kirai Tenzi katika sentensi:
   Jirani mwema alinipa chakula (alama 2)

i) Unda nomino kutokana na vitenzi:
   i) Chelewa (alama 1)
   ii) Andika (alama 1)

m) Onyesha hali katika sentensi zifuatazo:
   i) Henda mvua ikanyesha leo. (alama 1)
   ii) Miti hukatwa kila siku duniani. (alama 1)

n) Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia neon "japo"
   i) Selina alijitahidi sana .
   (ii) Selina hakushinda mbio hizo (alama 1)

o) Andika kinyume cha:
   Mwise alikunja nguo alizokuwa ameanika (alama 2)

p) Sahihisha sentensi:
   Mtoto ambaye niliyemsomesha ameasi jamii (alama 1)

q) andika katika msemo wa taarifa. "Sitathubutu kumpa pesa zangu" Mkolwe alisema. (alama 2)

r) Tunga sentensi kuongyesha tofautu kati ya vitate vifuatavyo (alama 2)
   **Suku** na **zuka**

s) Eleza matumizi ya ritifaa katika: 'N" shamchukua (alama 2)

t) Andika **udogo** na **ukubwa** wa neno 'kiti' (alama 2)

u) Eleza matumizi ya "na" katika sentensi: (alama 2)
   Sofia na Raeli wanaandaliwa chai na mpishi

4 **ISIMU JAMII**

**Soma kifungu kifuatacho ujibu maswali yanayofuata.**

Kwa mujibu wa sheria kifungu nambari 3 sehemu ya A ya sheri za nchi, umepatikana na hatia ya kutatiza utulivu wa raia wapenda amani kwa kuwatusi na kutisha kuwapiga.

Kiongozi wa mashtaka amethibitisha haya wa kuwaleta mashahidi ambao wametoa ushahidi usiotetereka kuhusu vitendo vyako katika tukio hilo. Korti hii imeonelea una hatia na imeamuru ufungwe jela kwa muda wa miaka miwili bila faini ili liwe funzo kwako na kwa wenzako wenye tabia kama zako. Una majuma mawili kukata rufani.

a) Lugha iliyo katika kifungu hiki hutumika katika muktadha upi? (alama 1)

b) Toa ushaidi wa jibu lako (alama 3)

c) Zaidi ya sifa zilizo katika kifungu hiki, eleza sifa zingine sita za matumizi ya ligha katika muktadha huu. (alama 6)

102/1
K1SWAHILI Karatasi ya 1
INSHA Oct/Nov. 2007
Saa 1 $^{3}/_{4}$

1.INSHA YA LAZIMA:

Andika barua kwa mhariri wa gazeti ukilalamikia hali ya watu nchini kwenu kuhamia mataifa ya nje kwa wingi,

2. Eleza vile tatizo la uhaba wa maji linavyoweza kutatuliwa hapa nchini.

3. Mshikamano katika familia hutegemea mambo mengi. Fafanua,

4. Bahati ya m \venzio usiilalie ralango wazi.

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**

**Oct/Nov. 2007**
**saa $2^1/_2$**

1. UFAHAMU

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Takwimu ambazo zimetolewa na shirika la kazi la kimataifa (ILU) zinaonyesha kuwa ulanguzi. wa watoto umetangaa hususan katika mataifa yanayoendelea. Ipo tumbi ya sababu za kuelezea kwa nini biashara hii imeshamiri.

Atharj mojawapo ya utandawazi ni kuunda mtandao mpana ulimwenguni. Mtandao huo unaweza kutumiwa kwa njia chanya au njia basi. Njia chanya ni zile zinazoukiliwa kuwafaidi wanajamii kwa kuendeleza ubinadamu na kuboresha hali ya maisha kiuchumi, kisiasa na kitamaduni, Maarifa yanayosambazwa huweza kuwa <u>chachu ya kuumua ari va maendeleo.</u> elimu na mafanikio katika mataifa mengi ulimwenguni. Njia hasi ni zile ambazo <u>maarubu</u> yake ni kuwanufaisha wachache huku zikiwahasiri wengi.

Kuwepo kwa mtandao kunawapa wenye nia tule kama usafirishaji na ulanguzi wa watoto fursa ya kuzitosheleza hawaa zao. Wanaoshiriki katika biashara hii huongozwa na <u>pashau</u> ya utajiri, Hawachelei kuwalangua watoto wanaochimbukia mataifa ya kimaskini huko ugaibuni wanakozongomezwa kwenye madanguro, kufanyishwa kazi za sulubu na za kitopasi na kuiishi maisha duni.

Asilimia kubwa ya watoto hurubuniwa kwa ahadi ghushi za kujiendeleza kimasomo. Wengine huuzwa kutokana na msaada wa jamaa zao wanaotovukwa na utu na kuwa mawakala katika amali hii ya kusikitisha. Biashara hii huweza kusahilishwa kwa kuwepo kwa mfumo fisadi wa kisheria, msarnbaratiko wa muundo wa jamaa na ubinafsi wa kijamii.

Ipo haja kubwa ya ushirikiano wa mataifa alkulihali kuikomesha biashara hii haramu. Jamii ya ulimwengu isipofanya hivi. itakuwa imekitia kizazi kizima kitanzi na kuitumbukiza kesho yake kwenye matatizo kathiri.

(a) Ni kwa jinsi gani utandawazi umechangia katika biashara ya ulanguzi wa watoto?
(alama 2)

(b) Mwand is hi wa kifungu anapendekeza hatua zipi kusuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto?

(c) Eleza jinsi watoto wanaolanguliwa wanavyoishi huko ughaibuni. (alama 3)

(d) Kulingana na muktadha, kifungu chachu ya kuumua ari ya maendeleo" kina maana gani? (alama 2)

(e) Jamii isiyosuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto itakuwa na hatima gani? (alama 3)

(f) Eleza maana ya

(i) maarubu

(ii) pashau...

(alama 2} MUHTASARI

Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ni nguzo kuu katika ulimwengu wa leo. Kimsingi, ubinafsishaji ni hatua na harakati zinazochukuliwa kupunguza kushiriki kwa serikali katika uendeshaji wa mashirika na kuhimiza kupanuka kwa sekta ya kibinafsi.

Serikali huweza kuhimiza, kutokana na uuzaji, uhawilishaji wa mali fcutoka umiliki wa umma hadi kwenye umilikaji wa sekta ya kibinafsi. Aidha, serikaii inaweza kuuza hisa zake kwenye mashirika ya umma. Njia nyingine ni kuchochea ugavi wa zabuni kupitia kwa mikataba ambayo inashindaniwa na mashirika au kampuni tofauti. Lengo kuu la ubinafsishaji ni kuigatua nafasi ya serikaii katika utendakazi oa uejideshaji wa mashirika.

Uuzaji wa mashirika ya kiserikali au hisa huwa chanzo cha mapato yanayoweza kutumiwa kuendesha miradi mingine. Hii ni njia ya kupunguza hanja ya serikali inayotokana na uendcshaji wa mashirika yasiyoleta faida. Ubinafsishaji huzuia uwezekano wa kuingiliwa kwa mashirika na wanasiasa, huimarisha utamaduni mpya wa muundo wa mashirika na huvunja uhodhi wa kiserikali. Ubinafsishaji huweza kuatika mbegu za ujasiriamali wa raia, kutamani kuanzisha amali tofauti.

Ubinafsishaji huweza kuyaruhusu mashirika ya kimataifa kutwaa mashirika muhimu nchini, kufutwa kazi kwa wafenyikazi na kuongezeka kwa umaskini Ubinafsishaji wa sekta zinazohusiana na elimu na afya huweza kuathiri vibaya wenye mapato ya chini.

Ubinafsishaji haumaanishi ufanisi wa utendakazi wa makampuni na mashirika. Aidha, ikiwa haupo utaratibu mzuri wa kutathmini au kupima thamani za hisa pana uwezekano wa hisa zinazouzwa kupewa thamani ya juu au ya chini.

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa kifungu, fanya muhtasari wa aya ya kwaza na ya pili. (maneno 35 - 40} (alarna 6, I ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

(b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika **aya ya** tatu na ya nne (maneno 45 - 50) alama 9, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi (alama 2)

MATUMIZI YA LUGHA

(a) Tunga sentensi moja ukitumia nomino dhahania.

(b) Eleza maana rnbili za sentensi ifuatayo:

Hawa ni watoto wa-marehemu Bwana Nzovu na Bi Makambo. (alama 2)

(c) Unda nomino moja kutokana na kitenzi "ghafilika". (alama I)

(d) Andika kwa wingi: Nyundo hii imevunjika mpini wake. (alama 1)

(e} Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia jedwali.

mvulana mrefu anavuka barabara. (alama 3)

(f) Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo. (alama 2)

(i) Karama ...........................................................................................

(ii) Gharama ...........................................................................................

(g) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo:

(i) Mtoto mwenyewe alienda shatnbani. (alama 1)

ii) Kazi yetu haihitajiki shuleni.

(alama 1)

(h) Koloni/nukta mbili *(:)* hutumiwa katika kuorodhesha, Onyesha matumizi mengine matatu ya koloni (: ) (aiama 3)

(i) Tunga sentensi itakayoonyesha matumizi ya kihusishi cha a-unganifu. lalama *2}*

(j) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo 'Mkulima aliyepanda wakati ufaao amepata mavuno mazuri. (.alama 2)

(k) Ainisha viainbishi katika neno: kujidhiki. (alama 2)

(!) Tambua na ueleze aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo
'Kalamu aliyokuwa nayo mwalimu ni va mwanafunzi. (alama 2)

(m) Andika viwakilishi ngeli vya nomino zituatazo:

(i) Chakula............ .,....,.........................................................................

(alama 1) (ii)

Kwetu ..............................................................................................

(alama 1) (n)

Badilisha sentensi ifuatayo ill iwe katika hali ya kuamuru.
Baba ingia ndani. (alama 2)

(o) Eleza maana ya sentensi
'Ningalikuwa na pesa ningalinunua nyumba na ningalistarehe'. (alama 2)

(p) Fafanua aina za hali zinazotumika katika sentensi hizi.

(i) Mwimbaji aliimba, akacheza na akaehanganisha sana. (alama 1)

ii) Sharigazi huja kila mara. (alama 1

(q) Tunga sentensi MOJA itakayoonyesha maana. mbili tofauti za neno pembe. (alama 2)

(r) Andika katika msemo wa taarifa "Nitakuarifu nikimwona", Elma alisema, (alama 3)

(s) Nyambuakitenzi "ota" kama kinavyotokea katika kirai "ota ndoto" ili tofauti tatu zijitokeze: (alama 3)

4. Isimu Jamii

Huku ukitoa mifano mwafaka. fafanua kaida tano katika jamii ambazo matumizi ya lugha hutegemea. (alama 10)

**102/3**
**KISWAHIU**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**Oct/Nov. 2007**
**(Lazima)** **saa: $2^1/_2$**

*Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata:*

1 Tohara, usimwazie, mwanamke,
Tohara, usikarimbie, mwili wake,
Tohara, usiifikie, ngozi yake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

2 Tohara, hiyo haramu, adha kwake,
Tohara, ni kubwa sumu, si kufu yake, Tohara, ni za
kudumu, dhara zake,
Tohara ya mwanamke, katwaani shtezie!

3 Tohara, kile kijembe, usikishike,
Tohara, yule kiumbe, si haki yake,
Tohara, usimtimbe. kwayo makeke,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

4 Tohara, ni tamaduni, usiyashike, Tohara, ati uzimani.
ajumuike, Tohara, umaahini. kwa mwanamke,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

5 Tohara, akijifungua, ataabike.
Tohara, yaweza ua, hufa wanawake, Tohara,
inausumbua, uhai wake,
Tohara ya mwanamke. katwaani siwazie!

6 Tohara, na siku hizi, haya uyashike,
Tohara, gonjwa umaizi, lije iimshike,
Tohara, ageuke uzi, hue mWili wake,
Tohara ya mwanamke. katwaani siwazie!

7 Tohara, nasisitiza, rawanamke,
Tohara, inaibeza, hadhi yake,
Tohara, inadumaza, fikira yake,
Tohara ya mwanamke, zamu yake ipitile!

(a) Eleza dhamira ya msanii katika shairi hili, (alama -)

(b) Fafanua madhara manne ya tohara kwa mwanamke. (alama *4)*

(c) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi ziiizotumika katika shairi, (alama 4)

(d) Kulingana na mshatrl mwanamke hupashwa tohara kwa nini? (alama 2)

(e) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari. (alama 4)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi

(i) adha
(ii) usimdmbe (alama 2)

(g) Upashaji wa tohara kwa mwanamke ni mojawapo ya maswala ibuka katika jamii yetu. Taja maswala ibuka mengine mawili yanayohusu mwanamke. (alama 2)

**RIWAYA**
**Z.BURHANI: Mwisho wa Kosa**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2 Onyesha jinsi ukengeushi unavyojitokeza katika riwaya ya Mwisho wa Kosa. (alama 20)

3 Eleza jinsi ambavyo KINAYA kimetumiwa katika. riwaya ya Mwisho wa Kosa. (alama 20)

TAMTHILIA
KITHAKA WA MBERIA: Kifo Kisimani
Jibu swali la 4 au la 5.

4 Ukirejelea tamthilia ya Kifo Kisimani, fafanua mambo yanayopiganiwa na umma katika nchi ya Butangi. (alama 20)

5 "Uovu wa mume si uovu wa mke"

(a) Eleza muktadha wa kauli hii. (alama 4)

(b) Onyesha jinsi mhusika anayerejelewa hapa alivyosaidia kupunguza mateso ya wana Butangi.. (alama 10)

(c) Eleza wasifu wa msemaji. (alama 6)

**HAD1THI FUPI**

**K.W. WAMITILA:** ***Mayai Waziri wa Maradhi***

6. Mimi nashughulika na wanyama wa porini, mambo yanayohusu binadamu mimi simo".

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama4)

(b) Onyesha jinsi mzungumzaji na wenzake wasivyowajali wananchi wanaowahuctamia. (alama 16)

FASIHI SIMULIZI

(a) Nini maana ya mighani/migani? alama4)

(b) Fatanua sifa tano za Mighani/migani. Alama 10)

(c) Eleza umuhimu wa mighani/migani: alama 6)

**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1 INSHA Okt/Nov, 2008**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

**Maagizo**

Andika Insha mbili insha ya kwanza ni ya lazima.
Kisha chagua insha moja nyingine kutoka hizo tatu zilizobakia.

Kila insha isipungue maneno 400.

Kila insha ina alama 20.

1. **Insha ya lazima.**
Andika tahariri kwa gazeti la Raia ukieleza hatua zinazochukuliwa nchini ili kumwendeleza kielimu mtoto msichana.

2. "Ufisadi ndicho kikwazo kikuu katika maendeleo ya uchumi wa taifa lolote." Thibitisha.

3. Matikiti na matango ndiyo maponya njaa.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa ; "Aha! Kumbe mwungana akivuliwa nguo huchutama. Sitaisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka maishani kama nilivyoaibika siku hiyo."

**Kenva Certificate of Secondary Education**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**
**Saa: $2\frac{1}{2}$**

**Maagizo**

Andika jina lako na namba yako katika nafasi ziliizoachiwa hapo juu. Weka sahihiyako na

Tarehe ya mtihani katika nafasi zilizoachiwa hapo juu. Jibu waswali yote. Majibu yako

yaandikwe katika.nafasi zilizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

| **Swali** | **Upeo** | **A lama** |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **Jumla** | | |

## 1 UFAHAMU

*Soma makala yafitatayo kisha ujibu maswali.*

Kuna aina kuu za hisia zinazotawala na kuongoza maisha ya mwanadamu: kuona, kusikia, kugusa, kuonja na kunusa. Ni vigumu kusema ni hisia gani muhimu kuzidi nyingine ingawa ni dhahiii alhari kubwa humuangukia mabuluku asiyeweza kuona. Inasernekana kuwa mishipa ya fahamu inayounga ubongo na macho ni rnikubwa zaidi kuliko mishipa ya fahamu inayounga ubongo na viwamfao vya masikio. Na katika maisha na nyemdo za kila siku kuona hupewa uzito mkubwa minghairi ya **kusikia** Pengine basi sio ajabu. kama itakavyobainika punde baadaye. kuwa kazi nyingi za fasihi andishi zimeelemea mno katika hisia hii kana kwamba zile nyingine kuu hazipo kabisa. Hakika hili ni kosa. Maana kusikia kugusa, kuonja. na kunusa nako ndiko humkamilisha mwanadamu aweze kuyafaidi maisha yake. Na hata mbele ya sheria, ushahidi huweza kutolewa mintaaraf u ya kusikia, kugusa, kuonja na kunusa alimradi shahidi awe amesikia, kugusa. kuonja. au kunusa mwenyewe. Ushahidi wa kuambiwa haukubaliwi.

Kwa hivyo basi kazi ya sanaa ambayoitazituma fikra za msomaji zihisi kuona, kusikia, kuonja kugusa, na. kunusa matendo na mazingira yanayosimuliwa humpeleka msomaji huyo katika mipaka na nyanja za juu za ufahamu na furaha.

Kila hisia ina umuhimu wake kutokana na mazingira ya tukio linalohusika ati kusimuliwa. Maana kazi zote za sanaa hutokana na matendo na maisha ya watu ambao katika matukio, visa na mazingira yao hutumia hisia zao zote tano ama kwa pamoja an kwa nyakati mbalimbali. Ili basi msomaji aweze kupata mandhari kamili, na hata yeye mwenyewe ashiriki katika matukio yenyewe kwa kuchukia, kuonea huruma. n.k muhimu, kabia ya yote, apate hisia zote hizo tano. Kazi ya sanaa inayojihusisha na hisia moja tu au mbili huwa muflisi.kisanii kwa vile inashindwa kuwasilisha mandhari za hali halisi kwa msomaji. Je, mara ngapi nyoyo zetu husononeka au kuripukwa kwa maya kwa sababa ya sauti ndogo tu ya ndege aliaye pekee nyikani, au nyimbo yazamani? Sauti ya ndege huweza kuieta majonzi ya mtaka mingi mno ya utotoni wakati ambapo mtu alifiwa na mzazi, ndugu, jamaa au sahibu wake. Kadhalika nyimbo ya kale huweza kuchimbua ashiki ya zamani baina ya wapenzi.au kutonesha jeraha la masaibu na madhila yaliyopita. Na wala sio nyimbo na sauti ya ndege tu, pengine hata" hanifu ya maua huwa na nguvu za kumbukumbu kubwa mno.

Licha ya yote hayo, matumizi ya hisia nyingi yanasaidia kujenga mandhari kamili ya tukio katika akili ya msomaji Mathalan badala ya kuelezwa tu kuwa paliandaliwa chakula kizuri. msomaji anaelezwa vitu ambavyo vimeandaliwa pamoja na hamfu yake. Au badala ya kuambiwa mtu fulani alikuwa na wajihi wa kutisha. huelezwa na kuelewa vyema zaidi kwa kuainishia jinsi pua macho, rangi, nywele, mdomo na meno ya mtu huyo yalivyo. Na hivyohivyo kwa mifano mingine kadha wa kadha kama vile hasira na ucheshi. Kutokana na maelezo ya kutosha ya hisia msomaji huweza kumuashiki ianabi. au akadondokwa na ute kutamani chakula ambacho hakipo mbele yake.

Na sio hivyo tu. Hisia zinazotumiwa huweza kumfanya msomaji atafakari zaidi. Ataweza kufikia uamuzi kuhusu picha zinazochorwa kutokana na hisia mbalimbali na wafa sio kauli za rnkatomkato za mwandishi kama ilivyogusiwa hapo juu. Kauli za mkatomkato sio tu hudumaza sanaa, bali pia hudhalilisha hata akili ya msomaji kwani unbuji wa mwandishi ni pamoja na kufanya matendo na mazingira anayoyasimulia yawasilishe na kuwakilisha fikira za wahusika wake na hata zake mwenyewe.

Hivyo ni dhahiri kuwa hisia humsaidia msomaji kuzama katika matendo na kuelewa fikra za mwandishi mwenyewe, asili na makazi yake, kuwadadisi na kuwaelewa wahusika wenyewe,n.k.

Makala kutoka: *Safari, A J. 'Hisia Katito Fasihi Andishi*
*Katika Mutokozi M.Mna* Aftfw? *ong o (Wah.) (1993:331*
*Fasihi uandishi na uchapishaji Dar-es-Salaam; Dar-cs-*
*$alaam Univ. Press*

(a) Taja na ueleze uwanja ambao hutilia mkazo hisia zote. (alama 3)

(b) Kwa mujibu wa kifungu hiki, ni nini matokeo ya kusisitiza hisia ya kuona katika fasihi andishi? (alama 2)

(c) (i) Mwandishi ana maoni gani kuhusu kazi nzuri ya sanaa. (alama 2)

(ii) Maoni hayo yana umuhimu gani? (alama 4)

(d) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu ulichosoma.

(i) muflisi kisanii ....................................v……………………………

(ii) jeraha la masaibu…………………………………………………………….

(iii) kumuashiki janabi..…………………………………………………………

(iv) umbuji.........................................................................................(alama 4)

2. UFUPISHO

Uchumi wa soko huria ni hali ya kiuchumi ambapo itokeapo amali, shughuli na harakati zote za kiuchumi ghairi ya zile ambazo ni za lazima kwa serikali au dola kama ulinzi, sheria na mpangilio mzima wa jamii, huwa huria kwa watu binafsi. Msingi wa soko huria, sifa kuu ya utandawazi, ni kuibua na kudumisha mazingira na hali zinazochochea na kumruhusu mtu yeyote kuongozwa na hawaa, au matamanio ya kibiashara anayoyaona sawa pasi na hofu ya kuingiliwa na udhibiti wa serikali.

Mazingira hayo yanawapa watu satua ya kufanya maamuzi kuhusu hatima yao ya kiuchumi. uamuzi kuhusu suala la ajira yao, matumizi ya mtaji - kipato na harija zake, na

uwekezaji mzima. Suala mojawapo linaloibuka kuhustana na mfumo wa soko huria ni kuweka mipaka bainifu na wazi baina ya amali na shughuli zinazohusishwa na serikali na zile ambazo huachwa huria kwa watu. Kwa mfano, inaaminiwa kuwa haki ya kuishi na kulindwa dhidi ya shambulizi, liwe la kijambazi au la kigaidi, ni ya kimsingi ambayo haiwezi kuhusishwa na uwezo wa kiuchumi wa mtu binafsi. Aidha huduma za kimsingi za afya nazo zinaingia katika kumbo hili. Ikiwa huduma hizi zitaachwa huria pana uwezekano mkubwa kuwa zitaishia kuwa istihaki ya wenye mtaji na kipato cha'juu tu.

Licha ya kuwepo kwa sheria au kanuni huria kutoka nyanja maalum. hutokea hali ambapo udhibiti wa kiserikali ni lazima. Hili hutokea pale ambapo ipo haja ya kuyalinda mazingira hasa kuiokana na tichnfiizi wa viwandu au rasiiia. Aidha mlhibiti htio ni laziina pale ambapohaki za watu wengine zinahusika; yaani ikiwa uhuru wa hata mtu mmoja unaadhirika kutokana na sera hizo. pana haja ya kuingilia ili kuisawazisha hali yenyewe.

(a) Andika kwa muhtasari maana ya uchumi wa soko huria kulingana na taarifa hii (maneno 25-30) **(alama** 5. I ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

(b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza katika aya ya pili na ya tatu. (Maneno 70-75) (alama 10, 3 za mtiririko)

Matayarisho

Jibu

## 3 MATUMIZI YA LUGHA

(a) Tambua **mzizi** katika neno
"msahaulifu".,……………,…,…………………………,……,.,…… alam aI)

(b) Tunga sentensi ukitumia **kivumishi cha nomino** alama 1
)

…,.,….,………_.….,…,..,..,..,…….,……….-…….,…,,………,… ….. .

(c) Andika kinyume cha:
Wasichana watatu wanoingia darasani kwa haraka. alama 2)

(d) (i) Fafanua maana ya **"mofimuhuru** (alama

I)

(ii) Toa mfano inmoja wa mofimu huru (alama 1

(e) Tambua kiambishi awali na tamati katika neno alaye. (alarna 2)

(f) Tumia kirejeshi-amba-kuimganisha sentensi **zifuatazo**

(i) Mwanafunzi yule ni mrefu.

(ii) Mwanafunzi yule amepita mtihani. (alama
2)

.........................................................................

(g) Sahihisha sentensi hii:
Waya yangu imepotea...............................................................(alama I)

(h) Taja aina ya yambwa iliyopigiwa mstari katika sensensi ifuatayo:
Mpishi arnempikia nigeni waji vizuri. alama I)

(i) Neno "Chuo" lina maana ya "Shule inayotoa mafunzo maaluum ya kazi fulani Tunga sentensi mbili kubainisha matumizi mengine mawili ya neno hili. Alama 2

(j) Ibadilishe chagizo ya mahali kwa ile ya wakati katika sentensi ifuatayo: Mchezaji aliucheza mpira mjini Malindi. Alama 1

(k) EIeza maana mbili za .sentensi:
Yohana alimpigia Husha mpira. (alama *2*)

(l) Kanusha:
Sisi tumemaliza kujenga nyumba ambayo ingalikuwa yake angalifurahi. (alama 1)

(m) Unda nomino kutokana na:

(i) Zingua...................................................................... (alama 1)

(ii) Tosa ..................................................................... (alama 1)

(n) Ichoree vielelezo matawi sentensi:
Paka mdogo amepanda mchungwani.

(o) Tumia kihusishi badalia kutunga upya senten.si hii:
Mgeni yuko katika nyumba, (alama 1)

(p) Unda kitenzi kutokana na neno "sahili..........................................(alama1)

(q) Eleza tofauti kati ya sauti |z| na [d| (alama 2)

(r) Tambua aina **ya kitenzi** kilichopigiwa mstari katika sentensi.

Mzee hu<u>enda</u> anacheza kamari. (alama I)

(s) Badilisha kiwakilishi kimilikishi kwa kiwakilishi kionyeshi katika sentensi:
Chake kilipatikana nchini. (alama I)

(t) Tumia mfano mmoja mmoja kutofautisha baina ya sentensi sahili na ambatano.
(alama 4)

(u) Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha nomino. alarna I)

(v) Andika kwa wingi:

Mvua imebomoa nyumba ya jirani. (alama I)

(w) Akifisha kifungu kifuatacho:

huenda serikali iwazie kuidhibiti bei ya petroli hatuwezi kuyaruhusu makampuni ya petroli kuunyanyasa umma alisema waziri wa kawi bei ya petroli imeongezwa mara nne katika kipindi cha mwezi mmoja (alama 4)

**ISIMU JAMII**

Eleza huku ukitoa mifano sifa tano za kimsingi zinazotambulisha sajili ya mazumgumzo,

(alama 10)

# KARATASI YA TATU 2008

(LAZIMA) USHAIRI

*Soma shairi hili fusha ujibu maswali yanayofuata.*

WASAKATONGE

1. **Wasakatonge na juakali**
Wabeba zege ya maroshani,
Ni msukuma mikokoteni,
Pia makuli bandarini,
Ni wachimbaji wa migodini,
*Lakini maisha yao chini*

2. **Juakali na wasakatonge**
Wao ni manamba mashambani,
Ni wachapa kazi viwandani,
Mayaya na madobi wa nyumbani,
Ni matopasi wa majaani,
*Lakini bado ni masikini.*

3. **Wasakatonge na juakali**
Wao huweka serikalini,
Wanasiasa madarakani,
Dola ikawa mikononi,
Wachaguliwa na ikuluni,
*Lakini wachaguaji duni*

4. **Juakali na wasakatonge**
Wao ni wengi ulimwenguni,
Tabaka lisilo ahueni.
Siku zote wako matesoni,
Ziada ya pato hawaoni,
*Lakini watakomboka lini?*
(Mohammed Seif Khatib)

(a) "Shairi hili ni la kukatisha tamaa". Fafanua rai hii kwa kutoa mifano minne. (alama 4)

(b) Taja tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima na uonyeshe mifano miwili ya jinsi iiivyotumika. (alama 3)

(c) Eleza umbo la shairi hili. (alama 5)

(d) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari. (alama 4)

(e) Onyesha mifano miwili ya maadiii yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 2)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi.

(i) Manamba

(ii) Tabaka lisilo ahueni alama

## TAMTHILIA

***Jibu swali la 2 an la 3,***

Kithaka wa Mberia: Kifo Kisimani

2 Ukitumia mifano, onyesha matumizi matano ya mbinu ya ishara kama ilivyotumiwa katika tamthilia ya Kifo Kisimani. (alama 20)

3 "Kwa hakika, kama mzazi hana kifani katika Butangi nzima. Na pengine hata katika ulimwengu mzima."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) "Watu waliojiita washauri wa Mtemi Bokono walikuwa si washauri halisi bali wanafiki waliomdanganya," Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano mitano.

(alama 16)

## RIWAYA

***Jibu swali Ia 4au la** 5.*

Z. Burhani: *Mwisho wa Kosa.*

4 "Wanawake katika riwaya ya Mwisho wa Kosa wamepewa nafasi ndogo katika masuala ya maendeleo ya kijamii," Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano kumi, (alama 20)

5 Eleza jinsi wahusika wafuatao wanavyoafiki anwani ya riwaya ya Mwisho wa Kosa.

( a) Ali (alama 10)
(b) Asha (alama 10)

## HADITHI FUPI

K. W. Wamitila *(mhariri): Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*

6 "Umdhaniaye ndiye, kumbe siye".
Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine, onyesha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

FASIHI S1MULIZI

7 Fafanua sifa zozote kumi za mtambaji bora wa ngano. (20 alama)

**MWQNGQZO WA MAJIBU MTIHANI WA KCSE**
**KISWAHILI 2OO7 KARATASI 102/1 INSHA**

1. Barua kwa mhariri
   - Barua hii iandikwe ikizingatia mtindo wa uandishi wa barua rasmi Iwe na anwani ya mwandishi. Iwe na anwani ya mwandikiwa (mhariri)
   - Mtajo (kwa mhariri)
     Kiini /lengo (kichwa cha maoni)
   - Aya (zikiwa na maudhui ya barua)

- Hitimisho

**Maudhui**

- Mwandishi alenge kiini cha habari anayoiandikia.
- Aweke hoja zake kwa njia inayodhihilika
- Jambo analolishughulikia mwandishi liwe na uzito wa kumfanyia mhariri alichapishe gazetini
- Lugha anayoitumia izingatie kiwango cha wasomaji wa gazet/ au jarida na atumie msamiati mwafaka

**Vidokezo: sababu za watu kuhamia mataifa yanje.**

- Wengi huenda kwa sababu ya kujiendeleza kielimu
- Wengine huenda kutafuta kazi sababu ya uhaba wa kazi nchini
- Mshahara duni kazini
- Tamaa ya kutajirika haraka
- Wakimbizi wa kisiasa
- Umaskini

**Masuluhisho; vidokezo**

- Vyuo vikuu kuongezewa nchini
- Serikali ipanue viwanda /kuwaajiri raia
- Wafanyakazi kulipwa mishahara kulingana na kazi wafanyayo /serikali kuboresha mishahara.
- Wananchi kuondoa tama ya kutajirika /kuridhika na kile wanacho/wanachopata
- Sera na mwdngozo mwafaka wa kisiasa kuimarishwa Demokrasia kuzingatiwa ili kuzuia tatizo la wakimbizi.
- Serikali na raia kuweka bidii kazini ili kuimarisha uchumi wa nchi kwa kuzalisha mali.

**2. Vikokezo: matatizo ya uhaba wa maji nchini**

- Maji safi hayapatikani kwa wingi
- Maji hutumiwa vibaya
- Mifereji hutoboka na hairekebishwi na wengine hufunguria na kuyaacha maji yakitiririka.
- Gharama ya juu ya maji.
- Huduma na usabasaji wa maji
- Ukosefu wa maji kijijini.
- Visima kukauka,
- Kuharibu chemichemi za maji

**Masuluhisho: vodokezo**

- Watu kubadili tabia ya kuchafua maji
- Watu kubadili tabia ya kutumia maji ovyo ovyo.
- Mifereji iiiyotoboka irekebishwe mara moja wahusika wanapofahamishwa
- Baraza la maji liwajibike /lljitoiee kutoa huduma ya maji kwa wanakijiji.
- Serikali isaidie katika ujenzi wa mabwawa
- Serikali na watu kuchimba vislma katika maeneo mbalimbali.
- Serikali kujitolea kuhifadhi chemichemi za maji

**3. Vidokezo: Mshikamano katika familia**

- Maadiii mema /heshima/adabu
- Uaminifu baina ya mke/mume
- Mazungumzo ya wazi katika familia
- Mwongozo /mafunzo yanayohitajika katika imani ya dini
- Mapenzi kudhihlrishwa kwa wote bila mapendeleo
- Matumizi mazuri ya raslimaii ya familia
- Mfano mzuri kutoka kwa wazazi hadi kwa watoto
- Kula pamoja /kuomba pamoja
- Kushauriana /kupeana nasaha kwa njia nzuri
- Kukosoana /kurekebisha makosa kwa njia nzuri
- Kuwakuza watoto kwa kuwapa mafunzo mwafaka

**4. Bahati ya mwenzio usilalie mlango wazi** **<u>Maneno muhimu</u>**

- Bahati - neema/jambo jema
- Usiialie mlango wazi - usfiegemee

**<u>Maana va nje</u>**

Huwezi acha kufunga mlango wako ukisubiri neema ya mtu eti inaweza kukupata.

**<u>Maana va ndani</u>**

- Hakuna mtu ambaye anaweza kupata bahati (neema) ambayo imenuiwa mtu mwingine. Hutumiwa kuwashauri watu ambao hupenda kutegemea vitu vya watu wengine wakomeshe tabia hiyo na wajibidiishe kutafuta vyao.
- Mtahiniwa aandike kisa au visa kudhihirisha ukweli wa methali hii.

**<u>Usahihisho KARATASI 1O2/2 -2O07</u>**
**<u>KARATASI 2 LUGHA UFAHAMU</u>**

a. i) Mtandao umewapa wenye nia tule kusafirisha na kuiangua watoto nafasi ya kutosheleza ashiki zao

(i)Mtandao umetumiwa kwa njia hasi ambayo maarubu yake ni kuwanufaisha wachache huku zikiwahasiri wengi

b. i) Mataifa kjjshirfkiana kuikomesha biashara hil haramu.

ii) Wanaoshiriki wakomeshe tabia ya tama ya utajiri

iii) Wanaoshiriki waache kutumia mtandao kama *njia* ya

kuzitosheleza hawaa zao.
iv) Kuundwa mfumo usio na ufisadi wa kisheria
v) Kuzuia msambaratiko wa muundo wa jamaa
vi) kumaliza ubinafsi wa kijamii.

c, - Watoto huzongomezwa kwenye madanguro
- kufanyishwa kazi za sulubu na za kitopasi
- na kuishi maisha duni.

d. Maana ni kule kuchochea bidii/ari/hima kwa watu ili wafanye kazi kwa pamoja na kuleta maendeleo

e. i) Msambaratiko wa muundo wa jamaa
ii) Ubinafsi .
iii) Jamii isiyokuwa na elimu kwa sababu ya kutokuwaelimisha watoto na badala yake kwalungua hatimaye kukosa maendeieo.
iv) Ufisadi wa kisheria utasahilishwa ili kuendeieza biashara hii

f. i) Maarubu - nia/kusudi/sababu/azma/madhumuni/lengo/kiini
ii) pashau - tama/shauku/uchu/kiu.

## UFUPISHQ

a) UBINAFSISHAJI
- Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ni nguzo kuu ulimwenguni
- Hupunguza kushiriki kwa serikari kuendesha mashirika na huhimiza upanuzi wa sekta ya kibinafsi
- Kuuzia umma hisa za mashirika na kuchochea ugari wa zabuni.
- Huiondoa serikali kwenye utenda kazi na kuendesha mashirika. (alama 6,1 ya utiririko)
- Kuingatua nafasi ya serikaii katika utendakazi.

b) Athari za Ubinafsishaji
- Mapato huzafiwa na huutumiwa kuanzisha miradi mingine:
- Hupunguza miradi ya serikali isiyoleta faida
- Huzuia wanasiasa kuingilia mashirika
- Huimarisha utam'aduni mpya na kuvunja uhodhi wa serikali
- Raia hupewa nafasi kuzalisha mali
Hutwaa mashirika muhimu nchini
Hufuta kazi wafanyakazi
Ubinafsishaji wa elimu na afya huadhiri maskini
Kipimo cha kutathmini *hisa* chafaa kuwepo.
(alama *9,1 ya* utuririko)

## MATUMIZI YA LUGHA

a) Atunge sentensi yenye nomino yoyote ya 'dhahania.si lazima iwe mwanzoni mwa sentensi. Ujinga,shetani,uongo, wivu n.k, Mfano; ujinga wake ulimtia matatani (alama 2)

b) i) Baadhi ya watoto ni wa bwana Nzovu na wengine ni wa Bi makambo
ii) watoto wote ni wa BW nzovu bi BI Makambo
iii*)* Wote waweza kuwa marehemu BW.Nzovu na Bi Makambo
*iv)* Hawa ni watoto wa BW Nzovu na Bi makambo pamoja
v) *BI* Nzovu ndiye marehemu na Bi Makambo yuhai. (alama 2)

c) kughafilika/ghafiliko/kighafilikishi/mgafilikishi/mghafilike/ ughafilikaji"/mghafilikishwa/mgafilikiwa/ughafili/mghafi/i/mgafala/(hata katika wingi) (alama 1)

d) Nyundo hizi zimevunjika mipini yake.

e)

| S | | | |
|---|---|---|---|
| KN | | KT | |
| N | V | T | "N |
| Mvulana | Mrefu | Anavuka | Barabara |

(aiama 2)

f) i Lazima atunge sentensi karama-kipawa /uwezo kutoka kwa mungu) '(gharama -matumizi ya pesa/,Bei ya kitu yenye thamani.

Karama yake ilimwezesha kupata mtoto baada ya kukaa muda mrefu licha ya kuwa gharama ya kumlea ilikuwa nitatizo (alama 2)

(alama 1)

g) i) Mwenyewe - kivumishi cha pekee

(alama 1)

ii)Yetu - kivumishi kimilikishi

h)(i) Kusisitiza jina Fulani au jambo la kipekee k.m Kenya ina mlima mrnoja tu ambao una theluji mlima Kenya

(ii) Katika maandishi ya kitamthilia /dayalojia
Mwaiimu:kazungu mbona leo hujaoga?
Kazungu: Mwalimu nimeoga
iii)Kuonyesha saa na dakika.k.m 11.30 kamili
iv kutaja mafungu ya bibilia/kurani
v) kuandika tarehe
vl) Kuandika mada au barua rasmi
vii) katika hesabu kuonyesha uuiano (Ratio)
vlil) katika ufafanuzi

ix) Barua pepe-udahilishi zozote 3x1

i) sentensi iwe na a unganifu k,v. ya cha la n.k.

Alijificha **kando ya** gari (alama **2)**

j) i) Mkulima aliyepanda wakati ufaao (kishazi tegemezi)

ii)Amepata mavuno mazuri -(kishazi huru) (alama 2)
k) i) Ku- kiambishi kiwakiiishi cha nafsi
ii)ji - kirejeshi
iii) Dhiki- shina la kitenzi (alama 2)

I) Aliyokuwa - kitenzi kishirikishi kikamilifu

ii)Ni -kitenzi kishirikishi kipungufu (alama 1)

m) i) Chakula - KI / ki-VI (alama 1)
ii)Ku - ku /ku-ku) (alama 2)
n) Baba ! ingia ndani!

o) i)Hana matumaini ya kupata pesa kujenga nyumba na kustarehe

(kitendo hakiwezekani)
ii) Mtu huyu hakuwa na pesa, hakununua nyumba na hakustarehe
iii) hakuna uwezekano/Haiwezekani
iv) Amepoteza matumaini
v) wakati uliopita

p) i) mfululizo wa vitenzi / Mfuatano wa vitenzi.
ii) hali ya kurudiarudia/ kila wakati .Hali ya mazoea (alama2
\
q) ***atunge sentensi moja itakayodhihirisha maana mbuli ya*** **PEMBE**
i) sehernu ya mnyama/Baragumu
II) Ncha ya kitu k.v. chaki
iii) Mahari pa siri/ faragha
iv) sahemu k.v. ktk nyumba
v) masafa marefu ya dunia (pembe za dunia)

Fahali wale wawili walikuwa wame'pangiwa na wanasarakasi **wale** wakutane pembeni mwa uwanja ili wapigane kwa pembe
(alama **2}**

r) Elma alisema (kuwa) angelimw/angemwarifu kama angelimwona/angemwona.

s) i)Otea ndoto/otesha ndoto/oteshwa ndoto/otewa ndoto (alama 3)

## ISIMU 3AMU

(i) Cheo/hadhi -wodogo
- wakubwa
ii) umri -vijana

-wazee

ii) wakati/misimu
iv) Tabaka -matajiri
v) Mazingira
vi) Muktadha
vii) Hali/Hisia/Afya
viii) Mada -kile kinachozungumziwa
ix) Madhumuni/lengo
x) Malezi
xl) Dini/Imani
xii) Uhusiano-
xiii) Taaluma-Kazi
xivj Lugha azijuazo mtu
xv) Kiwango cha elimu
xvi) Njia ya mawasiliano
xvri) Hadhira
xviii) Tajriba - ufuzi wa juu

i. Kutaja kaida 1

Katoa mfano-1 alama 10

**KARATASI 3: 1O2/3**

**FASIHI**

**1. USHAIRI**

a). Msanii katika shairi hili anatuma ujumbe wa-kukomesha tohara ya wanawake kwa sababu athari zake ni mbaya kwa mwanamke. (alama 2)

b) i) Mwanamke hutaabika anapojifungua
ii)Tohara yaweza kuua mwanamke..

iii)Tohara hubeza hadhi ya mwanamke.
iv)Tohara -hudumiza fikra ya mwanamke (alama 2)

c) i) Takriri -Kurudiarudia maneno k.m tohara

(alama 4)

(alama 2)

ii)Istiari -Tohara ni kubwa sumu
iii)Tafsida -akijifungua badala ya akizaa

d) Kwa sababu ni utamaduni

e) Uelewe tohara ya siku hizi ni ugonjwa mkubwa unaomshika mwanamke na kumfanya akonde sana Tohara ya mwanamke asilari ikomeshwe, (alama 4)

f) (i) Adha -Jambo linalosumbua au kuleta shida/tabu/udhia.
ii)Usimtimbe - Hali ya kumlazimishia mwanamke tohara. (alama 2)

g) i)Uhuru wa mwanamke
ii)Mwanamke kurithi mali kutoka kwa babake.
iii)Ndoa za mapema /lazima kwa wasichana. (alama 2)

**2.RIWAYA Z.BURHANI: MWISHO WA KOSA** (alama 20)

Ukengeushi ni hali ya kumfanya mtu kufuata tabia mbaya au kupotoka kitabia. Baadhi ya wahusika wa mwisho wa kosa walidhihirisha tabia hizi.

**a) Monika**

- Alipenda starehe kupita kiasi, kutembea na wanaume wasiofaa na kutojali onyo la Rashid
- Aliwaacha wadogo wake wakiwa na njaa wakati Bi Tatu aliposafiri.
- alivutiwa na kijana Karim na kuanza kufanya vitendo vya kumshawishi ampende Alidhamini watu wenye vyeo vikubwa na fedha
- Anatoka kwao bila kuaga
- Anatumia lugha mbaya kwa babake
- Alishiklia utamaduni wa kigeni na kudharau utamaduni wa kiafrika
- Alipenda uhuru usio na mipaka na ubinafsi
- Alimchukua Rasid mchumbake Saiama
- Monika kymwonyesha Bi.Keti dharau kwa kutupa kibakuli na kumwaga uji wake na kuuita mchafu.
- Alimbeza Saiama kuwa si mrembo na si mtamaduni.
- Hakuwasaidia wazazi wake ingawa aiikuwa na mshahara mkubwa
- Anapenda kustareheshwa
- 

**b) Matata**

- Alifanya mfainu ya kumwachisha Rashid kazi kwa sababu ya monika
- Anatumia madaraka yake vibaya kwa kuwafukuza wapangaji

Anamshawishi Alison amfute Rashid kazi hivyo kama kiongozi waziri alikengeuka maadili ya jamii

- Alimuoa mtoto mdogo isivyostahili
- Alimlaghai Monika kuwa angemuoa
- Ingawa ameoa lakini ana wasichana wengi.
- Anamhini mwenye nyumba kwa kutolipa kodi kwa muda mrefu
-

c) **<u>Hassani</u>**

- Hupenda kutazama sinema za kitoto
- Hapendi kusoma ili azidi kujiendeleza
- Kukosa kumtunza Muna inavyotakiwa
- Anamnyima uhuru wa kutoka na wenziwe
- anamnyima fursa kuwatembelea wazazi wake
- Anampiga Muna

**d) Salimu**

- Ana kazi nyingi lakini anaziacha ill aonane na Matata.
- Alitumia fedha chungu nzima kumpa msichana fulani atalii Marekani
- Anatumia fedha za umma vibaya
- Anashawishiwa na waziri Matata amwachishe Rashid kazi, naye alifanya hivyo kwa shingo upande,

**e) Asha**

- Anamwonea wivu Bi.keti kwa urembo wake
- Anasingizia kuwa ana mgogoro na mumewe ili apate njia ya kuviiba vyombo vya dhahabu na amsingizie Bi.Keti kuwa ndiye mwizi
- Alijaribu kuficha ila za mumewe za kucheza kamari na madeni aliyo nayo
- Ilibidi akiri uovu wake aliomfanyia keti ndipo apewe msaada wa fedha na Bi Mariamu.

**f) <u>Rashid</u>**

- Aliishi na Monika licha ya kwamba hawakuwa wameoana Alikubali fedha kutoka kwa Alison

**q) Alison**

Anampa Rashid hundi nono ili ashughulikie zabuni.

**3.KINAYA (alama 20}**

- Ni kinaya Rashid anapopokea barua ya kufutwa kazi anapowazia kuwa ni kiongezeo cha mshahara kinyume cha hayo ni barua ya kumfuta kazi
- Monika akisomeshwa kwa shida huko Ulaya Wazazi walitegemea akihitimu na kupata kazi angewasaidia, lakini hakufanya hivyo. Monika alitumia pesa hizo peke yake. Mamake aiiiazimika kukopa salama alipohitgji pesa.
- Kinaya ni mbinu amipayo marnbo yanayotokea huwa kinyume cha matarajio
- Tabia anayofanya mheshimiwa waziri wa eiimu Bwana Matata ni kinyume cha wadhifa wake
- Anapendekeza Rashid kufutwa na ni mfanyakazi mwenye bidii ujuzi na hawa ndio husukuma gurudumu la maendeleo
- Anamwoa msichana wa miaka kumi na sita ambaye ni binti mdogo hajahitimu masomo ya juu. Badaia ya kuhimiza elimu ya wasichana , yeye anapnyesha mfano ulio kinyume kabisa.

» Wazfri Saiimu Hamadi anamfukuza Rashid kazini kinyume cha matarajio yake na'hata rafikiye karne. (Rashid afikuwa mfanya kazi hodari afifanya uchambuzi wa zabuni na yale makampuni ya nje peke yake na wajumbe wote wakakubaiiane naye/laklni badala ya kumpa motisha, anamfukuza)

**102/1**

**Kiswahili**

**Karatasi ya 1**

**INSHA**

**OCT/NOV. 2009**

**SAA 1 ¾**

**INSHA YA LAZIMA**

1. Umealikwa kitongojini mwenu kama mgeni wa heshima katika hafla ya kuxindua kundi la wasanii wa Kikwetu. Andika hotuba utakayotoa y kuonyesha umuhimu wa sanaa na michezo.

2. "Utalii una madhara mengi kuliko faida hapa nchini." Jadili.

3. Samaki huanza kuoza kichwani.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa: Hapo ndipo nilipotambua kuwa kama maswala yao hayatashughulikiew kwa dhati, vijana ni kama bomu ambalo liko tayari kulipuka wakati wowote.

1. **UFAHAMU**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Wanasaikolojia wanabainisha kati ya sehemu mbili kuu katika akili ya binadamu: Ung'amuzi na ung'amuzibwete. Ung'amuzi ni sehemu ya ubongo ambayo kimsingi hupanua na kudadavua yanayotendeka hususan mchana. Ung'amuzibwete ni kibinimethali chake; hufanya kazi wakati binadamu anapolemazwa na usingizi. Baadhi ya mambo anayoshuhudia binadamu mchana yanaingia kwenye ung'amuzibwete wake na kutokeza katika ndoto zake usiku.

Kwa mujibu wa mawazo ya Sigmund freud, mwanasaikolojia wa jadi anayechukuliwa nawengi kama mwasisi wa taaluma ya saikolojia, mambo yanayopatikana katika unga'amuzibwete mambo yana sifa hasi. Freud alidahili kuwa binadamu huyaficha na kuyabania kwenye ung'amuzibwete mambo ambayo hawezi juyasema kadamnasi. Alieleza kuwa matamanio yasiyokubalika, makatazo ya jamii, fikra na kauli zilizoharamishwa na miko ya kijamii hubanwa katika ung'amuzibwete. Shehena hiyo ndiyo inayochipuza kwa njia ya ishara za ndoto, mitelezo ya kauli, yaani maneno au kauli zinazotukoka bila wenye kukusudia, ishara na lugha ya kitamathali katika uandishi wa kibunifu na kadhalika.

Ung'amuzibwete un uwezo mkubwa wa kuathiri matendo ya binadamu. Huu ndio msingi unaowafanya wanasaikolojia wengi, akiwepo freud, kusema kuwa tajiriba ya motto inaweza kufichwa kwenye sehemu hiyo na hatimaye kuishia kutokeza katika utu uzima wake. Kwa kuwa tunapoingiliana na binadamu

wenzetu kila siku tunayang'amuzibwete unapotawala binadamu wenzetu watashindwa kutuelewa. Hii ndiyo hali anayokuwa nayo mwendawazimu. Ung'amuzibwete wake hutawala. Sisi tunaotawaliwa na ung'amuzi tunashindwa kumwelewa; naye bila shaka anashindwa kutuelewa.

Carl Gustav Jung, aliyewahi kuwa mwanafunzi wa Freud, aliupinga mwelekeo wa Freud wa kuungalia ung'amuzibwete kama jaa la mawazo mabaya, matamanio, nia, fikira tuli na dhana ambazo ni hasi. Jung alizuka na dhana mbili muhimu: Ung'amuzibwete wa kibinafsi na un'gabuzibwete jumuishi. Alisema mambo, fikra na uzoefu wowote mbaya unaomuhusu mtu binafsi . Dhana ya ung'a muzibwete jumuishi aliitumia kuelezea sehemu ya akili ya binadamu ambayo inamfanya ayatende matendo Fulani kama binadamu wenzake licha ya tofauti zao kiwakati na kijiografia. Kwa mfano, binadamu wengi wana sherehe za kuzaliwa motto, kuoza, ibada au mviga unaohusiana na kifo licha ya tofauti zao. Jung alisema kuwa kinachochochea hali hii ni urithi Fulani wa kila mwanadamu. Urithi huo unapatikana katika ung'amuzibwete jumuishi.

Upo mwafikiano kati ya wataalamu hawa wawili kuwa ung'auzibwete una uwezo wa kuathiri ung'amuzi matendo ya binadamu ya king'amuzi. Wanasaikolojia wanashikilia kuwa binadamu hawezi kukamilika bila kuzihusisha sehemu zote mbile kwa sababu zinaathiriana.

a) Kwan in ung'amuzibwete unaelezwa kama kinyme cha ung'amuzi? (alama 2)

b) Eleza mtazamo wa Freud kuhusu ung'amuzibwete. (alama 3)

c) Kwa mujibu wa Freud yaliyomo kwenye ung'amuzibwete hudhihirika vipi?

(alama 4)

d) Eleza tofauti ya mawazo kati ya Sigmund Freud na Carl Gustav Jung.

(alama 4)

e) taja hoja inayowafungamanisha Jung na Freud. (alama 2)

2. **MUHTASARI**

Utaifa ni mshikamano wa hisia zinazowafungamanisha watu wanaoishi katika taifa moja. Taif huundwa na watu wanaoishi katika nchi moja na ambao wanajitambua kisiasa kama watu wenye mwelekeo, mwono na hatima sawa. Utaifa umejengwa kwenye hisia za mapenzi kwenye hisisia za mapenzi kwa nchi na utambuzi wa kwamba rangi, cheo, hadhi, eneo, kabila au tofauti nyinginezo baina ya watu wanaoishi katika nchi moja si sbabu ya kuwatenganisha.

Nchi moja huweza kuwa na watu wa makabila tofauti, wenye matabaka ya kila nui na mawazo ainat. Watu hao wanapotambua kuwa kuna sherisi nyinyine inayowaunganisha kama fahari ya kuwa watu waochi hiyo, falsafa na imani sawa ambayo ishara yake kuu ni winbo wa taifa na kuwa tofauti kati yao muhimu huwa wamefikia kuunda taifa.

Mhili mkuu wa utaifa ni uzalendo. Uzaleno ni mapenzi makubwa aliyo nayo mtu kwa nchi yake. Malezi haya ndiyo yanyoongoza matendo yake, matamanio yake, mawazo yake, itikadi yake mwonoulimwengu wake na muhimu zaidi mkabala wake kuihusu nchi yake na hatima ya nchi yenywe. Uzalendo ni nguzo muhimu sana ya taifa. Mzalendo hawezi kuyatenda mambo yanayoweza kuletea mkama nchi yake.

Matendo ya mzalendo huangazwa na mwenge wa mema anayoitakia nchi au taifa lake. Hawezi kushiriki kwenye harakati na amali ambazo zinahujumu au kufumua mshikamano wa taifa zima au kutawaliwa na kitiba cha kutaka kujinufaisha yeye mwenyewe au jamii yake finyu. Matendo ya mzalendo wa kitaifa yanaongozwa na mwelekeo wa kuiboresha nchi yake. Swali linalomwongoza mtu huyo ni: nimeifanyia nini nchi yangu au taifa lahgu? Alhasili mtu anayeipenda nchi yake hawezi kuongozwa na umero wa kibinafsi tu wa kujilimbikia mali, ujiri au pesa. Yuko radhi kuhasirika kama mtu binafsi ili taifa au nchi yake inufaike.

Utaifa ni mche aali ambao unapaliliwa kwa uzalendo, kuepuka hawaa za nafsi, kusinywa na taasubi za kikabila na kuach tama ya kujinufaiha. Hali hiyo inapofikiwa, hatima ya wanajamii wa taifa linahusika huwa nzuri na mustakabali wao na wa vizazi vyao huwa wa matumaini makubwa.

a) Dondoa sifa kuu za utaifa. (maneno 40- 50) (alama 6, 1 ya mtiririko)

matayarisho.

Jibu

b) kwa kutumia maneno kati ya 60-70, onyesho misingi ya kumtathmini mzalendo.

(alama 9, 1 ya mitiriko)

Matayarisho .

Jibu

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) andika sentensi mbili zifuatazo kama sentensi moja kwa kutumia kiwakilishi kirejeshi.

i) duka la Bahati lina bidhaa nyingi

ii) Juma anafanya kazi katika duka la Bahati. (alama 2)

b) i) Eleza matumizi mawili ya kiambishi –ji- (alama 2)

ii) tunga sentensi moja kuonyesha moja ya matumizi hayo.(alama 2)

c) Tumia visawe vya maneno yaliyopigwa mstari kuandika tena sentensi ifuatayo:

<u>Ukuta</u> umemweumiza <u>mvulana</u> alipokuwa <u>akiuparaga</u> (alama 3)

d) chora vielelezo matawi vya sentensi ifuatayo:

Bakari, Roda na Hirsi wamefurahi kupita mtihani. (alama 4)

e) Tambua sauti ambazo si za ufizi katika sauti hizi.

M, t, n, z, gh. (alama 1)

f) Tunga sentensi sahihi ukitumia –fa- katika hali ya mazoa. (alama 2)

g) Onyesha kwa kupiga mstari iliko shadda katika maneno mawili yafuatayo:

i) Malaika

ii) Nge (alama 2)

h) Eleza maana mbili za sentensi:

Kiharusi chake kimewaitia hofu. (alama 2)

i) tunga sentensi ukitumia kielezi cha jinsi cha nomino ifuatayo:

Uganda (alama 2)

j) Bainisha sentensi sahili zilizo katika sentensi mseto ifuatayo:

Hamali ambaye ameugua alisema kuwa angekwenda hospitali jana

(alama 3)

k) Andika ukubwa wa sentensi:

Ndovu wa Kiafrika ameharibu kichaka (alama 2)

I) Iandike tena sentensi ifuatayo bila kutumia vitenzi visaidizi

Wachezaji huenda wakawa wanaweza kushinda mchezo wa leo.(alama 2)

m) andika kw msemo halisi: Baba alipotuuliza kama tungependa kwenda Mombasa wakati wa likizo tulimjibu kwamba tulitaka kwenda Kisumu kwa kuwa tulikuwa hatujaliona Ziwa Victoria. (alama 3)

n) Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi mawili ya kinyota(*) katika sarufi ya Kiswahili. (alama 3)

o) Kanusha sentensi ifuatayo:

hapo napo ndipo nitakapo. (alama 1)

p) andika kinyume cha:

furaha amehamia mjni. (a lama 1)

q) andika maneno yafuatayo katika kauli zilizoonyeshwa katika mabano

| | Neon | Kauli | Jibu |
|---|---|---|---|
| i) | Imba | (tendesha)…………………………………… | |
| ii) | choka | (tendea) ………………………………………… | |

. **ISIMUJAMII**

Eleza majukumu matano matano matano ya Kiswahili kama lugha ya Kitaifa na Kimataifa.

(alama 10)

# 102/3
# KISWAHILI
# KARATASI YA 3
# FASIHI
# OKT./NOV. 2009
# SAA 2 ½

**RIWAYA**

**S.A MOHAMED: UTENGANO**

1. Lazima

" Katu asingajitia kibuibui na kutanga na njia.  Lo, kachoshwa na shimiri za baruti anazoshindiliwa moyoni mwake."

a) eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) taja na ufafunue tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili (alama 4)

c) Eleza umuhimu wa kisa kinachorejelewa na dondoo. (alama 4)

d) kwa kurejelea matukio mengine katika riwaya ya Utengano, fafanua maudhui mawili yayoashiriwa na dondoo hili. (8 mks)

## USHAIRI

Jibu swali la 2 au la 3

2 Soma shairi kisha ujibu maswali yanayofuata:

KIBARUWA: Abdilatif Abdalla

Kwenye shamba hilo kubwa asilani hakunyi mvuwa!
Ni kwa mitilizi ya jasho langu ndiyo hunweshezewa
Kwenye shamba hilo kubwa sasa imeshaiva kahawa
Na bunize ni matone ya damu yangu niliyotowa
Ndipo mte ukatipuza!

Buni hiyo itakaangwa buni hiyo itapondwapondwa
Buni hiyo itasagwa na buni hiyo itafyondwafyondwa
Bali itabaki nyeusi kama ngozi yangu Kibaruwa

Waulize ndege kwa nyimbo nyanana watutumbuizao
Iulize na mito kwa furaha maji itiririkao
Uulize na upepo mkali kwa ghadhabu uvumao-.

Viulize: Ni nani araukaye na mapema kuzitema mbuga na kuzilaza?
Viulize: Ni nani akweaye minazi tangu kuchapo hadi lingiapo giza?
Viulize: Ni nani abebeshwaye mizigo hadi maungo yakageuka shaza?
Halfuye hana faida moja apatay wala malipo yanayotosheleza-
Isipokuwa kusundugwa na kutupiwa matambara na vyakula viliyooza?
Viulize: Ni nani huyo ni nani!

Viulize: Ni nani aliyemaye mashamba na kuyapoliliya?
Na mimea kochokocho ikajaa kwa uzito ikajinamiya?
Hatimaye nani atajirikaye mali yakammiminikiya
Akatoa na kitambi kama mja mzito wa miezi tisiya
Na akaongeza magari na wanawake kutoka na kuingiya?
Viulize: Ni nani huyo nani1

Na hao ndege kwa nyimbo nyanana watutumbuizao
Nayo hiyo mito kwa furaha maji itirikao
Na huo upepo mkali wenye ghadhabu uvumao
Vyote hivyo vitatu vitakujibu kawa umoja wao

"Ni Kibaruwa Manamba ndiye mtendaji hayo!"

a) Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 2)

b) Kwa kutoa mifano, eleza aina mbili za idhini ya kishairi alizotumia mshairi (alama 4)

c) kwa kurejelea ubeti wa tatu taja na ueleze tamathali ya usemi na mbinu ya kimuundo mshairi (alama 4)

d) Huku ukitoa mifano, eleza kwa kifupi mwelekeo wa mshairi kuhusu vibarua. (alama 4)

e) andika ubeti wa tano katika lugha ya nathari (alama 4)

f) Onyesha utata wa maana katika matumizi ya Kibaruwa Manamba (alama 2)

3. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yayofuata:

Kila Mchimba Kisima
Musa Mzenga

1. Tenda utendapo tendo, tenda tendo kwa hekima,
Lindamane mwenendo, sawa na yakio kalmia,
Kalmia yenye upendo, kufurahisha mtima,
Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

2. Utendapo la faraja, tendo ni yako salama,
Ya kukupa kila tija, na ushindi wa daima,
Upate njema daraja, duniani na kiyama,
Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

3. Utendapo la miuja, tendo ni yako nakama
Ya kukutia harija, hasara kukuandama,
Usione afuwaja, mwanza ajue heshima,
Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe

4. Nakwambia uelewe, pulika ninayosema,
Si ari ya mwenginewe, kumuonya kwa lazima,
Mtu hufunza mwanawe, Kwanza ajue heshima,
Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

5. Nisipokwambia wewe, kukufunza kila jema,
Kusudi nikuongowe, uepukwe na tujuma,
Matusi ndimi nipawe, ila na kila lawama,

Kila mchimba kisima, bundi hungia mwenyewe

6. Hii si heri ujuwe, matusi kuigandama,
Hadhi usiniuzuwe, hamithilishwa na nyama,
Fikiri moyo utuwe, nikupapo taaluma
Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

7. shika tena utambuwe, wasia huu ni mwema
Matendo usipunguwe, mazuri kutenda hima,
Yatende ubarikiwe, upawe na taadhima
Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

8. Yakupasa uchunguwe, kila jambo kulipima
Upime ufafanuwe, mambo yote kwa alama
La kuwaka ulijuwe, pia lipi la kuzima,
Kila mchimba kisima hungia mwenyewe.

a) Eleza maudhui ya shairi hili. (alama 4)

b) Ujumbe unaowasilishwa katika shairi hili una hadhira lengwa tatu. Zitaje na utoe mifano. (alama 6)

c) Eleza umuhimu wa kipokeo kinachotumiwa katika shairi hili (alama 4)

d) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 4)

e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi:

i) afuwaja
ii) taaluma (alama 2)

## K.C.S.E MWAKA WA 2010 KARATASI YA 102/1

**1 Insha ya Lazima:**

Andika wasifu wa ndugu yako ambaye amepanga hafla ya kuchangisha pesa za kumgharamia masomo ya Chuo Kikuu.

2 Eleza hatua zinazochukuliwa na serikali kuparabana na ufisadi hapa nchini.

3 "Wakenya hawawezi kuafikia umoja wa kltaifa iwapo wataendelea kutumia lugha zao za kienyeji." Jadili

;

4 Binadamu ni ngamba hakosi la kuaraba.

## K.C.S.E MWAKA WA 2010 KARATASI YA 102/2

1 UFAHAMU (alama 15)

*Soma kifungu kifnatacho kisha ujibu maswali*

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jatnii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukoa miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni vale yanayojulikanakama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano him hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu, unawcza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya kipindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea.

Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daiina. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii wanaoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri, uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii inasigana na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari yameghoshi ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutw aji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa rripito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna vighairi hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na 'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mirumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwezake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa, ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, maranki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (alama 1)
(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (alama 1)
(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)
(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (alama 4)
(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. (alama 2)
(f) Je, kifungu, hiki kina ujumbe gani mkuu? (alama 2)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu.

(i) inasigana
(ii) yameghoshi
(iii) vighairi

**2. MUHTASARI** (alama 15)

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwa uchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea wenzo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifahuelezwakwatamathali hii kutokananauwezo wa: kuyadhibiti, kuyaendesha, kuyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ambaye ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanaweza kuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chirnbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine wengi pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha maarifa mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu mmoja huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu hawezi kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo mzito wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia za ishara au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishwa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano, kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambamba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana. Kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', 'mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu, ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapo mfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe, ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za ueneaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a) Fupisha aya ya pili na ya tatu. (maneno 55 - 60) (alama 5, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

**(b)** Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane. (maneno 100 - 110). (alama 10, 2 za utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

**3. MATUMIZI YA LUGHA** (alama 40)

(a) Toa mfano wa neno lenye muundo wa silabi ya irabu pekee (alama 1)

(b) Eleza maana mbili zaneno: Barabara. (alama 2)

(c) Sahihisha sentensi:
Abiria walisafiri na ndege. (alama 1)

(d) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi:
Mwanafunzi mkongwe amepewa tuzo kwa kuwa hodari masomoni. (alama 4)

(e) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi.
Usingeacha masomo, usingetaabika vile. (alama 2)

(f) Tunga sentensi ukitumia kielezi cha:
(i) Jumla . (alama 1)
(ii) Namna linganisho . (alama 1)

g) Ainisha shaminsho na chagizo katika sentensi: Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo.
Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo. (alama 2)

(h) Eleza maana mbili zinazopatikana katika sentensi: Nenda ukaniletee mbuzi. (alama 2)

(i) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya ngeli ya U-U. (alama 2)

(J) Andika katika usemi wa taarifa.
"Mito yetu imechafuka sana; itabidi tuungane mikono wakubwa kwa wadogo, wanaume kwa wanawake ili tuisafishe." Mwanamazingira alituhimiza. (alama 3)

(k) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale.
Amina na Mustafa huimba taarabu. (alama 4)

(1) Eleza matumizi ya <u>ku</u> katika sentensi:
Sikumwelewa alivyoeleza namna ya kuwatunza mbwa wake. (alama 2)

(m) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi la katika kauli ya kutendwa. (alama 2)

(n) Eleza kazi ya kila kitenzi katika sentensi:
Mkulima angetaka kupalilia shamba lake mapema. (alama
4)

(o) Taja na utofautishe vipasuo vya ufizi.

(p) Onyesha jinsi moja moja ya matumizi ya viwakifishi vifuatavyo:- (alama 3)

(i) nusu koloni(;)
(ii) herufi kubwa
(iii) Kishangao(!)

**4 ISIMUJAMH** (alama 10)

"Benki yenyewe haina kitu ... CD4 count yake iko chini ... Ni emergency ... Tutampoteza ikikosekana."

(a) Taja sajili inayorejelewa na manerio haya. (alama 2)

(b) Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo. (alama 8)

# K.C.S.E MWAKA WA 2010 KARATASI YA 102/3

**SEHEMU A: USHAIRI** (alama 20) **1** **(LAZIMA)**

*Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.* **Dhamiri yangu**

Dhamiri imenifunga shingoni.
Nami kama mbuzi nimefungwa
Kwenye mti wa utu. Kamba ni fupi
Na nimekwishachora duara.
Majani niwezayo kufikia yote nimekula.
Ninaona majani mengi mbele yangu
Lakini siwezi kuyafikia: kamba, kamba.

Oh! Nimefungwa kama mbwa.
Nami kwa mbaya bahati, katika
Uhuru kupigania, sahani ya mbingu
Nimeipiga teke na niigusapo kwa mdomo
Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena
Kuifikia na hapa nilipofungwa
Nimekwishapachafua na kuhama siwezi.

Kamba isiyoonekana haikatiki.
Nami sasa sitaki ikatike, maana,
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba
Aliharibu na mbwa aliuma watu.
Ninamshukuru aliyenifunga hapa
Lakini lazima nitamke kwa nguvu "Hapa nilipo sina uhuru!"

(E. Kezilahabi)

(a) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia. (alama 4)

(b) Kwa nini mshairi haoni haja ya yeye kuwa huru? (aiama 2)

(c) Eleza maana ya mshororo ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi.
"Kamba isiyoonekana haikatiki." (alama 2)

(d) Taja na utoe mifano ya aina mbili za tamathali zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)

(e) Kwa kutoa mifano miwili, eleza jinsi matumizi ya mishata yanavyojitokeza katika shairi hili. (alama 4)

(f) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (alama 4)

## SEHEMU B: RIWAYA

***SA.Mohamed: Utengano***

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. "...wewe kwako toka lini mwanamke kuwa mtu? Wangapi umewatenda?"

   (a) Eleza muktadhawa dondoo hili. (alama 4)

   (b) Kwa kutoa mifano minne mwafaka, dhihirisha ukweli wa dondoo hili. (alama 16)

3. Kwa kurejelea vipengele vifuatavyo vya matumizi ya lugha katika riwaya ya *Utengano*, onyesha jinsi mwandishi amevitumia kufanikisha maudhui:

   i) uzungumzinafsi; (alama 10)

   ii) taswira (alama 10)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**Kithaka Wa Mberia: *Kifo Kisimani***

*Jibu swali la 4 au la* 5

4. "Dalili ya mvua ni mawingu."
Kwa kuzingatia utawala wa Mtemi Bokono, thibitisha usemi huu. (alama 20)

5. "Nitoeni! Nitoeni kaburini. Ondoeni udongo. Ondoeni udongo nitoke kaburini."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Taja na ueleze tamathali za usemi mbili zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Kwa kurejelea tamthiliya nzima, fafanua hoja **sita** kuonyesha jinsi dondoo hili linavyoonyesha kinyume cha mambo. (alama 12)

## SEHEMU D: HADITHIFUPINA FASIHI SIMULIZI

**K. W. Wamitila:** *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 aula.7*

6 "Ana nini mtoto huyu! Ninamtesekea na ufakiri wote huu nilionao..."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Eleza tatizo alilokuwa nalo anayerejelewa kisha ufafanue vitendo vinavyodhihirisha kwamba alikuwa na tatizo,
(alama 6)

(c) Anayetoa kauli hii alikuwa na msimamo gam kuhusu tatizo la mtoto?
(alama 4)

(d) Kwa kutoa mifano mitatu mwafaka, eleza hali zinazoweza kulaumiwa kwa tatizo la anayerejelewa.

(alama 6)

## FASIHI SIMULIZI

7 Huku ukitoa mifano mwafaka, **linganisha** na **utofautishe** kipera cha vitendawili na kile cha methali.

(alama 20)

*102/1*
**KISWAHILI Karatasi ya 1 INSHA**
# Okt./Nov. 2011
***Muda: Saa 1$^{3}/_{4}$***

Maagizo

1. **Andika insha** mbili. **Insha ya kwanza ni ya** lazima.
2. **Kisha chagua insha moja nyingine kittoka kwa hizo tatu zilizobakia.**
3. **Kila insha isipungue maneno 400.**
4. **Kila insha ina alama 20.**
5. Karatasi hit ina kurasa 2 zilizopigwa chap a.
6. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**1** ***Insha ya lazima.***

Wewe kama mwanafunzi umepata nafasi ya kumhoji Mkurugenzi wa Habari nchini kuhusu umuhimu wa magazeti kwa wanafimzi wa shule za sekondari. Andika mahoji.ano hayo.

2 "Magari ya matatu yameleta faida nyingi hapa nchini kuliko hasara." Jadili.

3 Pele hupewa msi kucha.

4 Andika insha itakayomalizika kwa:

"Niliipapia ile bilauri ya maji kwa pupa. Sikuwa na uhakika kuwa kiu yangu ingekatika. Nikapiga mafunda mawili, matatu. Baada ya kugumia bilauri yote, ndipo nilipotambua kuwa kweli maji ni uhai."

# 102/2
# KISAWHILI
### KARATASI ya 2
### LUGHA
### 2011

**UFAHAMU** (Alama15)

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Changamoto kubwa inayowakabili watu wengi katika mataifa yanayoendelea ni suala la chakula. Suala hili linaweza kuangaliwa katika sawia mbili tofauti. Kuna tatizo linalofungamana na uhaba wa chakula chenyewe, Uhaba huu unaweza kutokana na utegemezi mkubwa kwa zaraa kama nyenzo kuu ya uzalishaji wa chakula.

Zaraa katika mataifa mengi hususan yanayoendelea, hutegemea mvua. Kupatikana kwa mvua huathiriwa na mabadiliko ya tabianchi ulimwenguni. Matendo na amali za watu kama ukataji wa miti na uchafuzi wa mazingira huwa na athari hasi kwenye tabianchi hiyo. Mabadiliko ya tabianchi huweza kuvyaza ukame kutokana na **ngambi ya mvua.**

Kibinimethali hutokea wakati mafuriko yanapotokea na labda kuyasomba mazao mashambani na kusababisha baa la njaa. Hali hizi mbili husababisha matatizo makubwa ya chakula na kuathiri pakubwa suala zima la usalama wa chakula. Hi kuzuia uwezekano wa kuwepo kwa shida hii, pana haja ya kuwepo kwa mikakati na sera za kuhakikisha kuna usalama wa chakula. Kwa mfano, pana haja ya kukuza kilimo cha umwagiliaji ili kuepuka **adha** inayosababishwa na ukosefu wa mvua. Kwa upande mwingine, sharti zichukuliwe hatua mufidi za kuzuia na kupambana na athari za gharika.

Changamoto nyingine inahusiana na usalama wa chakula chenyewe. Chakula kilichosibikwa na vijasumu au kwa njia nyingine ile huweza kumdhuru anayehusika. Msibiko wa chakula unatokana na vyanzo tofauti. Mathalan, uandalizi wa chakula kilichochafuliwa na choo, kutozingatia mbeko za usafi, uandaaji wa chakula na kukiweka katika hali ya uvuguvugu kabla ya kukipakua - hali inayochochea ukuaji wa viini na ulaji wa chakula kisichoandaliwa vyema.

Ili kuepuka uwezekano wa kuadhirika, pana haja ya kuzingatia usafi wa chakula na uandalizi unaofaa. Fauka ya hayo, vyombo vya uandalizi viwe safi, kanuni za usafi zifuatwe, upikaji na uandaaji uwe kamilifu. Hali hii isipozingatiwa, siha za raia wenyewezitaathirika pakubwa.

**Maswali**

(a) Taja aina **mbili** za kuangalia suala la chakula katika mataifa yanayoendelea. (alama 2)

(b) Taja hatua **mbili** zmazoweza kuchukuliwa kupambana na tatizo la chakula. (alama 2)

c) Eleza jinsi nne tofauti namna chakula kinavyoweza kuwa si salama? (alama 4)

(d) Kwa nini inahalisi kukipakua chakula baada ya kukiandaa tu? (alama 1)

(e) Ni mapendekezo gani anayoyatoa mwandishi kuhakikisha kuwa chakula kinafaa? (alama 4)

(f) Eleza maana ya maneno haya jinsi yalivyotumiwa: (alama 2)

(i) Ngambi yamvua ........................................................................................

(ii) Adha.........................................................................................................

**MUHTASARI**

Uwazaji tunduizi ni tendo ambalo huhusisha matumizi ya akili. Uwazaji huu umekitwa kwenye matumizi ya michakato kama makini, upangiliaji, uteuzi na tathmini. Hata hivyo, uwazaji huu si mchakato mwepesi bali ni mchakato changamano.

Mchakato wa uwazaji tunduizi unahusisha stadi na mikabala tofauti. Mathalan, kuweza kutambua na kubainisha misimamo ya watu wengine, hoja wanazozua na uamuzi waliofikia, kutathmini au kupima ushahidi uliopo ili kubainisha mitazamo tofauti. Vilevile. uwazaji tunduizi hushirikisha kupima hoja za upinzani na ushahidi uliopo kwa njia ya haki pamoja na kutambua yaliyofichwa au ukweli uliofunikwa na taswira ya juu juu. Hali kadhalika, uwazaji tunduizi hujumuisha kutambua mbinu zinazotumiwa kufikia misimamo fulani kwa mvuto zaidi na kwa matumizi ya mbinu za kishawishi. Aidha, uwazaji huu huhitaji kutathmini masuala kwa mtindo ulio wazi, kufikia uamuzi kama hoja zinazotumiwa zina mashiko au zinakubalika kuwa nzuri. Zaidi ya hayo, uwazaji tunduizi unahusisha kuwasilisha mtazarao kwa njia yenye uwazaji mzuri na inayoshawishi.

Uwazaji tunduizi una manufaa anuwai. Mosi, unasaidia kujenga makini ya utendaji. Pili, hupevusha uwezo wa usomaji kwa kuufanya usomaji huo uwe na malengo wazi. Fauka ya hayo, unamsaidia mtumiaji kutambua hoja kuu katika matini au ujumbe fulani bila ya kuzongwazongwa na hoja duni za pembeni. Uwazaji huu unasaidia kuuchonga uwezo wa kuikabili au kuiitikia hali fulani na kukuza stadi za uchanganuzi. Mwanadamu huwa mtu tofauti na bora anapoujenga na kuuimarisha uwazaji tunduizi wake.

**Maswali**

(a) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha ay a mbili za mwanzo.
(Maneno 70 - 80) (alama 10; alama 2 za utiririko)
**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

(b) Andika kwa muhtasari mambo muhimu katika aya ya tatu.
(Maneno 35 - 40) (alama 5; alama I ya utiririko)
**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

3 **MATUMIZI YA LUGHA.**

(a) Tumiamzizi '-enye'katika sentensi kama:

(i) Kivumishi.......................................

(ii) Kiwakilishi ....................................

(alama 2)

(b) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa:-

Paka mweupe araenaswa mguuni .(alama 2)

(c) Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo:-

(i) Kiyeyusho ..................................................................................................

(ii) Kimadende..................................................................................................

(alama 1)

(d) Onyesha shamirisho kitondo, kipozi na ala katika sentensi ifuatayo:-

Kipkemboi alimbebea mwalimu mzigo kwa gari. (alama 3)

(e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.

Maria alipika taratibu huku mama akimwelekeza vizuri. (alama 4)

(f) Nomino 'furaha' iko katika ngeli gani?

.......................................................................................................... (alama 1)

(g) Andika kinyume cha sentensi:

Watoto wameombwa waanike nguo. (alama 2)

(h) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa. Mama alishangilia arusi ya mwana.

Anza: Mwana ...................................................................................... (alama 2)

(i) Tumia kirejeshi 'O' katika sentensi ifuatayo:-

Mtu ambaye hutupa tope hujichafua mwenyewe. (alama 2)

(j) Kanusha sentensi ifuatayo:

Mgonjwa huyo alipona na kurejea nyurabani. (alama 2)

(k) Ainisha vihusishi katika sentensi:

Ame aliwasili mapema kuliko wengine halafu akaondoka. (alama 2)

(1) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno "chuma". (alama 4)

(i) ................................

(ii) ................................

(m) Unda noniino kutokana na kitenzi 'tafakari' ................................................ (alama 1)

(n) Eleza maana mbili za sentensi:

Tuliitwa na Juma ........................................................................................ (alama 2)

(o) Ainisha viambishi katika kitenzi:-

Tutaonana........................................................................................ (alama 2)

(p) Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi cha kinyume. (alama 2)

(q) Huku ukitoa mifano eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (alama 2)

(r) Akifisha kifungu kifuatacho:

Mzee alimwambia mwanawe njoo nikupeleke kwa babu yako angalau umjue mtoto aliuliza nani babu? (alama 4)

**ISIMUJAMII**

(a) Bainisha changamoto **tano** zinazoikabili lugha ya Kiswahili kama somo katika shule za upili nchini Kenya. (alama 5)

(b) Eleza namna **tano** za kukabiliana na changamoto ulizobainisha hapo juu. (alama 5)

# KISAWHILI

## KARATASI ya 3
## FASIHI
## 2011

### SEHEMU A: TAMTHILIA

**KITHAKA WA MBERIA:** *Kifo Kisimani*
***Swali la lazima***

1 "Alijiona pwagu. Lakini Butangi ina pwaguzi pia."
Eleza tofauti baina ya wahusika wanaorejelewa. (alama 20)

### SEHEMU B: RIWAYA

**S.A.MOHAMED:**
*Utengano* ***Jibu swali la 2 au la 3***

2 Eleza namna mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa riwaya ya Utengano:

(i) Kwelikinzani
(ii) Sadfa. **(alama 20)**

3 "Uhuru alioutaka na ulimwengu alioufahamu Maimuna umemdhuru hatimaye."
Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano **kumi.** (alama 20)

### SEHEMU C: USHAIRI
***Jibu swali la 4 au la 5***

**KUJITEGEMEA**

1. Nchi ni ile ambayo, imekita ardhini
Siyo ile iombayo, **ghaibu** na majirani
Taratibu siyo hiyo, wanachi twambizaneni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

2. Chumo lote na mitaji, leo limo maganjani
Bepari na wanyonyaji, wasalie maguguni

Shime utekelezaji, vingine havifanani
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

3. Twaishije tujihoji, wanachi humu nchini
Kila tunachohitaji, kupatakwe ugenini
Hiyo ni tete haviji, tongo tupangusaneni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

4. Kuomba wataalamu, ni mwendo haulingani
Tupate wa humu humu, wajuzi wa kila fani
Mbele washike hatamu, kwa mapimo na makini
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

5. Tuufuate wongozi, pamwe na nyingi imani
Tushiriki kila kazi, na mambo yalomkini
Mikopo ina kinyezi, si kitu cha tumaini
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

6. Yote hatuyatimizi, alotimiza ni nani
Lakini tuwe maizi, tusizurure mijini
Tukamshabilii kozi, kipanga au kunguni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

7. Shujaa itakiwavyo, aonekane vitani
Na sisi vita tunavyo, roho kwa roho ugani
'Kutegemea' vilivyo, kondo tujiamueni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

*Boukhet Amana: Malenga waMrima*

Mwinyihatibu Mohammed
Oxford University Press
1977

(a) Mtunzi wa shairi hili ana dhamira gani? (alama 2)

(b) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu moja. (alama 2)

(c) Eleza mambo **matatu** ambayo mshairi anashauri nchi ifanye ili kujitegemea. (alama 3)

(d) Taja aina moja ya idhini ya kishairi iliyojitokeza kwa wingi zaidi katika shairi na utoe mifano mitano ya matumizi yake. (alama 7)

(e) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi:

(i) Ghaibu

(ii) Tukamshabihi.

(alama 2)

**HAKI**

1. Haki watutisha, tusikuandame, kwa matendo yetu,
Watukorofisha, tusikuandame, kila penye kitu,
Mbona watugwisha, miba ituchonie, kwenye huu mwitu,
Tutokwe nautu!

2. Hatutakufanya, mwana kwa mvyele, aliyemzaa,
Haki watunyima, machumi ya mbele, na nyingi hadaa,
Tuchumayo nyanya, uchungu umbele, hatuna wasaa,
Haki twashangaa!

3. Na kambi nzima, kunaiyenea, hasa hapa petu,
Tunakutazama, kwa kuulizia, kuweza thubutu,
Na kwenye milima, ilotueka, kupandia watu,
Usifanyekatu!

4. Sio hao mabwana, waloteuliwa, kupata mwangaza,
Haki wakubana, lilotarajiwa, kwenye hichi kiza,
Ndevu kuchomana, wengine kuliwa, tukijiingiza,
**Kambi yatuviza!**

5. Haki huna njia, kizuizi mali, ndio njia panda,
Tukiifatia, hatufiki mbali, wengi tunaganda,
Sio yetu nia, lakini akili, mali ishapenda,
Haki yatuponza!

6. Wala hutasemwa, sababu ni nyoyo, kwisha haribika,
Ya mali kuchumwa, vyovyote iwavyo, itavyopatika,
Wakati mtumwa, ushatumwa ndivyo, na ushatufika,
Kwetu ni mashaka!

7. Haki hufanyiki, papitapo mambo, na vikubwa visa,
Watu hawataki, kutenda kijambo, tunu yao pesa,
Sisi kwetu dhiki, yatunisha tumbo, wao hata hisa,
Nandio yasasa!

8. Haki husimami, kwa viumbe sisi, tuvyojaaliwa,
Na huna ulimi, **kuweza tukisi,** tukageukiwa,
Zama za uchumi, zishashika kasi, nguvu zishapewa,
Haki wauliwa!

9. Iwe hivi haki, hakuna mmoja, akukumbukae,
Hatuna ashiki, kuvuta la haja, haki ituvae,
Mbona hatutaki, twalia na tija, haki iambae,
Hakitamati!

**Suleiman A. Ali:** ***Malenga Wapya***

(a) Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 2)

(b) Huku ukitoa mfano, eleza aina ya shairi hili. (alama 3)

(c) Taja na ufafanue tamathali ya usemi inayotawala katika shairi hili. (alama 3)

(d) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, onyesha aina tatu za idhini ya kishairi

katika shairi hili. (alama 6)

(e) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Mshairi ana maana gani kwa kusema;

(i) Kambi yatuviza

(ii) Kuwezatukisi.

(alama 2)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**K.W. WAMITILA:** *Mayai Waziri Wa Maradhi na Hadithi Nyinginezo*

***Jibu swali la 6 au la 7***

6 "Cheche ndogo hufanya moto mkubwa,"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama

4)

(b) Fafanua maudhui **manne** yanayohusiana na chanzo cha tukio linalorejelewa
katika dondoo hilo. (alama
8)

(c) Eleza matokeo **manne** ya tukio linalorejelewa katika dondoo. (alama 8)

7 "Mganga na wateja wake wote walikosa busara." Fafanua ukweli wa kauli hii kwa mifano **kumi** kutoka hadithi ya 'Siku ya Mganga.'

(alama 20)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

(a) Eleza maana ya malumbano ya utani. (alama 2)

(b) Bainisha sifa **nne** za malumbano ya utani. (alama 8)

(c) Fafanua majukumu **matano** ya malumbano ya utani katika jamii. (alama 10)

# KISWAHILI KARATASI YA KWANZA 2012

1 **Lazima**:

Wewe ni mkuu wa Baraza la Wanafunzi shuleni mwenu. Kumekuwa na visa vya wanafunzi kukiuka sheria za shule. Andika kumbukumbu za mkutano wa baraza hili uliofanyika kujadili suala hili.

2 Andika insha kuhusu umuhimu wa vijana katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

3 Andika insha inayobainisha maana ya methali: Chombo cha kuzama hakina usukani.

4 Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
Nilijaribu kuyafumbua macho yangu yaliyojaa uchovu kutokana na malimbikizo ya usingizi . . .

## KISWAHILI KARATASI YA pili 2012
## PILI

1 **UFAHAMU**: (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Nchi nyingi duniani zimetia sahihi mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Haki hizi ni pamoja na uhai, lishe bora inayotosha na makazi bora yaliyo salama. Hali kadhalika, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu inastahili kutolewa bure, iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Isitoshe, mtoto hastahili kupigwa, kudunishwa, wala kubaguliwa kwa namna yoyote ile; iwe kitabaka, kirangi, kijinsia au vinginevyo. Mtoto hapaswi kufanya kazi za kitumwa, nzito na za kushurutishwa. Vile vile, mtoto ana haki ya kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Fauka ya haya, mtoto anastahili kushirikishwa katika kufanya maamuzi yanayoweza kumwathiri maishani. Pia, mtoto ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum na habari kuhusu masuala mbalimbali. Pamoja na hayo, mtoto anastahili kupendwa na kuheshimiwa kimawazo na kihisia.

Haki za watoto zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, serikali na wazazi wakiwa katika mstari wa mbele. Hii ndiyo sababu serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba na sheria za nchi husika. Yeyote anayezikiuka anapasa kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Walakini, haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. Kuna watoto ambao hawajawahi hata kupata kibanda cha kuweka ubavu. Wengi wa hawa wamejipata wakiselelea kwenye mitaa na hata majaa ya miji na vijiji ambako hulazimika kupitisha usiku hata katika majira ya kipupwe na masika! Wengine hawapati chakula; licha ya kuwa wanatakiwa kupata chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi; kwani hata awamu moja ni adimu kupata! La kusikitisha ni kwamba wale wanaotarajiwa kuwa **vigogo** wa kuzilinda haki hizi ndio wanaoongoza katika kupalilia ukiukaji wazo. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kushinikizwa kufanya kazi za sulubu kipunda, kunyanyaswa kijinsia, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Baadhi ya wanaohusika na vitendo hivi hasi huwa wazazi au jamaa wa karibu kama vile wajomba, shangazi au wahudumu wa nyumbani.

Madhila yanayowapata watoto hayatokei tu katika mazingira ya nyumbani. Mateso huvuka mipaka na kufikia ngazi ya kimataifa. Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Linalokata maini ni kwamba baadhi ya viongozi katika mataifa haya hawafanyi lolote kuwanusuru. Lao huwa kuwatazama watoto wanaotakiwa kuwalinda wakigeuzwa kuwa mababe wa kuua na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia hulazimika kuvaa mabuti ya kijeshi ambayo **huwa nanga kwao** kubeba, licha ya bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani.

Mojawapo ya mambo ambayo viongozi nchini humu walilenga shabaha kuyafikia baada ya kujinyakulia uhuru ni elimu kwa wote. Hata hivyo, hii imekuwa kama ndoto isiyotabirika katika baadhi ya janibu. Ni kweli kwamba sera ya elimu bila malipo katika shule za msingi nchini humu inaendelea kutekelezwa. Hata hivyo, asilimia ya watoto na hata watu wazima wasiojua kusoma na kuandika ingali kubwa. Jukwaa la vijiji nchini humu na hata katika mataifa mengine ya ulimwengu wa tatu limesheheni idadi kubwa ya watoto wasioenda shuleni. Kichocheo kikuu cha hali hii ni kwamba wazazi na walezi wamejipata katika lindi la ufukara uliokithiri. Hata wanapojitahidi kujinyanyua na **kujikuna wajipatapo** kuyakidhi mahitaji ya kielimu ya wanao, wao hujipata wakitapatapa katika kinamasi hicho hicho cha ulitima. Matokeo ni kwamba watoto wa matajiri wanaendelea kuelimika huku wa maskini wakibakia kwenye kiza cha ujinga. **Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana**.

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima tuungane mikono na kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu utekelezaji wa haki za watoto. Twapaswa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati.

(a) Huku ukitoa mifano **minne**, eleza hali ya kinyume inayojitokeza katika aya ya pili. (alama 4)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(b) Eleza namna hali ya usalama inavyoathiri utekelezaji wa haki za watoto kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(c) Kwa kurejelea aya ya nne, onyesha mchango wa serikali katika kuwajibikia haki za watoto. (alama 3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(d) " Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu. (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. (alama 3)

(i) vigogo..........................................................................................................

(ii) huwa nanga kwao............................................................................................

(iii) kujikuna wajipatapo........................................................................................

**2** **UFUPISHO**: (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Wataalamu mbalimbali wamekuwa wakifanya utafiti kuhusu Ziwa Viktoria. Juhudi hizi za uchunguzi zimekuwa zikionyesha kwamba ziwa hili ambalo ndilo la pili kwa ukubwa miongoni mwa maziwa yenye maji matamu duniani linaangamia taratibu. Inakisiwa kuwa kukauka kwa ziwa hili kutahatarisha maisha ya watu zaidi ya milioni 30 ambao hulitegemea kwa chakula na mapato. Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Masuala ya Bahari na Uvuvi nchini ulionyesha kuwa Ziwa Viktoria linaangamia kwa kiasi cha mita tatu kila mwaka. Hivi sasa baadhi ya fuo zilizokuwa kwenye ziwa hili upande wa Kenya zimekauka. Mandhari ya fuo hizi nayo yameanza kutwaa sura mpya. Badala ya kupata madau na wavuvi wakiendesha shughuli zao katika maeneo haya, huenda isiwe ajabu kupata watoto wakicheza kandanda.

Rasilimali za samaki ziwani humu zinaendelea kudidimia huku wavuvi wakitupwa kwenye biwi la umaskini. Walisema wasemao kwamba akosaye la mama hata la mbwa huamwa. Wavuvi wamebuni mikakati ya kukabiliana na hali hii ambayo inatishia kukiangamiza kizazi chao. Wengi wao wameamua kufanya biashara maarufu kwa jina, 'bodaboda,' wengine wameingilia kilimo baada ya kushindwa kujikimu kimaisha kutokana na uvuvi. Wavuvi wanaoendelea kuvua samaki katika ziwa hili wamejipata katika hali ngumu ya kiuchumi. Hali hii imewalazimisha baadhi yao kuanza kuvua samaki katika maji ya mataifa jirani; jambo ambalo limewachongea, wengi wakatiwa mbaroni huku wengine wakinyanyaswa na maafisa wa usalama wa mataifa hayo jirani.

Sekta ya uchukuzi na mawasiliano nayo imeathirika si haba. Shughuli za uchukuzi katika ziwa hili zimetingwa na gugu-maji ambalo limetapakaa kote ziwani. Mbali na gugu-maji hili, shughuli za kilimo cha kunyunyizia maji zimetanzwa. Kadhalika, kupungua kwa viwango vya maji humu ziwani ni changamoto nyingine ambayo inawashughulisha wanaharakati wa mazingira. Inahofiwa kuwa mataifa ya Afrika Mashariki yanalipoteza ziwa hili hatua kwa hatua. Hakika, wanasayansi wa masuala ya bahari wameonya kuwa ziwa hili litakauka katika kipindi cha karne moja ijayo!

Ni dhahiri kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki ina jukumu la kulitunza ziwa hili kwa jino na ukucha. Serikali za nchi husika, hususan Kenya, Uganda na Tanzania zinapaswa kutekeleza sheria zinazodhibiti shughuli za uvuvi katika ziwa hili. Mathalan, kuna haja ya kuvua kwa misimu ili kukinga dhidi ya kuangamia kwa rasilimali za samaki. Wavuvi nao hawana budi kushauriwa

kuhusu umuhimu wa kufuata kanuni za uvuvi zilizowekwa na kutahadharishwa kuhusu madhara ya kuendesha uvuvi kiholela. Sheria kuhusu aina za nyavu za kuvulia pia inapaswa kutekelezwa vilivyo. Aidha, kuna haja ya serikali za muungano huu kukomesha shughuli za kilimo kandokando mwa ziwa hili, pamoja na kwenye mito iliyo katika ujirani wa ziwa lenyewe. Hatua hii itasaidia kukomesha kusombwa kwa udongo na mbolea kutoka mashambani hadi ziwani. Hali kadhalika, muungano huu unapaswa kuweka sheria za kusimamia matumizi ya maji. Hili litawadhibiti raia wenye mazoea ya kubadhiri maji.

Isitoshe, serikali za mataifa ya Afrika Mashariki hazina budi kuchunguza viwanda vinavyotupa taka ndani ya ziwa hili. Mbali na kuchafua maji, viwanda hivi vinaangamiza mimea na wanyama wa majini. Uchunguzi huo unapaswa pia kuhusisha mito inayomimina maji katika ziwa hili. Viwanda vyote vinavyotumia maji ya mito kama vile: Nzoia, Yala, Sondu-Miriu, Awach, Kuja na Kagera vinastahili kuchunguzwa pia.

Juhudi za kufikia ustawi wa kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki zinapaswa kutilia maanani uhifadhi wa Ziwa Viktoria. Kukauka kwa ziwa hili ni sawa na kukauka kwa maazimio na ndoto zote za serikali za nchi husika za kuboresha hali ya maisha ya raia wake. Wakati ni sasa.

(a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno 70 - 75. (alama 9, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho:**

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

**Nakala safi:**

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

(b) Huku ukitumia maneno 50 - 55, eleza masuala muhimu ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama 6, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho:**

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

**Nakala safi:**

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

3 **MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)

(a) Huku ukitoa mfano, fafanua dhana ya mzizi wa neno. (alama 2)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(b) Onyesha matumizi ya kiambishi **'ku'** katika sentensi ifuatayo:

Amani atakutengenezea mpini wa jembe kisha aelekee kule kwao. (alama 2)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(c) Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) Irabu ya mbele, wastani ..........................................................................................

(ii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini ...........................................................................

(d) Tumia kivumishi kionyeshi kisisitizi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya YA - YA kutunga sentensi. (alama 2)

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

(e) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali timilifu. (alama 2)

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

(f) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)

KN (N) + KT (T + E) + U + KN (N) + KT (T + E)

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

(g) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi changamano. (alama 2)

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

(h) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya: **koga** na **konga**. (alama 2)

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

(i) Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na nomino ya jamii. (alama 2)

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

(j) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. (alama 3)

(i) nywa (tendesha) .......................................................................................

(ii) la (tendeana).........................................................................................

(iii) vaa (tendwa) .........................................................................................

(k) Akifisha sentensi ifuatayo kubainisha dhana **tatu** tofauti.

Julius Kiptoo mwanawe Kung'u na Justine walikiletea kijiji chao sifa. (alama 3)

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

(l) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari.

<u>Naam</u>, ameleta <u>machache</u>. (alama 2)

.......................................................................................................................................

(m) Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu. (alama 2)

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

(n) (i) Eleza maana ya shadda. (alama 1)

.......................................................................................................................................

(ii) Onyesha panapotokea shadda katika neno: ‘ mteremko’. (alama 1)

.......................................................................................................................................

(o) Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

Sahibu yake alishikwa na kisunzi.

.......................................................................................................................................

(p) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari.

Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na viongozi wenye misimano thabiti mno.

(alama 3)

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

(q) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.

“ Shughuli yetu itamalizika kesho, ” mama alimwambia Juma. (alama 2)

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

(r) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo:

Watahiniwa hao walisoma maswali yote kwa makini. (alama 2)

.......................................................................................................................................

(s) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu/dhamira yake.

Funga majani matano matano kwa kila fungu. (alama 1)

.......................................................................................................................................

**4 ISIMUJAMII** (Alama 10)

Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha.

(a) Mazingira (alama 4)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(b) Madhumuni (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(c) Malezi (alama 4)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

# KISWAHILI KARATASI YA TATU 2012

## SEHEMU A: HADITHI FUPI

**K.W. Wamitila**: *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*

1 (a) Eleza nafsi ya usimulizi iliyotumiwa katika hadithi ya "Mkimbizi". (alama 3)

(b) Bainisha mifano **mitatu** ya mbinu rejeshi katika hadithi hii na ueleze umuhimu wa kila mojawapo. (alama 9)

(c) "Ukimbizi ni kikwazo cha maendeleo." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi hii. (alama **8)**

## SEHEMU B: RIWAYA

**Said A. Mohamed**: *Utengano*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2 'Lo, ama wewe mchawi,... Cheleko ... nakuvisha kilemba.'

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama **4)**

(b) Andika tamathali **mbili** za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama **4)**

(c) 'Wewe mchawi.' Onyesha jinsi kauli hii inavyomwafiki mzungumziwa kwa kurejelea riwaya. (alama 12)

3 "Wanawake katika *Utengano* ni vyombo vikuu vya ukiukaji wa haki za kibinadamu." Thibitisha. (alama 20)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**Kithaka wa Mberia**: *Kifo Kisimani*

*Jibu swali la 4 au la 5.*

**4** "Mtukufu Mtemi anafurahia sana ... Kama ujuavyo, anapenda sana watoto... Kwa hakika, kama mzazi, hana kifani katika Butangi nzima."

(a) (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Taja na utoe mfano wa sifa **moja** ya mzungumzaji inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(iii) Fafanua vichocheo **vinne** vya sifa uliyotaja katika (ii) hapa juu. (alama 4)

(b) Onyesha jinsi wanyonge katika *Kifo Kisimani* wanavyochangia katika ukandamizaji wao. (alama 10)

**5** "Anwani: '*Kifo Kisimani*' inaafiki tamthilia hii. Thibitisha. (alama 20)

## SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au la 7.*

**6** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**Said A. Mohamed**: *Mbele Ya Safari*

1. Ilipoanza safari, ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

2. Njaa ikawa thabiti, na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati, tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki
Tulijizatiti

3. Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari, utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari, juhudi iliyobaki
Tulijizatiti

4. Ile ilikuwa ndoto, mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto, sahala 'mekuwa dhiki
Wagombania kipato, utashi haukatiki
Na kutabakari

5. Msafara ukasita, kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita, mlima haupandiki
Basi sote 'kajipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

6. Tukiwa migongo wazi, tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi, kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia

7. Wakafikia makazi, ya pumbao na ashiki
Huko wakajibarizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

8. Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema mate, kwa umati halaiki
Imezima nia yote, kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

(a) Eleza safari inayorejelewa katika shairi hili. (alama 2)

(b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. (alama 6)

(c) Taja na ueleze bahari **mbili** za shairi hili ukizingatia: (alama 4)

(i) mizani;

(ii) vina.

(d) Andika ubeti wa **saba** kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(e) Eleza umuhimu wa aina **mbili** za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita. (alama 4)

**7** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

1. Wakati tunywapo chai hapa upenuni
Na kuwatazama watoto wetu
Wakicheza bembea kwa furaha
Tujue kamba ya bembea yetu imeshalika
Na bado kidogo tutaporomoka

2. Kulikuwa na wakati ulinisukuma juu
Nikaenda zaidi ya nusu duara
Kulikuwa na wakati nilikudaka
Ulipokaribia kuanguka
Na kulikuwa na wakati tulibebana kwa zamu
Mmoja wima akisukuma mwingine amekaa

3. Wakati huo, japo tulipaa mbele na nyuma
Tulicheka kwa matumaini yaliyotiwa chumvi
Na kisha tukaongozana jikoni kupika chajio
Ilikuwa adhuhuri yetu

4. Sasa tukisubiri ndoto tusizoweza kuzitekeleza tena
Tumalizie machicha ya chai yetu ya jioni
Bila ya kutematema na kwa tabasamu
Na baada ya hapo tujilambe utamuutamu
Uliobakia kwenye midomo yetu

5. Tukikumbuka siku ilee ya kwanza
Tulipokutana jioni chini ya mwembe
Tukitafuta tawi zuri gumu
La kufunga bembea yetu
Naye mbwa Simba akisubiri

6. Lakini kabla hatujaondoka kimyakimya
Kukamilisha nusu duara iliyobaki
**Tuhakikishe vikombe vyetu ni safi.**

(E. Kezilahabi)

(a) Fafanua maana ya kijuujuu na maana ya kitamathali ya shairi hili. (alama 6)

(b) Bainisha matumizi ya vipengele vifuatavyo katika shairi: (alama 6)

(i) Usimulizi;
(ii) Usambamba;
(iii) Taswira.

(c) Tambulisha mzungumzaji (nafsi-neni) katika shairi hili. (alama 2)

(d) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 4)

(e) Eleza maana ya mshororo: "Tuhakikishe vikombe vyetu ni safi." (alama 2)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8** (a) Huku ukitoa mifano, fafanua majukumu **matano** ya nyimbo. (alama 10)

(b) "Mwimbaji ana nafasi muhimu katika kufanikisha uwasilishaji wa wimbo." Thibitisha. (alama 10)

# 2013 K.C.S.E Kiswahili
# Paper 1

## KCSE KISWA PAPER1

**1 Lazima:**

Wewe ni meneja katika kampuni ya Jitihada ambapo pamekuwa na visa vya ukiukaji wa maadili ya kikazi. Waandikie wafanyakazi memo kuwaonya dhidi ya jambo hili.

2 "Rununu (simutamba) imeleta athari mbaya katika jamii." Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Usitukane wakunga na uzazi ungalipo.

4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
Moyo wangu ulidunda kwa matarajio makuu ...

# KARATASI YA PILI

**1. UFAHAMU:** (Alama 15)
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali,*

Gari lake kuukuu lilikuwa linapambana na barabara yenye mashimo yaliyoshiba na kutapika maji ya mvua ambayo sasa ilikuwa inaanza kupusa. Japo daima alipambana na usukani kunako mashimo haya yaliyotosha kuitwa magenge, alishukuru kwa hali hii. Vipi angeweza kulidhibiti gari lake hili kwenye barabara iliyosakafiwa nayo ikahitimu? Magurudumu haya yaliyong'ara kama upara wa shaibu aliyekula chumvi hadi ikamwogopa yangetii uelekezi wake? Mara ngapi gari hili limetaka kumwasi barabarani? Haya yalikuwa baadhi ya maswali yaliyompitikia akilini. Hakujitakilifu kutaka **kuyapa mji** maana mara ile mawazo yake yalitekwa na kubwagwa katika nchi ya mbali - nchi ambayo sasa aliiona kama sinema akilini mwake.

Alipofika nyumbani aliliegesha gari lake na kufululiza ndani. Siku mbili zilikuwa zimepita akiwa pale kazini. Madaktari kama yeye hawakuwa wengi. Alikuwa miongoni mwa madaktari wenye ujuzi katika hospitali hii ya kitaifa. Wenzake wengi walikuwa wamehamia ughaibuni walikokwenda kutafuta maisha. Mshahara wao wa mkia wa mbuzi uliwasukuma na kuwatema nje ya nchi yao. Wengi wa waliohamia ng'ambo waliona vigumu kubaki katika ajira ambayo kivuno chake kilishindwa kumvusha mtu hata nusu ya kwanza ya mwezi. Malalamishi ya kulilia ujira wa heshima yaligonga kwenye masikio yaliyotiwa zege. Na kweli wanavyosema, mwenye macho haambiwi tazama. Basi walitazama hapa na pale wakaona penye mianya ya matumaini, nao wakaiandama.

Hadi leo hii hamna la mno lililofanyika. Ndiyo maana Daktari Tabibu anarudi nyumbani tangu kuingia kazini hiyo juzi alfajiri. Hafanyi kwa kuwa katosheka, maana pia yeye ana dukuduku. Ana shaka ya mustakabali wake ikiwa mazingira ni haya ya kumsoza, maana umri nao unazidi kumla. Japo anatia na kutoa, mizani ya hesabu yake imeasi ulinganifu.

Daktari Tabibu waama ni mfungwa. Ametekwa na kuzuiwa katika kupenda na kuchukia mambo. Ni kama mti uliodumaa. Anatamani barabara nzuri za lami. Anatamani mshahara wa kumwezesha kukidhi mahitaji yake na kutimiza majukumu yake ya kimsingi. Jana amesema na rafiki yake aliye ng'ambo kwa simu ambayo sasa imetulia mkabala naye. Ingawa mwenzake huyu alikuwa mchangamfu na kumdokolea hali ya maisha ya kuridhisha kule ugenini kama vile wanataaluma kuenziwa, yapo vilevile yaliyomtia unyonge moyoni. Upweke ndio uliomtia **fukuto** kuu. Licha ya hela zote hizo za kupigiwa mfano, watu hawana muda wa kutembeleana na kujuliana hali au hata kukutana tu mkahawani wakashiriki mlo. Eti ni kila mtu na hamsini zake. Halafu ipo changamoto ya hali ya hewa. Baridi ya ng'ambo haifanyi mzaha katika kumtafuna mtu. Ni hali tofauti na ile aliyoizoea.
Daktari Tabibu alizitia kauli za rafiki yake kwenye mizani ya moyo wake. Akawaza ikiwa kweli si bora kulemazwa na mzizimo ugenini badala ya kuishi katika kinamasi cha kuumbuliwa nyumbani. Kishapunde lilimjia wazo la marehemu nyanyake na wengineo kama yeye waliofadhili masomo yake kupitia kwa serikali na njia ya kodi. Je, si usaliti huu? Vipi aikimbie nchi kabla ya kuihudumia ilhali imemjenga hadi kuwa daktari? Na je, wafanyakazi wake wa nyumbani watakwenda wapi?Atawaambiaje kuwa sasa hahitaji huduma zao kwa kuwa anakimbia nchi yake?

Mawazo yake yalikatizwa na simu iliyolia na kumshtua. Alipoitazama aliiona imeng'ara kwa mwangaza ulioweka wazi jina la mpigaji. Alifahamu kuwa leo hii tena dharura nyingine ilikuwa inamwalika hospitalini. Mwili wake ulimsaliti ingawa moyo wake ulimkumbusha kuwa lisilo budi hutendwa. Hapo ndipo alipoiinua ile simu tayari kusema na mwenzake upande wa pili.

"Haloo!" Sauti nyororo kutoka upande wa pili iliita.
"Haloo!"
"Naam! Dharura nyingine tena daktari. Unaombwa kuokoa maisha mengine tena!"
"Haya. Ila mwanzo nitahitaji kujimwagia maji, na pale pale akaikata ile simu.
Daktari Tabibu aliingia hamamuni huku kajifunga taulo kiunoni tayari kuoga. Aliyafungulia maji lakini ule mfereji uligoma kutapika maji. Ulikuwa umekauka kabisa. Daktari Tabibu aliduwaa pale. Aliufunga ule mfereji kabla ya kuiaga bafu.

(a) Eleza sababu nne zinazowafanya wataalamu kuhamia nchi za nje. (alama 4)

(b) "Hakuna masika yasiyokuwa na mbu." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hali ya waliohamia ng'ambo. (alama 3)

(c) Fafanua athari **tatu** zinazoikumba nchi ya msimulizi kutokana na uhamiaji ng'ambo wa wataalamu. (alama 3)

(d) Eleza mchango wa teknolojia kwa kurejelea kifungu. (alama 3)

(e) Eleza maana za msamiati ufuatao kulingana na taarifa. (alama 2)

(i) kuyapa mji

(ii) fukuto

**2. UFUPISHO:** (Alama 15)

*Soma kijungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Wakenya walipoipitisha katiba mpya waliidhinisha mfumo wa ugatuzi. Katika mfumo huu, mamlaka ya serikali kuu katika uongozi, usimamizi na utumiaji wa rasilimali za nchi hupunguzwa. Kiasi fulani cha mamlaka hutwaliwa na maeneo ya ugatuzi. Suala hili halikuzingatiwa katika katiba ya awali ambapo mamlaka yote yalikuwa mikononi mwa serikali kuu. Kutokana na upana na wingi wa maeneo nchini, iliiwia vigumu serikali kuu kuhakikisha kwamba kulikuwa na usawa wa kimaendeleo katika sehemu zote nchini.

Kwa mujibu wa katiba mpya, serikali kuu haina budi kuyasaidia maeneo yote ya ugatuzi ili yaweze kujinyanyua kiuchumi na kuboresha hali za maisha za wakazi wake. Vile vile ni jukumu la kila eneo la ugatuzi kuweka mikakati madhubuti ili kuchunguza na kubainisha rasilimali zote katika maeneo husika. Hili litasaidia kuvumbua rasilimali ambazo zinaweza kuchangia katika ustawishaji wa maeneo haya. Maeneo haya pia yanatakiwa kutafuta mbinu zitakazofanikisha uzalishaji na utumiaji wa rasilimali hizi kwa njia endelevu. Mojawapo ya mbinu hizi ni uongezaji thamani katika rasilimali yoyote inayozalishwa kwenye eneo mahususi.

Maeneo mengi ya ugatuzi nchini humu yanategemea kilimo cha ufugaji kama mhimili wa uchumi. Licha ya kuwa nguzo, kilimo hiki hakijawahi kupigiwa darubini vizuri kwa lengo la kukiimarisha ili kiwanufaishe wenyeji kikamilifu. Aghalabu wafugaji wengi huandama mbinu za jadi za ufugaji ambazo haziwahakikishii ongezeko la mapato. Isitoshe, wafugaji hawa wanakabiliwa na tatizo katika soko la mifugo ambapo wengi hupunjwa na matapeli. Pamoja na haya, baadhi ya wakazi huuza mifugo nje ya nchi wakiwa wazimawazima bila kuwazia matokeo ya kitendo hiki. Si ajabu kuwaona ng'ombe, ngamia, mbuzi na kondoo wakipakiwa kwenye malori na kusafirishwa nje ya nchi. Ukweli ni kwamba jambo hili ni hatari sana, si kwa uchumi wa maeneo husika tu, bali pia kwa Kenya kwa jumla. Hii ni kwa kuwa walionunua mifugo wazimawazima wanaweza kuhiari kutowachinja na badala yake kuwatumia kama mbegu za kuzalisha mifugo wao. Hapa pana hatari ya maeneo haya kupoteza wateja kwani baada ya muda huenda wanaonunua mifugo wakajitosheleza na kukosa kuja kununua mifugo wengine. Hali ikiwa hivyo, maeneo yaliyotegemea soko hili huenda yakalipoteza taratibu, na bila shaka kupoteza natija inayotokana na soko lenyewe.
Ili kudhibiti hali hii, itakuwa bora ikiwa viwanda vya kuchinjia mifugo na kupakia nyama vitajengwa katika maeneo haya ya ugatuzi. Hili litawawezesha wakazi kuuza nyama badala ya kuuza mifugo wazimawazima. Fauka ya haya, maeneo haya yatajikinga dhidi ya kupoteza bidhaa zinazotokana na mifugo. Hizi ni kama vile ngozi, kwato na pembe ambazo bila shaka zina natija kuu. Ngozi kwa mfano, ni bidhaa muhimu sana katika sekta ya utengenezaji wa mavazi na mifuko. Viwanda vinavyotumia ngozi kama malighafi vikijengwa katika maeneo haya, wakazi wake watanufaika si haba. Mathalani, viwanda vya kutengenezea viatu, mishipi, mifuko

na nguo vikianzishwa, wawekezaji watalazimika kuanzisha viwanda vingine vitegemezi. Kadhalika, ni dhahiri kwamba bidhaa zinazotokana na ngozi huhitaji kutiwa nakshi, Kuanzishwa kwa viwanda hivi basi kutazua haja ya kuanzishwa kwa viwanda vya kutengenezea rangi, pamoja na maduka ya kuuza bidhaa yenyewe. Isitoshe, gundi ya kugandisha bidhaa hizl itahitajika, hivyo kusababisha haja ya kuanzishwa kwa kiwanda cha gundi. Matokeo ya shughuli hizi zote ni kuzalishwa kwa nafasi anuwai za kazi kwa wakazi. Hili litakuwa na matokeo zaidi chanya, hususan kwa vijana. Badala ya kushiriki ulevi na burudani zinazowahatarisha, wataweza kujitafutia riziki katika viwanda hivi.

Juu ya hayo, mfumo wa ugatuzi utayawezesha maeneo husika kuongezea thamani utoaji wa huduma za kijamii na kiutawala kulingana na mahitaji ya maeneo haya. Ni muhimu hata hivyo kuzingatia kwamba kila eneo la ugatuzi lina upekee wake, navyo vipaumbele hutofautiana kulingana na maeneo. Kuna yale ambayo yatasisitiza usalama, mengine ujenzi na uimarishaji wa miundomsingi kama vile barabara, vituo vya afya na hata taasisi za elimu. La muhimu ni wakazi wa maeneo husika kubainisha ni lipi litatekelezwa kwanza.

Kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Kufanikiwa kwa mfumo wa ugatuzi kutategemea juhudi za kila mkazi wa eneo husika. Ni muhimu kila mkazi kujiona kuwa mmiliki wa eneo zima la ugatuzi na kuwajibika katika kuliendeleza kwa hali na mali. Uwajibikaji huu unajumuisha uteuzi wa viongozi wenye muono mzuri na ambao watawawezesha kuyankia malengo yao ya kimaendeleo. Hakika, mustakabali na uwepo wa eneo la ugatuzi utakuwa zao la maamuzi ya wanaeneo. Vilevile ufanisi wa maeneo ya ugatuzi utakuwa msingi wa ufanisi wa taifa kwa jumla.

(a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 85-90.

(alama 8, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

(b) Kwa kutumia maneno 75-80, bainisha masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama 7,1 ya mtiririko)

**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

**3 MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)**

(a) (i) Eleza maana ya sauti mwambatano. (alama2)

(ii) Andika sauti mwambatano inayotarnkiwa kwenye ufizi. (alama 1)

(b) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa kielezi.

Komu ameshona nguo <u>nzuri</u> na kuiuza sokoni. (alama 1)

(c) Tunga sentensi mojamoja kubainisha: (alama 4)

i) kihusishi cha wakati

(ii) kivumishi cha pekee chenye maana, "bila kubagua".

(d) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi.

Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama. (alama 2)

(e) Bainisha mofimu katika neno:

atamnywea (alama 3)

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo:

Madebe hayo yatasafirishwa pamoja na nyundo hizi. (alama 2)

(g) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo:

Ingawa mshahara wake si mkubwa anaikimu familia yake. (alama 2)

(h) Tunga sentensi **tatu** kuonyesha matumizi **matatu** tofauti ya kiambishi 'li'. (alama 3)

(i) (i) Eleza maana ya sentensi ya masharti. (alama 1)

(ii) Tunga sentensi ya masharti. (alama 2)

j) Tumia kiwakilishi cha 'a' unganifu katika sentensi kuonyesha:

(i) umilikaji (alama 2)

(ii) nafasi katika orodha au nafasi katika kundi (alama 2)

(k) Tunga sentensi yenye kikundi tenzi chenye muundo ufuatao:

Kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, nomino (alama 2)

(1) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi **mawili** tofauti ya kistari kirefu.
alama 2)

(m) Unganisha sentensi zifuatazo kuwa sentensi moja bila kurudia kitenzi.

Osore amempigia Ngungui simu. Ngungui amempigia Osore simu. (alama 2)

n) Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha vitenzi vilivyomo kuwa nomino:

Mayaka anapotumbuiza huchekesha sana. (alama 2)

(o) Andika maana **tatu** za neno: kanda. (alama 3)

(p) Andika visawe **viwili** vya nahau: enda kombo. (alama 2)

**ISIMUJAMII:** (Alama 10)

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Haya ng'ara ... Ng'ara leo! Nguo motomoto. Ng'ara leo kwa bei rahisi. Hamsini hamsini shati. Kuona ni bure. Bure kwa bure. Shika mwenyewe ujionee. Bei nafuu. Bei ya starehe. Haya haya. Usikose mwanangu! Hamsa! *Fifty!* Hamsa! *Fifty!* Hamsa na nyingine.

(a) Bainisha sajili ya mazungumzo haya. (alama 2)

(b) Eleza sifa **nane** za sajili hii kwa kurejelea kifungu hiki. (alama 8)

## KARATASI YA TATU

### SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1. Lazima**

2.

(a) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya vitanza ndimi. (alama 2)

(b) Fafanua majukumu **sita** ya vitanza ndimi katika jamii. (alama 6)

(c) Eleza mbinu **sita** unazoweza kutumia katika kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi. (alama 12)

### SEHEMU B: RIWAYA

**Said A. Mohamed:** *Utengano*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2. "Walifanya kazi, walimenyeka.
Lakini walilala na njaa ...
Njaa, ndiyo ilikuwa misumeno
Iliyokeketa matumbo yao. ..."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha tamathali **mbili** za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Kwa kurejelea riwaya. Onyesha jinsi wanyonge walivyomenyeka. (alama 12)

3. Jadili uhusiano uliopo kati ya wahusika na maudhui kwa kurejelea wahusika wafuatao:
(a) Shoka (alama 10)
(b) Kazija (alama 10)

**SEHEMU C: TAMTHILIA T. Arege:** *Mstahiki Meya*

*Jibu swali la 4 an la 5.*

4. Jadili mchango wa Wanacheneo katika kuivunja jamii yao. (alama 20)

5 "Ndiyo hivyo bwana. Elimu yetu hapa ni ya kawaida mno. Haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali."

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
(b) Bainisha tamathali ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili ukirejelea msemaji wa kauli hii. (alama 2)
(c) Kwa kurejelea tamthilia, fafanua mifano mingine **saba** ya matumizi ya tamathali uliyotaja katika (b) hapo juu. (alama 14)

**SEHEMU D: USHAIRI**

*Jibu swali la 6 au la 7.*

*6.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Sinongi aushi yangu, hii leo, kwa ukungu wa ujana,
Nikaiga rika langu, kwa vileo na mbio za wasichana,
Kiwa ni riziki yangu, mapokeo, kuoa na kuona,
Ni wakati utanena.

Nashukuru kwa ugumba, wenye ndimi, wanipagazao nao,
Wapitao wakiimba, eti mimi, ningapenda hali zao,
Haupandiki mgomba, wana nyemi, fisadi wa hadhi zao,
Eti ni kwa raha zao.

Ni lipi lenye kukera, kwa Muumbi, marufuku kwenye misa,
Ni mtu kuwa hawara, wa vitimbi, ama alozawa tasa?
Ugumba na ukapera, sio dhambi, wala haujawa kosa,
Waama sina makosa.

Bora tungeni vitabu, magazeti, mutangaze kwa rediyo,
Muwaite watribu, kina Siti, watuzwa ilimu hiyo,
Na zaidi muhutubu, kwa umati, muwambe ambayo siyo
Kwalo sichafuki moyo.

Hidhuru yote ni bure, sio kitu, kudhiki asodhikika,
Siwi nikaona ghere, lailatu, nyota njema itafika,

Kwa shangwe na njerejere kila mtu, mdomo utarumuka,
Akiri amejibika.
**(Mwalaa M. Nyanje)**

(a) Eleza jambo ambalo mzungumzaji (nafsineni) katika shairi hili anasingiziwa. (alama 2)

(b) Fafanua mambo **matano** ambayo mzungumzaji (nafsineni) anapinga katika shairi hili. (alama 5)

(c) Eleza umuhimu wa viishio vya beti za shairi hili. (alama 2)

(d) Andika ubeti wa **tatu** kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(e) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 5)

(f) Bainisha matumizi **mawili** ya tasfida katika shairi hili. (alama 2)

**7.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

1. Huno wakati mufti, vijana nawausia.
Msije juta laiti. mkamba sikuwambia.
Si hayati si mamati. vijana hino dunia.
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

2. Japo aula kushufu,na machoni vyavutia.
Dunia wana dhaifu, yaugua nisikia.
Vijana nawasarifu, falau mkisikia,
Ukiona vyang'aria, tahadhari vitakula.

3. Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria.
Msije andama baa, makaa kujipalia.
Jepusheni na zinaa. madhara kukadiria.
Uonapo vyang'aria. tahadhari vitakula.

4. Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia,
Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia.
Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia,
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

5. Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita ja umeme, leo yao sitoria,
Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia,
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

6. Nambie faida gani, nambie ipi fidia?
Upatayo hatimani, waja wakikufukia,
Ila kufa kama nyani, kasoro yako mkia,
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

7. Kikiki ikaze karaba, u kijana vumilia,
Ujifanye kama kwamba, u jiwe huna hisia,
Wakwambe watalokwamba, kwa lolotevumilia.
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

8 Vyatiririka tiriri, vina vyanikubalia,
Alo bora mshairi, pa tamu humalizia,
Nahitimisha shairi, dua ninawapigia,
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

9. Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia,
Wakingie wanarika, na anasa za dunia,
Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia,
Uonapo 'vyang'aria. tahadhari vitakula.

**(Mwalaa M. Nyanje)**

(a) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 4)

(b) Fafanua kwa kutoa mifano. mbinu **nne** alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 8)

(c) Nafsineni (mzungumzaji) katika shairi hili inasema na pande mbili. Zieleze pande hizo. (alama 2)

(d) Eleza umuhimu wa maswali ya balagha katika shairi hili. (alama 3)

(e) Bainisha toni ya shairi hili. (alama 3)

**SEHEMU E: HADITHI FUPI**

**K Walibora na S. A. Mohamed:** *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

"Kikaza" **(Robert Oduori)**

8. 'Wakaacha chungu kinatokota - bila kuivisha chakula'. Kwa hakika walijibu. "Ndio mtindo, na sisi tulifuata mitindo."

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Onyesha jinsi Wanatekede wanavyofuata mitindo na kuacha chungu kinaiokota bila kuivisha chakula. (alama 16)

## KCSE KISWA PAPER1

**1 Lazima:**

Wewe ni meneja katika kampuni ya Jitihada ambapo pamekuwa na visa vya ukiukaji wa maadili ya kikazi. Waandikie wafanyakazi memo kuwaonya dhidi ya jambo hili.

2 "Rununu (simutamba) imeleta athari mbaya katika jamii." Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Usitukane wakunga na uzazi ungalipo.

4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
Moyo wangu ulidunda kwa matarajio makuu ...

# KARATASI YA PILI

**1. UFAHAMU:** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali,*

Gari lake kuukuu lilikuwa linapambana na barabara yenye mashimo yaliyoshiba na kutapika maji ya mvua ambayo sasa ilikuwa inaanza kupusa. Japo daima alipambana na usukani kunako mashimo haya yaliyotosha kuitwa magenge, alishukuru kwa hali hii. Vipi angeweza kulidhibiti gari lake hili kwenye barabara iliyosakafiwa nayo ikahitimu? Magurudumu haya yaliyong'ara kama upara wa shaibu aliyekula chumvi hadi ikamwogopa yangetii uelekezi wake? Mara ngapi gari hili limetaka kumwasi barabarani? Haya yalikuwa baadhi ya maswali yaliyompitikia akilini. Hakujitakilifu kutaka **kuyapa mji** maana mara ile mawazo yake yalitekwa na kubwagwa katika nchi ya mbali - nchi ambayo sasa aliiona kama sinema akilini mwake.

Alipofika nyumbani aliliegesha gari lake na kufululiza ndani. Siku mbili zilikuwa zimepita akiwa pale kazini. Madaktari kama yeye hawakuwa wengi. Alikuwa miongoni mwa madaktari wenye ujuzi katika hospitali hii ya kitaifa. Wenzake wengi walikuwa wamehamia ughaibuni walikokwenda kutafuta maisha. Mshahara wao wa mkia wa mbuzi uliwasukuma na kuwatema nje ya nchi yao. Wengi wa waliohamia ng'ambo waliona vigumu kubaki katika ajira ambayo kivuno chake kilishindwa kumvusha mtu hata nusu ya kwanza ya mwezi. Malalamishi ya kulilia ujira wa heshima yaligonga kwenye masikio yaliyotiwa zege. Na kweli wanavyosema, mwenye macho haambiwi tazama. Basi walitazama hapa na pale wakaona penye mianya ya matumaini, nao wakaiandama.

Hadi leo hii hamna la mno lililofanyika. Ndiyo maana Daktari Tabibu anarudi nyumbani tangu kuingia kazini hiyo juzi alfajiri. Hafanyi kwa kuwa katosheka, maana pia yeye ana dukuduku. Ana shaka ya mustakabali wake ikiwa mazingira ni haya ya kumsoza, maana umri nao unazidi kumla. Japo anatia na kutoa, mizani ya hesabu yake imeasi ulinganifu.

Daktari Tabibu waama ni mfungwa. Ametekwa na kuzuiwa katika kupenda na kuchukia mambo. Ni kama mti uliodumaa. Anatamani barabara nzuri za lami. Anatamani mshahara wa kumwezesha kukidhi mahitaji yake na kutimiza majukumu yake ya kimsingi. Jana amesema na rafiki yake aliye ng'ambo kwa simu ambayo sasa imetulia mkabala naye. Ingawa mwenzake huyu alikuwa mchangamfu na kumdokolea hali ya maisha ya kuridhisha kule ugenini kama vile wanataaluma kuenziwa, yapo vilevile yaliyomtia unyonge moyoni. Upweke ndio uliomtia **fukuto** kuu. Licha ya hela zote hizo za kupigiwa mfano, watu hawana muda wa kutembeleana na kujuliana hali au hata kukutana tu mkahawani wakashiriki mlo. Eti ni kila mtu na hamsini zake. Halafu ipo changamoto ya hali ya hewa. Baridi ya ng'ambo haifanyi mzaha katika kumtafuna mtu. Ni hali tofauti na ile aliyoizoea.

Daktari Tabibu alizitia kauli za rafiki yake kwenye mizani ya moyo wake. Akawaza ikiwa kweli si bora kulemazwa na mzizimo ugenini badala ya kuishi katika kinamasi cha kuumbuliwa nyumbani. Kishapunde lilimjia wazo la marehemu nyanyake na wengineo kama yeye waliofadhili masomo yake kupitia kwa serikali na njia ya kodi. Je, si usaliti huu? Vipi aikimbie nchi kabla ya kuihudumia ilhali imemjenga hadi kuwa daktari? Na je, wafanyakazi wake wa nyumbani watakwenda wapi?Atawaambiaje kuwa sasa hahitaji huduma zao kwa kuwa anakimbia nchi yake?

Mawazo yake yalikatizwa na simu iliyolia na kumshtua. Alipoitazama aliiona imeng'ara kwa mwangaza ulioweka wazi jina la mpigaji. Alifahamu kuwa leo hii tena dharura nyingine ilikuwa inamwalika hospitalini. Mwili wake ulimsaliti ingawa moyo wake ulimkumbusha kuwa lisilo budi hutendwa. Hapo ndipo alipoiinua ile simu tayari kusema na mwenzake upande wa pili.

"Haloo!" Sauti nyororo kutoka upande wa pili iliita.
"Haloo!"
"Naam! Dharura nyingine tena daktari. Unaombwa kuokoa maisha mengine tena!"
"Haya. Ila mwanzo nitahitaji kujimwagia maji, na pale pale akaikata ile simu.
Daktari Tabibu aliingia hamamuni huku kajifunga taulo kiunoni tayari kuoga. Aliyafungulia maji lakini ule mfereji uligoma kutapika maji. Ulikuwa umekauka kabisa. Daktari Tabibu aliduwaa pale. Aliufunga ule mfereji kabla ya kuiaga bafu.

(b) Eleza sababu nne zinazowafanya wataalamu kuhamia nchi za nje. (alama 4)

(b) "Hakuna masika yasiyokuwa na mbu." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hali ya waliohamia ng'ambo. (alama 3)

(c) Fafanua athari **tatu** zinazoikumba nchi ya msimulizi kutokana na uhamiaji ng'ambo wa wataalamu. (alama 3)

(d) Eleza mchango wa teknolojia kwa kurejelea kifungu. (alama 3)

(e) Eleza maana za msamiati ufuatao kulingana na taarifa. (alama 2)

(i) kuyapa mji

(ii) fukuto

**2. UFUPISHO:** (Alama 15)
*Soma kijungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Wakenya walipoipitisha katiba mpya waliidhinisha mfumo wa ugatuzi. Katika mfumo huu, mamlaka ya serikali kuu katika uongozi, usimamizi na utumiaji wa rasilimali za nchi hupunguzwa. Kiasi fulani cha mamlaka hutwaliwa na maeneo ya ugatuzi. Suala hili halikuzingatiwa katika katiba ya awali ambapo mamlaka yote yalikuwa mikononi mwa serikali kuu. Kutokana na upana na wingi wa maeneo nchini, iliiwia vigumu serikali kuu kuhakikisha kwamba kulikuwa na usawa wa kimaendeleo katika sehemu zote nchini.

Kwa mujibu wa katiba mpya, serikali kuu haina budi kuyasaidia maeneo yote ya ugatuzi ili yaweze kujinyanyua kiuchumi na kuboresha hali za maisha za wakazi wake. Vile vile ni jukumu la kila eneo la ugatuzi kuweka mikakati madhubuti ili kuchunguza na kubainisha rasilimali zote katika maeneo husika. Hili litasaidia kuvumbua rasilimali ambazo zinaweza kuchangia katika ustawishaji wa maeneo haya. Maeneo haya pia yanatakiwa kutafuta mbinu zitakazofanikisha uzalishaji na utumiaji wa rasilimali hizi kwa njia endelevu. Mojawapo ya

mbinu hizi ni uongezaji thamani katika rasilimali yoyote inayozalishwa kwenye eneo mahususi.

Maeneo mengi ya ugatuzi nchini humu yanategemea kilimo cha ufugaji kama mhimili wa uchumi. Licha ya kuwa nguzo, kilimo hiki hakijawahi kupigiwa darubini vizuri kwa lengo la kukiimarisha ili kiwanufaishe wenyeji kikamilifu. Aghalabu wafugaji wengi huandama mbinu za jadi za ufugaji ambazo haziwahakikishii ongezeko la mapato. Isitoshe, wafugaji hawa wanakabiliwa na tatizo katika soko la mifugo ambapo wengi hupunjwa na matapeli. Pamoja na haya, baadhi ya wakazi huuza mifugo nje ya nchi wakiwa wazimawazima bila kuwazia matokeo ya kitendo hiki. Si ajabu kuwaona ng'ombe, ngamia, mbuzi na kondoo wakipakiwa kwenye malori na kusafirishwa nje ya nchi. Ukweli ni kwamba jambo hili ni hatari sana, si kwa uchumi wa maeneo husika tu, bali pia kwa Kenya kwa jumla. Hii ni kwa kuwa walionunua mifugo wazimawazima wanaweza kuhiari kutowachinja na badala yake kuwatumia kama mbegu za kuzalisha mifugo wao. Hapa pana hatari ya maeneo haya kupoteza wateja kwani baada ya muda huenda wanaonunua mifugo wakajitosheleza na kukosa kuja kununua mifugo wengine. Hali ikiwa hivyo, maeneo yaliyotegemea soko hili huenda yakalipoteza taratibu, na bila shaka kupoteza natija inayotokana na soko lenyewe.
Ili kudhibiti hali hii, itakuwa bora ikiwa viwanda vya kuchinjia mifugo na kupakia nyama vitajengwa katika maeneo haya ya ugatuzi. Hili litawawezesha wakazi kuuza nyama badala ya kuuza mifugo wazimawazima. Fauka ya haya, maeneo haya yatajikinga dhidi ya kupoteza bidhaa zinazotokana na mifugo. Hizi ni kama vile ngozi, kwato na pembe ambazo bila shaka zina natija kuu. Ngozi kwa mfano, ni bidhaa muhimu sana katika sekta ya utengenezaji wa mavazi na mifuko. Viwanda vinavyotumia ngozi kama malighafi vikijengwa katika maeneo haya, wakazi wake watanufaika si haba. Mathalani, viwanda vya kutengenezea viatu, mishipi, mifuko na nguo vikianzishwa, wawekezaji watalazimika kuanzisha viwanda vingine vitegemezi. Kadhalika, ni dhahiri kwamba bidhaa zinazotokana na ngozi huhitaji kutiwa nakshi, Kuanzishwa kwa viwanda hivi basi kutazua haja ya kuanzishwa kwa viwanda vya kutengenezea rangi, pamoja na maduka ya kuuza bidhaa yenyewe. Isitoshe, gundi ya kugandisha bidhaa hizl itahitajika, hivyo kusababisha haja ya kuanzishwa kwa kiwanda cha gundi. Matokeo ya shughuli hizi zote ni kuzalishwa kwa nafasi anuwai za kazi kwa wakazi. Hili litakuwa na matokeo zaidi chanya, hususan kwa vijana. Badala ya kushiriki uievi na burudani zinazowahatarisha, wataweza kujitafutia riziki katika viwanda hivi.

Juu ya hayo, mfumo wa ugatuzi utayawezesha maeneo husika kuongezea thamani utoaji wa huduma za kijamii na kiutawala kulingana na mahitaji ya maeneo haya. Ni muhimu hata hivyo kuzingatia kwamba kila eneo la ugatuzi lina upekee wake, navyo vipaumbele hutofautiana kulingana na maeneo. Kuna yale ambayo yatasisitiza usalama, mengine ujenzi na uimarishaji wa miundomsingi kama vile barabara, vituo vya afya na hata taasisi za elimu. La muhimu ni wakazi wa maeneo husika kubainisha ni lipi litatekelezwa kwanza.

Kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Kufanikiwa kwa mfumo wa ugatuzi kutategemea juhudi za kila mkazi wa eneo husika. Ni muhimu kila mkazi kujiona kuwa mmiliki wa eneo zima la ugatuzi na kuwajibika katika kuliendeleza kwa hali na mali. Uwajibikaji huu unajumuisha uteuzi wa viongozi wenye muono mzuri na ambao watawawezesha kuyankia malengo yao ya kimaendeleo. Hakika, mustakabali na uwepo wa eneo la ugatuzi utakuwa zao la maamuzi ya wanaeneo. Vilevile ufanisi wa maeneo ya ugatuzi utakuwa msingi wa ufanisi wa taifa kwa jumla.

(a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 85-90.

(alama 8, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

(b) Kwa kutumia maneno 75-80, bainisha masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama 7,1 ya mtiririko)

**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

3 MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)

(a) (i) Eleza maana ya sauti mwambatano. (alama2)

(ii) Andika sauti mwambatano inayotarnkiwa kwenye ufizi. (alama 1)

(b) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa kielezi.
Komu ameshona nguo <u>nzuri</u> na kuiuza sokoni. (alama 1)

(c) Tunga sentensi mojamoja kubainisha: (alama 4)

i) kihusishi cha wakati

(ii) kivumishi cha pekee chenye maana, "bila kubagua".

(d) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi.
Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama. (alama 2)

(e) Bainisha mofimu katika neno:
atamnywea (alama 3)

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo:
Madebe hayo yatasafirishwa pamoja na nyundo hizi. (alama 2)

(g) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo:
Ingawa mshahara wake si mkubwa anaikimu familia yake. (alama 2)

(h) Tunga sentensi **tatu** kuonyesha matumizi **matatu** tofauti ya kiambishi 'Ii'. (alama 3)

(i) (i) Eleza maana ya sentensi ya masharti. (alama 1)

(ii) Tunga sentensi ya masharti. (alama 2)

j) Tumia kiwakilishi cha 'a' unganifu katika sentensi kuonyesha:
(i) umilikaji (alama 2)

(ii) nafasi katika orodha au nafasi katika kundi (alama 2)

(k) Tunga sentensi yenye kikundi tenzi chenye muundo ufuatao:
Kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, nomino (alama 2)

(1) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi **mawili** tofauti ya kistari kirefu.
alama 2)

(m) Unganisha sentensi zifuatazo kuwa sentensi moja bila kurudia kitenzi.
Osore amempigia Ngungui simu. Ngungui amempigia Osore simu. (alama 2)

n) Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha vitenzi vilivyomo kuwa nomino:
Mayaka anapotumbuiza huchekesha sana. (alama 2)

(o) Andika maana **tatu** za neno: kanda. (alama 3)

(p) Andika visawe **viwili** vya nahau: enda kombo. (alama 2)

**ISIMUJAMII:** (Alama 10)
*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*
Haya ng'ara ... Ng'ara leo! Nguo motomoto. Ng'ara leo kwa bei rahisi. Hamsini hamsini shati. Kuona ni bure. Bure kwa bure. Shika mwenyewe ujionee. Bei nafuu. Bei ya starehe. Haya haya. Usikose mwanangu! Hamsa! *Fifty!* Hamsa! *Fifty!* Hamsa na nyingine.

(a) Bainisha sajili ya mazungumzo haya. (alama 2)

(b) Eleza sifa **nane** za sajili hii kwa kurejelea kifungu hiki. (alama 8)

## KARATASI YA TATU

### SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1. Lazima**

(a) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya vitanza ndimi. (alama 2)

(b) Fafanua majukumu **sita** ya vitanza ndimi katika jamii. (alama 6)

(c) Eleza mbinu **sita** unazoweza kutumia katika kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi. (alama 12)

### SEHEMU B: RIWAYA

**Said A. Mohamed:** *Utengano*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2. "Walifanya kazi, walimenyeka.
Lakini walilala na njaa ...
Njaa, ndiyo ilikuwa misumeno
Iliyokeketa matumbo yao. ..."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha tamathali **mbili** za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Kwa kurejelea riwaya. Onyesha jinsi wanyonge walivyomenyeka. (alama 12)

3. Jadili uhusiano uliopo kati ya wahusika na maudhui kwa kurejelea wahusika wafuatao:

(a) Shoka (alama 10)

(b) Kazija (alama 10)

### SEHEMU C: TAMTHILIA T. Arege: *Mstahiki Meya*

*Jibu swali la 4 an la 5.*

4. Jadili mchango wa Wanacheneo katika kuivunja jamii yao. (alama 20)

5 "Ndiyo hivyo bwana. Elimu yetu hapa ni ya kawaida mno. Haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali."

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

(b) Bainisha tamathali ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili ukirejelea msemaji wa kauli hii. (alama 2)

(c) Kwa kurejelea tamthilia, fafanua mifano mingine **saba** ya matumizi ya tamathali uliyotaja katika (b) hapo juu. (alama 14)

### SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au la 7.*

*6.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Sinongi aushi yangu, hii leo, kwa ukungu wa ujana,
Nikaiga rika langu, kwa vileo na mbio za wasichana,
Kiwa ni riziki yangu, mapokeo, kuoa na kuona,
Ni wakati utanena.

Nashukuru kwa ugumba, wenye ndimi, wanipagazao nao,
Wapitao wakiimba, eti mimi, ningapenda hali zao,
Haupandiki mgomba, wana nyemi, fisadi wa hadhi zao,
Eti ni kwa raha zao.

Ni lipi lenye kukera, kwa Muumbi, marufuku kwenye misa,
Ni mtu kuwa hawara, wa vitimbi, ama alozawa tasa?
Ugumba na ukapera, sio dhambi, wala haujawa kosa,
Waama sina makosa.

Bora tungeni vitabu, magazeti, mutangaze kwa rediyo,
Muwaite watribu, kina Siti, watuzwa ilimu hiyo,
Na zaidi muhutubu, kwa umati, muwambe ambayo siyo
Kwalo sichafuki moyo.

Hidhuru yote ni bure, sio kitu, kudhiki asodhikika,
Siwi nikaona ghere, lailatu, nyota njema itafika,
Kwa shangwe na njerejere kila mtu, mdomo utarumuka,
Akiri amejibika.

**(Mwalaa M. Nyanje)**

(a) Eleza jambo ambalo mzungumzaji (nafsineni) katika shairi hili anasingiziwa. (alama 2)

(b) Fafanua mambo **matano** ambayo mzungumzaji (nafsineni) anapinga katika shairi hili. (alama 5)

(c) Eleza umuhimu wa viishio vya beti za shairi hili. (alama 2)

(d) Andika ubeti wa **tatu** kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(e) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 5)

(f) Bainisha matumizi **mawili** ya tasfida katika shairi hili. (alama 2)

**7.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

1. Huno wakati mufti, vijana nawausia.
Msije juta laiti. mkamba sikuwambia.
Si hayati si mamati. vijana hino dunia.
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

2. Japo aula kushufu,na machoni vyavutia.
Dunia wana dhaifu, yaugua nisikia.
Vijana nawasarifu, falau mkisikia,
Ukiona vyang'aria, tahadhari vitakula.

3. Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria.
Msije andama baa, makaa kujipalia.
Jepusheni na zinaa. madhara kukadiria.
Uonapo vyang'aria. tahadhari vitakula.

4. Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia,
Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia.
Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia,
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

5. Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita ja umeme, leo yao sitoria,
Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia,
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

6. Nambie faida gani, nambie ipi fidia?
Upatayo hatimani, waja wakikufukia,
Ila kufa kama nyani, kasoro yako mkia,
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

7. Kikiki ikaze karaba, u kijana vumilia,
Ujifanye kama kwamba, u jiwe huna hisia,
Wakwambe watalokwamba, kwa lolotevumilia.
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

8 Vyatiririka tiriri, vina vyanikubalia,
Alo bora mshairi, pa tamu humalizia,
Nahitimisha shairi, dua ninawapigia,
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

l9. Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia,
Wakingie wanarika, na anasa za dunia,
Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia,
Uonapo 'vyang'aria. tahadhari vitakula.

**(Mwalaa M. Nyanje)**

(a) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 4)

(b) Fafanua kwa kutoa mifano. mbinu **nne** alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 8)

(c) Nafsineni (mzungumzaji) katika shairi hili inasema na pande mbili. Zieleze pande hizo. (alama 2)

(d) Eleza umuhimu wa maswali ya balagha katika shairi hili. (alama 3)

(e) Bainisha toni ya shairi hili. (alama 3)

**SEHEMU E: HADITHI FUPI**

**K Walibora na S. A. Mohamed:** *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

"Kikaza" **(Robert Oduori)**

8. 'Wakaacha chungu kinatokota - bila kuivisha chakula'. Kwa hakika walijibu. "Ndio mtindo, na sisi tulifuata mitindo."

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Onyesha jinsi Wanatekede wanavyofuata mitindo na kuacha chungu kinaiokota bila kuivisha chakula.

## 3.2 KISWAHILI (102)

### 3.2.1 Kiswahili Paper 1 (102/1)

**1 Lazima**

Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa kuchunguza vyanzo vya ongezeko la visa vya wanafunzi katika eneo la Telekeza kuacha shule kabla ya kukamilisha masomo yao. Andika ripoti ya uchunguzi huo.

2 Andika insha kuhusu umuhimu wa tamasha za muziki katika maisha ya vijana.

3 Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

Usipoziba ufa utajenga ukuta.

4 Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:

Nilimtazama kwa muda. Macho yake yalijaa machozi ya furaha na majonzi...

### 3.2.2 Kiswahili Paper 2 (102/2)

**1 UFAHAMU**: (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Siku moja nilifika kumwona babu yangu kule kwetu kijijini bila kumtolea taarifa mbele. Nilipofika nilimkuta amevaa magwanda yake yaliyokula chumvi hadi yakakinai. Alinitazama huku akitabasamu akisema, "Tabia hii ya kuja kwako bila taarifa utaikoma. Ukiendelea hivi utakuja **kwenda kwa wakwe wako upate ndio wanakwenda uchi**."

Kauli hii ya babu ilinifanya kucheka. Tulisalimiana huku tunapigana pambaja. Harufu ya manukato niliyojirashia asubuhi hiyo ilikutana na kuchanganyika na harufu ya jasho lake. Baadaye tuliingia ndani, tukaketi kwenye makochi yaliyokuwa yameanza kuonyesha dalili za kuchoka. Baada ya kuulizana habari za kimsingi nilitaka kujua alipokuwa nyanya.

"Nyanyako ameenda kumwona jirani yetu mgonjwa. Amepata ajali akitoka mjini alikokuwa ameenda kuwatembelea wajukuu wake. Raha yote ya kuwaona iligeuka karaha." Alinyamaza kidogo, akaguna, kisha akaendelea, "Barabara hizi, sijui mwaziita 'haibei', zimewala watu wetu. Huwezi kuwahesabia vidole tena."

Kwa muda nilikosa la kusema. Niliona niubadili mkondo wa mazungumzo. Nilianza kwa kumweleza kuwa mazingira ya kijijini yalipendeza. Kwa kweli mandhari yale ya kijani kote hadi upeo wa macho yalinisisimua sana. Sauti za ndege zilikuwa mfano wa muziki wa chini uliochezwa ili kuyapamba mazungumzo yetu. Mara mojamoja nilitekwa na sarakasi ya jogoo aliyetanua mabawa yake na kukaribia kuzungumza, utadhani ni sauti ya mwanadamu. Nilipokuwa ninamtazama yule jogoo, nilishtukia mkono wa babu ukiushika wangu, akaniongoza nje akisema, "Haina haja kuyamezameza mate. Huyu jogoo ni wako. Leo tutamfanya kitoweo kwa ajili yako. Najua kule mjini mnakula kuku wa miigizo tu. Faida yao kwa mwili ni duni."

Tulishirikiana kumkamata yule jogoo lakini baada ya muda nilichoka. Moyo wangu ulikuwa unapiga kwa nguvu ajabu. **Niliona kisunzi**, nikakaa. Nikiwa ninajipumzisha chini ya kivuli cha mpera nilisikia sauti za watoto waliokuwa wamejiunga na babu kumkamata yule jogoo.

Tukiwa tunasubiri chakula cha mchana, niliona hii kuwa fursa mufti kumweleza babu kwamba nilifika kusudi niende naye mjini. Nilipolitamka tu hili alicheka sana. Aliniambia, "Mji ni wenu nyinyi. Sisi watu wa shamba raha yetu ni kufukuzana na kazi hizi za sulubu. Kwenda kukaa mjini na nguvu zote hizi faida yake nini? Nasikia siku hizi huko mjini kuna misongamano ya magari isiyoisha. Kuna haja gani kwenda kushinda kwenye gari kuharibu muda wako kwa sababu ya msongamano? Mimi hapa kwangu nikitaka kwenda kuzitekeleza shughuli zangu sipati kizuizi. Ninakwenda tu."

"Sikiliza babu," nilimwambia, "mji una raha yake. Wingi wa magari ni ishara ya maendeleo. Uwezo wa kifedha wa watu uko juu kuliko wa hapa kijijini. Leo hii mtu akipatwa na dharura ya ugonjwa hapa, kijiji kitafanya takilifu kumfikisha hospitalini. Mjini usafiri upo kila mahali wakati wowote."

"Kule mjini mnadai kuona mwanga na kuujua ustaarabu ila mmenoa," alisema babu, "maisha yenu, afadhali ndege warukao angani. Ni kama mnachupa kutoka upande mmoja hadi mwingine, kana kwamba mnaendeshwa kwa nguvu za mtambo usioonekana. Jamaa hawajuani tena. Mizizi yenu hamuitambui. Mmekuwa mithili ya miti inayopendeza lakini isiyo na mizizi ya kutosha. Upepo hafifu uvumapo inalemewa na kujibwaga chini. Je, huo ndio ustaarabu? Ustaarabu kwetu sisi watu wa hapa kijijini ni mtu kuwaamkua wenzake kila kukicha. Ni kujuliana hali. Ni kuombana kibaba cha unga au kibakuli cha mboga. Tunaishi tukijuana, si majina na sura tu, bali pia hata upishi wetu. Nyinyi mnaishi pasi na kujua majirani wenu. Je, wewe hukuona hata kuku wangu hawa wanatangamana?"

Swali hili lilipoachiliwa nilihisi kama aliyetwikwa nanga. Kijasho chembamba kilinitoka. Kwa bahati nzuri meza ilikuwa imeisha kuandaliwa; kipindi cha kupambana mezani kikawadia. Nilipokuwa nikila nilitambua kitu kimoja; yule kuku alikuwa na ladha ya kupendeza, tofauti na tuliozoea kuwala kule mjini. Ila nililoliona tu ni kuwa alikuwa mgumu kidogo. Nilipokuwa nikilifikiria hili niliisikia sauti ya babu tena.

"Chunga asikung'oe meno. Huyu ni kuku hasa. Atakusaidia kuimarisha meno. Hutakuwa na haja ya kwenda kumwona daktari wa meno. Sisi hapa hata kushiriki chakula kunatukumbusha kuwa kila shughuli ni kazi tosha. Hatuna muda wa kulaza damu." Alichukua bilauri ya maji, akapiga tama, kisha akaendelea kuinyofoa sima yake ya bada.

(a) Huku ukirejelea kifungu, fafanua faida **sita** utakazopata ukiishi shamba. (alama 6)

(b) Eleza mtazamo wa wahusika wafuatao kuhusu mji:

(i) msimulizi (alama 3)

(ii) babu (alama 4)

(c) Andika maana ya fungu lifuatalo la maneno kwa mujibu wa taarifa: (alama 1)

kwenda kwa wakwe wako upate ndio wanakwenda uchi

(d) Andika kisawe cha: (alama 1)

Niliona kisunzi

**2 UFUPISHO:** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Katika ulimwengu huu tunaoishi wenye hekaheka nyingi, mwanadamu anaendeshwa na maisha mfano wa gurudumu la gari. Kwa watu wenye kufanya kazi katika mazingira ya ofisi ambapo wanaketi mchana kutwa, mazoezi ni muhimu sana. Baadhi ya watu huona fahari wapigapo tai na kuelekea au kutoka kazini kwa gari. Tabia hii ya mwanadamu inamsahaulisha kuwa mwili wake ulidhamiriwa kufanya mazoezi ya viungo kwa kutembea au kufanya kazi zenye kuhitaji misuli kupashwa moto. Watu wengi hawana habari kuwa mazoezi yana faida tele kwao.

Wataalamu wa sayansi wamebainisha kuwa watu wanaoidhiki miili yao kwa mazoezi ya mara kwa mara huishi zaidi kuliko wasiofanya mazoezi. Watu hawa huwa wamo katika hali nzuri ya afya na wenye nguvu kuliko wale ambao hawaishughulishi miili yao kwa mazoezi au kazi zinazohitaji utumiaji nguvu.

Ni dhahiri kwamba mazoezi huchochea kuundwa kwa seli mpya za ubongo. Utafiti wa kisayansi umebainisha kuwa sehemu za ubongo zenye kusisimuliwa kwa mazoezi ndizo hutekeleza jukumu la kukumbuka na kujifunza. Bila mazoezi sehemu hizi zitashindwa kukumbuka au kujifunza maarifa mapya. Vile vile, imethibitishwa kwamba watu wanaoshiriki shughuli zenye kuwahitaji kutumia nguvu hutia fora katika mambo yanayowahitaji kukumbuka, kufanya maamuzi, pamoja na kusuluhisha matatizo.

Hali kadhalika, mazoezi huimarisha siha ya binadamu. Mathalani, matatizo ya moyo yanaweza kukabiliwa kwa kufanya mazoezi ya viungo. Kufanya mazoezi mara kwa mara huufanya moyo kuwa imara na kuuwezesha kutekeleza jukumu lake ipasavyo. Ifahamike kwamba moyo wenye siha huweza kupiga kiasi kikubwa cha damu bila ya juhudi kubwa. Hili bila shaka litamkinga binadamu dhidi ya kulemewa na kazi.

Isitoshe, kushiriki mazoezi au shughuli zenye kutumia nguvu mara kwa mara huuweka mwili katika hali nzuri ya kupambana na magonjwa. Utafiti wa kisayansi umeonyesha kuwa shughuli kiasi zinazomhitaji mtu kutumia nguvu, pamoja na upunguzaji wa uzito, na uzingatiaji wa lishe bora, huweza kupunguza uwezekano wa kupata ugonjwa wa kisukari kwa baina ya asilimia 50 na 60. Mazoezi hayapunguzi tu shinikizo la damu, bali pia hatari ya kupata kiharusi. Aidha, kufanya mazoezi mara kwa mara husaidia kudhibiti uzani wa mwili. Mtu anapokula kiasi cha chakula kinachozidi mahitaji yake ya kimwili huweza kujinenepea na kushindwa kutekeleza majukumu ya kimsingi. Mazoezi husaidia kuzichoma kalori zisizohitajika mwilini. Hatua hii, licha ya kusaidia kupunguza uzani, huvisisimua viungo vya mwili. Matokeo ya haya ni utendakazi wa hali ya juu bila kuchoka. Vilevile mwili unaofanya mazoezi haudorori. Umbo la mtu anayefanya mazoezi hupendeza.

Juu ya hayo, kufanya mazoezi mara kwa mara husaidia kujenga misuli yenye nguvu. Misuli inapokuwa na nguvu tunaweza kulifanya jambo kwa muda mrefu bila kuchoka. Mbali

na misuli kuimarika, mazoezi na shughuli zinazohitaji utumiaji nguvu husukuma hewa na virutubisho kwenye viungo mahususi vya mwili na kuvisaidia kufanya kazi vyema zaidi.

Hali kadhalika, mazoezi husaidia kujenga mifupa. Kadiri binadamu anavyoshiriki katika shughuli kama vile kuruka, ndivyo anavyoiimarisha mifupa yake. Shughuli ya aina hii huipa mifupa uzito ambao unaiwezesha kukua na kujengeka ikiwa na nguvu. Mazoezi pia hukawiza kudhoofika kwa mifupa.

Kunyooshanyoosha viungo nako huchangia kuufanya mwili kuwa imara na wenye kunyumbuka. Hali hii ya mwili hupunguza uwezekano wa kupata majeraha. Mwili usionyumbuka humfanya mtu ashindwe kutekeleza hata shughuli nyepesi zinazomhitaji kutumia nguvu. Si ibra kupata kwamba kuitekeleza shughuli ndogo tu humfanya mtu kupata maumivu.

Utulivu wa akili nao huweza kupatikana kwa kufanya mazoezi. Imebainishwa kwamba kufanya mazoezi kwa angalau dakika thelathini kwa muda wa baina ya siku tatu na tano kwa wiki hupunguza kwa kiasi kikubwa, dalili za unyong'onyevu. Na je, wajua kwamba kufanya mazoezi husaidia kupata usingizi? Mazoezi ni mfano wa bembea inayokutuliza na kukupa usingizi.

Mke ni nguo, mgomba kupaliliwa. Nao mwili wa binadamu, kama mgomba, unahitaji kushirikishwa katika mazoezi ili kuuwezesha kuwa na hamu ya kutenda kazi.

(a) Kwa kurejelea aya **tano** za kwanza, eleza matatizo ya kiafya yanayoweza kupatikana kwa kutofanya mazoezi. (maneno 100) (alama 9, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Nakala Safi

(b) Fupisha ujumbe wa aya **tano** za mwisho kwa maneno 80. (alama 6, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Nakala Safi

## 3 MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)

(a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) nazali ya kaakaa laini ..........

(ii) kikwamizo ghuna cha mdomo na meno ..........

(iii) irabu ya nyuma, wastani ..........

(iv) kiyeyusho cha kaakaa gumu ..........

(b) Bainisha silabi katika neno: wanyweshavyo. (alama 1)

(c) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kubadilisha nomino zilizopigiwa mstari kuwa vitenzi.

Wafanyakazi wote watafanyiwa <u>tathmini</u> ili kupata <u>suluhu</u> ya matatizo hayo. (alama 2)

(d) Andika sentensi ifuatayo katika umoja.

Mkihifadhi nafaka hizo vizuri maeneo haya yatakuwa na vyakula vya kutosha. (alama 2)

(e) Andika neno **moja** lenye mofimu zifuatazo: (alama 2)

nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita, yambwa, mzizi, kauli tendesha, kauli tenda

(f) Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno: kama (alama 2)

(i) kiunganishi

(ii) kihusishi

(g) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kivumishi. (alama 2)

(h) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.

Nyumba hizo zilijengwa mbali na mji ule. (alama 1)

(i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)

nomino ya jamii, kirai kihusishi, kitenzi kishirikishi, kielezi cha mahali

(j) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. (alama 1)

Chakula kinachozalishwa kwa njia za kiasili kina viinilishe vingi.

Anza kwa: Viinilishe vingi

(k) Tumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigiwa mstari.

<u>Mtalii</u> atazuru <u>mbuga</u>. (alama 1)

(l) Akifisha sentensi ifuatayo:

basi mwanangu akasema daudi hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia vision 2030 wewe waonaje (alama 3)

(m) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi cha wakati.

Beti alijishindia tuzo. Beti alishiriki katika utunzaji wa mazingira. (alama 1)

(n) Tumia 'kwa' katika sentensi kuonyesha: (alama 2)

(i) sababu

(ii) pamoja na

(o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi.

Mvua ilinyesha tulipokuwa tukilima. (alama 3)

(p) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa.

Malik alipuliza siwa akiwa kwa Shaka. (alama 2)

(q) Onyesha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo:

Mumbi alitia embe kapuni likaiva. (alama 1)

(r) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea.

Mmomonyoko wa udongo ulipozuiliwa mashamba yalinawiri. (alama 2)

(s) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **vito** na **fito**. (alama 2)

(t) Methali: Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi, huambiwa mtu anayezidharau shida za wengine. Mtu asiyetambua kuwa kuna wengine wanaoweza kulimudu jambo kuliko yeye huambiwa methali gani? (alama 1)

(u) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

Mwenyewe alikipenda kwa dhati.

(v) Tunatumia kihisishi "makiwa" tunapotaka kumtuliza aliyefiwa, na .............................. tunapotaka mtu atupishe. (alama 1)

(w) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba tendo lilifanikiwa kwa sababu ya kufanikiwa kwa tendo lingine. (alama 1)

(x) Andika nahau inayojumuisha ujumbe ufuatao: (alama 1)

kumzuia mtu kupata kitu japo huna haja nacho

(y) Shumbi ni kwa udongo, ............................ kwa chumvi, na ........................ kwa mtama. (alama 1)

4 **ISIMUJAMII:** (Alama 10)

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Mtu I: Wewe njoo hapa! (*Kwa sauti kubwa.*) Fanya upesi!

Mtu II: (*Anakimbia mbio.*) Naja *Sir*.

Mtu I: (*Anamtazama.*) Unajifanya mwerevu?

Mtu II: Hapana *Sir* ... eh ... afande.

Mtu I: Jina?

Mtu II: Samwel Kibao

Mtu I: (*Huku anaandika.*) Lete kitambulisho.

Mtu II: Sina hapa *Sir*.

Mtu I: Huna kitambulisho? Utafanyiwa *booking* vipi?

Mtu II: Naomba ...

Mtu I: Naomba! Naomba! Unaomba nini? Wazururaji kama nyinyi tunawajua. Mnajidai hamjui kuna *curfew*. Mnajiponza wenyewe na kuwahasiri wenzenu. Kisha, "Serikali saidia". Usiniharibie muda wangu. (*Akiashiria.*) Ingia ndani! Utakuwa mgeni wetu leo. Tutakukirimu chakula na chumba. (*Anamsukuma ndani.*)

(a) Bainisha sajili ya makala haya. (alama 2)

(b) Eleza sifa **nane** za sajili hii kwa kurejelea makala haya. (alama 8)

## 3.2.3 Kiswahili Paper 3 (102/3)

### SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI

1 **Lazima**

(a) *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

Hadithi ya Jabari inasimuliwa na jamii nyingi. Jabari alizaliwa kashika mkuki mkononi. Mawio ambayo kilio chake, ambacho kwa kweli kilikuwa mngurumo, kilipopasua anga, nyota kubwa ilianguka kutoka mbinguni. Ulimwengu mzima ulitetemeka na kutwaa giza.

Hata kabla mama mtu hajampa ziwa, Jabari alikuwa amevuvumuka na kuwa ghulamu wa miraba minne. Haikuchukua muda, hata vita kati ya jamii ya Sule na Suna vikaanza; kikosi cha Sule cha wapiganaji mia moja kikawajia vijana wa Suna kwa sime na nyuta. Jabari aliwakabili kwa konde moja pekee, akakirambisha dongo kita kizima.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 1)

(ii) Toa sababu **mbili** kuthibitisha jibu lako la (i) hapa juu. (alama 1)

(iii) Eleza manufaa **sita** ambayo jamii itapata kwa kukirithisha kipera hiki kwa vizazi vijavyo. (alama 6)

(b) *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

Ndimi Mwimo mdumishaji ukoo
Ndimi ndovu mtetemesha ardhi
Aliyepigana vita, ukoo kuauni
Ziliporindima zangu nyayo
adui alinywea, mafahali na mitamba akatukabidhi
Kwenye misitu sikuwa na kifani
Paa na hata visungura
vilijikabidhi kwangu
kwa kuinusa tu mata
Nani aliyewahi
ngomani kunipiku?
Makoo hawakunisifu, wakalilia nikaha?
Kwenye nyanja za michuano
nani angethubutu, ndaro kunipigia?
Sikuwabwaga chini, kwa yangu maozi, hata kabla hatujavaana?

(i) Andika aina ya sifo hii. (alama 1)

(ii) Bainisha shughuli **mbili** za kiuchumi na **mbili** za kijamii zinazoendelezwa na jamii inayosawiriwa na utungo huu. (alama 2)

(iii) Eleza mambo **matano** ambayo yanaweza kuzingatiwa ili kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama 5)

(c) Eleza faida **nne** za matumizi ya nyimbo katika uwasilishaji wa ngano. (alama 4)

## SEHEMU B: RIWAYA

**K. Walibora:** *Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2 "Moyo ulimpapa na kijasho chembamba kumtekenya juu ya mwanzi wa pua. Akahisi uchungu wa mwiba wa kujidunga."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Huku ukirejelea riwaya hii, fafanua kwa kutoa hoja **nane**, namna anayelengwa na kauli hii alivyojidunga miiba. (alama 16)

3 (a) "Imani ni kielelezo cha vijana waliowajibika." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea mifano **kumi** kutoka *Kidagaa Kimemwozea*. (alama 10)

(b) "Nadhani Mzungu pale alipo hana budi kutambua ukomavu wa Mwafrika katika kila sekta ya maisha."
Onyesha kinyume katika kauli iliyopigiwa mstari kwa kurejelea uongozi wa Tomoko. (alama 10)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**T. Arege:** *Mstahiki Meya*

*Jibu swali la 4 au la 5.*

4 "Kushindana naye ni kama kushindana na ndovu. Utapasuka."

(a) (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Bainisha tamathali **moja** ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(b) Kwa kurejelea hoja **saba**, thibitisha kwamba kushindana na anayerejelewa na kauli hii ni sawa na kushindana na ndovu. (alama 14)

5 "Wahenga wanasema dawa ya adui ni kummegea unachokula."

(a) (i) Andika suala linalodokezwa na kauli iliyopigiwa mstari. (alama 2)

(ii) Jadili hoja **nane** zinazoonyesha namna suala hili linavyozorotesha hali ya maisha Cheneo. (alama 8)

(b) Jadili jinsi vyombo vya usalama vilivyotumiwa kuuendeleza uongozi wa Cheneo. (alama 10)

## SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au la 7.*

6 *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu;
Na miti yote hujipinda migongo
kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea ha ha ha ha ha ha ...

Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani
katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho;
Kuna jambo gani linamridhisha?
Kama si kujua ni kutokujua
Laiti angalijua, laiti angalijua!

(T. Arege)

(a) Eleza hali ya mzungumziwa katika shairi hili. (alama 4)

(b) Huku ukitoa mifano, onyesha aina **mbili** za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(c) Fafanua aina **tatu** za taswira ukirejelea ubeti wa pili. (alama 3)

(d) Eleza umuhimu wa maswali ya balagha katika shairi hili. (alama 2)

(e) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili: (alama 3)

- (i) tashhisi
- (ii) kinaya
- (iii) tashbihi

(f) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

(g) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 1)

(h) Changanua muundo wa shairi hili. (alama 3)

7 *Soma Shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**T. Arege:** *Mwili*

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili.

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.

Vingekuwepo viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajuta, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili.

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili.

(a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 4)

(b) Fafanua mbinu **nne** za lugha zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 8)

(c) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

(d) Ni nani anayezungumziwa na nafsineni katika shairi hili? (alama 1)

(e) Eleza bahari ya shairi hili kwa kurejelea vipande. (alama 2)

(f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. (alama 3)

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

**K. Walibora na S. A. Mohamed (Wah) :** *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

"Mizizi na Matawi" **(A. Abdulla Ali)**

**8** (a) "Mwisho, naomba sote tusameheane kwa dhati."

(i) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(ii) Jadili umuhimu wa hotuba ya mzungumzaji katika hadithi hii. (alama 8)

(b) Onyesha jinsi hadithi, "Mke wangu" ilivyotumia kinaya kufanikisha ujumbe wake. (alama 8)

**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**
**Nov. 2016**
Muda: Saa 1¾

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**Kenya Certificate of Secondary Education**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**
Muda: Saa 1¾

## Maagizo

*(a)* *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima****.*
*(b)* *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
*(c)* *Kila insha isipungue maneno* ***400****.*
*(d)* *Kila insha ina alama 20.*
*(e)* *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(f)* *Insha zote* ***sharti*** *ziandikwe katika kijitabu cha majibu ulichopewa.*
*(g)* ***Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa.***
*(h)* ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

© 2016 The Kenya National Examinations Council

1 **Lazima**

Wewe ni katibu wa kamati inayochunguza jinsi ya kupambana na tatizo sugu la dawa za kulevya. Andika ripoti ukitoa mapendekezo ya kamati.

2 "Utalii una faida nyingi kuliko madhara nchini Kenya." Jadili.

3 Andika insha inayobainisha maana ya methali: Chombo cha kuzama hakina usukani.

4 Tunga kisa kitakachomalizika kwa:

"Niligugumia ile chupa ya maji kwa pupa. Sikuamini kuwa kiu yangu ingekatika. Baada ya kumaliza kunywa maji yote, ndipo nilipotambua kwa kweli kuwa maji ni uhai.

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

Jina ................................................................ Nambari ya Mtahiniwa ..................................

102/2
Karatasi ya 2
LUGHA
Nov. 2016
Muda: Saa 2½

Sahihi ya Mtahiniwa ........................................

Tarche ..............................................................

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**Kenya Certificate of Secondary Education**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**
Muda: Saa 2½

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(c) Jibu maswali yote.*
*(d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*(e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kweye kijitabu hiki.*
*(g) **Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.***
*(h) **Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

***Kwa matumizi ya mtahini pekee***

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **Jumla** | **80** | |

**1 UFAHAMU:** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Ulimwengu unatakiwa kuzua mbinu za kulitatua tatizo la ufukara ambao ni kikwazo kikuu cha juhudi za maendeleo. Ufukara unayakabili mataifa mengi yanayoendelea na **kuyatosa** kwenye shida nyingi huku mataifa ya magharibi yakizidi kupiga hatua kubwa za kimaendeleo. Tofauti iliyopo kati ya mataifa yanayoendelea na yaliyoendelea inaendelea kuongezeka kila siku.

Miongoni mwa sababu zinazochangia katika ufukara huu ni pamoja na ufisadi, uongozi mbaya, **turathi za kikoloni** na uchumi unaotegemea kilimo ambacho hutegemea mvua isiyoweza kutabirika. Vilevile, mataifa yanayoendelea yana idadi kubwa ya watu inayoupiku uwezo wa mataifa husika. Pamoja na haya, mataifa haya hayana uwezo wa kuwakomboa raia wake kutoka katika lindi la umaskini huu unaokithiri. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za kazi huchangia pia katika tatizo hili.

Ni wazi kuwa ufukara una athari hasi kote ulimwenguni. Aghalabu, ufukara huchipuza matendo mabaya. Ni rahisi kuwashawishi wananchi maskini kushiriki katika uhalifu ili kujinasua kutoka kwenye lindi la kimaskini. Udhaifu huu huweza kuzaa mbegu ya **kuatika** maovu ya kila aina ukiwemo ugaidi.

Mataifa yaliyoendelea yanatakiwa **kuyaburai** madeni yanayoyadai mataifa yanayaoendelea kama njia moja ya kupambana na ufukara. Mataifa haya maskini hutumia asilimia kubwa ya mapato ya kitaifa kuyalipia madeni haya. Hali hii imeyafanya mataifa haya kushindwa kujikwamua kutoka kwenye minyororo ya ufukara. Njia nyingine ya kuyasaidia mataifa haya ni kukubali kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi husika.

Mataifa yanayoendelea nayo yanatakiwa kuchukua hatua katika kuwanusuru raia wake kutoka kwenye dhiki hii. Ni sharti yaibuke na mikakati kabambe ya kupambana na ufukara. Itakuwa na faida kubwa iwapo mataifa haya yataunda sera zinazotambua ufukara kama tatizo kuu linalozikabili na kuweka mikakati ya kuwaokoa raia wake kutoka kwenye tatizo hili. Pamoja na mikakati hii ni kuzalisha nafasi za kazi, kuimarisha miundo msingi, kuendeleza elimu inayolenga kutatua matatizo maalumu katika jamii na kupanua viwanda. Kuna pia haja ya viongozi kuwa waangalifu ili mfumo wa soko huru ambao unaendelezwa na mataifa yaliyondelea usiishie kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia. Maamuzi yote ya sera za kiuchumi sharti yauzingatie uhalisia wa maisha ya raia wa mataifa haya.

(a) Eleza athari za madeni kwa nchi zinazoendelea. (alama 2)

(b) Kwa nini umaskini unatawala mataifa yanayoendelea? (alama 4)

(c) Mwandishi anatoa mapendekezo yapi kwa mataifa yanayoendelea katika kutatua tatizo la ufukakra? (alama 4)

(d) Mfumo wa siko huru una mathara gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)

(e) Taja visawe vya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)

(i) turathi za kikoloni

(ii) kuatika

(iii) kuyaburai

2 **MUHTASARI:** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Taifa huundwa na watu wanaoishi katika nchi moja na wanaojitambua kisiasa kama watu walio na mwelekeo, maono na hatima sawa. Utaifa hujengwa kwenye misingi ya mapenzi kwa nchi. Utambuzi wa cheo, eneo, hadhi, rangi na hata makabila wanakotoka raia wa taifa moja si chanzo cha kuwatanganisha.

Nchi moja huweza kuundwa na watu walio na tofauti chungu nzima zikiwemo tofauti za kikabila, kitabaka na kimawazo. Hata hivyo, watu hawa huwa na kitu mfano wa gundi kinachowaunganisha na kuwafanya kuonea fahari nchi yao. Watu hao huwa na falsafa na imani sawa kama taifa inayoashiriwa hasa na wimbo wa taifa. Hata hivyo haya yote hayawezi kuwafikia katika kiwango cha kuunda taifa.

Uzalendo ndio mhimili mkuu wa utaifa. Uzalendo ni mapenzi aliyo nayo mtu kwa nchi yake. Mapenzi haya humwongoza mtu katika mawazo yake, itikadi yake, matendo yake, matamanio yake na mkabala wake kuhusu nchi na hatima ya nchi yake. Mzalendo hawezi kushiriki katika matendo yanayoweza kuiletea nchi yake maangamizo kwa vyovyote vile.

Mzalendo huongozwa na mwenge wa wema. Mzalendo hawezi kushiriki kwenye shughuli zozote zinazohujumu mshikamano wa kitaifa. Yeye hatawaliwi na ubinafsi wa kutaka kufaidi nafsi yake na ya jamii yake finyu. Matendo yake yote huongozwa na ari ya kuiboresha nchi yake. Anayeipenda nchi yake hujiepusha na ulafi wa kujilimbikizia mali. Yuko radhi kuhasirika mradi taifa lake linufaike.

Utaifa ni mche aali unaopaliliwa kwa uzalendo, kuepuka uchu wa nafsi na taasubi hasi zikuwepo za kikabila na ubinafsi. Hali hii inapofikiwa, hatima ya taifa na mustakabali wa raia wake huwa wenye matumaini makubwa.

(a) Kwa maneno 40 – 50 dondoa sifa kuu za utaifa. (alama 6, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

Nakala safi

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

(b) Ni nini misingi ya kutathmini mzalendo? (maneno 60 – 70) (alama 9, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

Nakala safi

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

**3 MATUMIZI YA LUGHA:** (alama 40)

(a) Tumia nomino yoyote katika ngeli ya I – I kutunga sentensi. (alama 1)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(b) (i) Nini maana ya silabi. (alama 2)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(ii) Tunga neno lenye muundo huu wa silabi:
Irabu + konsonanti + konsonanti + irabu.

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(c) Tunga sentensi hii upya kwa kufuata maagizo:
Wasichana wanaingia darasani kwa haraka. (Andika kinyume chake). (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(d) Tambua kiambishi awali na tamati kati neno:
Alalaye (alama 2)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(e) Ainisha vivumishi katika sentensi hii.
Mzee mwenyewe ni mkongwe na amepewa zawadi kwa kuwa shamba lake lilitoa mazao mengi. (alama 4)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(f) Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama. (yakinisha sentensi hii) (alama 2)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(g) "Shughuli yetu itakamilika kesho", mama alimwambia mwanaye Juma (Andika katika usemi wa taarifa). (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(h) Changamua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi.
Mpira ulichezwa tulipokuwa tukipika. (alama 3)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(i) Dhihirisha matumizi matatu tofauti ya kimaana yatakayotokea kitenzi "ona" kikinyambuliwa katika kirai hiki "ona ndoto". (alama 3)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(j) Eleza matumizi ya hali za "ka" na "hu" katika sentensi zifuatazo:

(i) Balozi <u>hu</u>ja hapa kila mara. (alama 1)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(ii) Mpishi alipika, a<u>ka</u>pakuwa na a<u>ka</u>gawa chakula. (alama 1)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(k) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi:
Tuliitwa na baba. (alama 2)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(l) Akifisha:
Shangazi alimwambia mwanawe njoo nikupeleke kwenu jioni motto aliuliza kwetu wapi? (alama 4)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

(m) Eleza matumizi mawili ya kiambishi –ji- (alama 2)

(i) ..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(ii) ..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(n) Tunga sentensi hii upya kwa kutumia visawe vya maneno yaliyopigwa mstari. (alama 3)

Kiambaza kilimuumiza ghulamu alipokuwa akipanda.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(o) Tumia kitenzi "Fa" katika sentensi kuonyesha mazoea. (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(p) Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo:
Babu alifika mapema kuliko wote halafu akaondoka. (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(q) Tumia kitenzi "tafakari" kama nomino katika sentensi. (alama 1)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(r) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigwa mstari. Mwanamziki ataembelea mji. (alama 1)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

4 **ISIMUJAMII** (Alama 10)

Kwa kutoa mifano maridhawa, eleza kaida zozote tano ambazo matumizi ya lugha hutegemea katika jamii.

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

Name ........................................................................ **Index Number** ..................................................

**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**
**Nov. 2016**
Muda: Saa 2½

**Candidate's Signature** .......................................

**Date** .....................................................................

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**Kenya Certificate of Secondary Education**
KISWAHILI
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**
Muda: Saa 2½

**Maagizo**

*(a) Jibu maswali **manne** pekee.*
*(b) Swali la **kwanza** ni **lazima.***
*(c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
*(d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja.***
*(e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(f) Majibu yote **sharti** yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.*
***(g) Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapa.***
***(h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

*© 2016 The Kenya National Examinations Council*

## SEHEMU A: HADITHI FUPI

**K. Walibora** na **S. A. Mohamed:** *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

1. **Lazima**
Jadili maudhui ya elimu kwa mujibu wa "Kanda la Usufi", "Shaka ya Mambo" na "Tazama na Mauti". (Alama 20)

## SEHEMU B: RIWAYA

**K. Walibora:** *Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. Fafanua mjukumu ya elimu na dini katika jamii kwa mujibu wa riwaya: Kidagaa Kimemwozea. (Alama 20)

3. "Wasemao husema, atafutaye hachoki."

 (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

 (b) Kauli hii ina maana gani kwa mujibu wa muktadha huu. (Alama 2)

 (c) Jadili umuhimu wa kinachotafutwa katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (Alama 14)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**T. Arege:** *Mstahiki Meya*

*Jibu swali la 4 au la 5*

4. "Anwani Mstahiki Meya ni kinaya." Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia. (Alama 20)

5. "…dawa ya adui ni kummegea unachokula."

 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

 (b) Jadili jinsi dawa inayorejelewa inavyozorotesha hali katika mji wa Cheneo. (Alama 16)

## SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au la 7*

**6.** Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

**Kilio cha Lugha**

Ni wimbo najiimbia, nijiliwaze
Sina wa kusaidia, **nasongwa** sina nafasi
Kiwa kwetu naumia, kwengine si mahususi
Lugha ya mtu mweusi, Kiswahili chalilia.

Wataalamu ni nani, mulipo mwaninyanyasa
Hamna nami imani, wala kupanga siasa,
Mwasema sayansini, siku ningalitosa,
Mwanambia nikotosa, kuiva sijafika.

Ela muelewe sana, Maamuma na Imamu,
Mulipokuwa vijana, kwenu nilikuwa timamu,
Sasa mumesoma sana, mwaniona ni haramu,
Mujue kuwa dawamu, utumwa mwauridhia.

Mzaliwapo mwalia, 'maa', maneno ya kwanza,
Lugha munayokulia, ya mama zetu ya kwanza,
Wa lugha muwedoria, muweze na kuikuza,
Sio kujipendekeza, uzungu kuigiza.

Majira ya ukoloni, ukombozi kusambaza,
Lugha mulithamini, Kiswahili kufukiza,
Hata kule risavuni, kizungu hanikuwaza,
Sasa mbona mwanibeza, mbali mwanitupilia?

Sayansi sio asili, msamiatiwe sinao,
Sayansi yataka mbali, msamiati ni wa hao
Nitakuwa Kiswahili, kiomba majina yao
Lugha kujikuza kwao, huomba linalofaa.

Enyi viongozi wetu ipangeni nadharia,
Kujenga siasa yetu, tuzidi kuwa huria
Lugha hata 'mbusha watu, tuche **kuriaria**,
Sifa ni kwa chake mtu, cha mwenzi hutoringia.

Utajiri wangu hasa, nikiwatajia wote,
Msamiati huwa, ni wa Afrika yote,
Na methali za kuasa, nahau na ngeli zote,
Na nisemwapo popote, ujumbe hukamilika.

Afrika ndipo petu, pa wabantu halisi,
Baba na mama ni Bantu, shina la wangu ukwasi,
Warabu na wengi wetu, sio wangu **Adinasi**
Kwao 'meomba kiasi, ili kujizidisha.

Mfumo mpya hongera, wa elimu humu Kenya,
Lugha takuwa imara, ukabila tutafinya,
Kiswahili ni ibara, kila mtu kiimanya,
Methali imetuonya, mtumwa si mwasilia.

Tamati lugha yalia, yabaguliwa bayana,
Kukua imeridhia, msamiati kufana,
Wengine wataijulia, kwa marefu na mapana,
Lugha yenu ya maana, mwaipuuza yalia.

(a) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (Alama 2)

(b) Kwa kutoa hoja **nne**, eleza kwa nini shairi hili likaitwa kilio cha lugha. (Alama 4)

(c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

(d) Eleza toni ya shairi hili. (Alama 2)

(e) Tambua uhuru wa kishairi uliotumiwa kwa kurejelea mifano **mitatu**. (Alama 3)

(f) Bainisha nafsineni katika shairi. (Alama 2)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa shairi. (Alama 3)

- (i) nasongwa
- (ii) kuriaria
- (iii) adinasi

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

**T. Arege:** *Barabara*

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nituliza akili.

Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na **kuruba**
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
"Kuwa tayari kupanda na kushuka."

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima nifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka.

Jambo moja nakukumbukia: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendelee kijitahidi kwa kila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii **barabara yenye ukungu**
Nikinaswa na kujinasua
Yumkini nitafika mwisho wake
Ingawa wangu mwisho haitauwahi kabla.

(a) Eleza toni ya shairi hili. (Alama 2)

(b) Tambua nafsineni katika shairi hili. (Alama 2)

(c) Mshairi ana maana gani anaposema "Kuwa tayari kupanda na kushuka" katika ubeti wa **tatu**? (Alama 2)

(d) Fafanua tamathali **tano** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili ukizitolea mifano mwafaka. (Alama 10)

(e) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa **tano** wa shairi hili. (Alama 2)

(f) Eleza maana ya: (Alama 2)

(i) kuruba

(ii) barabara yenye ukungu

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8.** (a) Kwa kutumia mifano mwafaka eleza majukumu **matano** ya nyimbo katika jamii. (Alama 10)

(b) Ili kuweza kufanikisha uwasilishaji wa utanzu wa nyimbo kwa hadhira eleza mambo anayohitaji mwimbaji. (Alama 10)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

**Lazima**

Shirika la kigeni la Tugawane limeanzisha kiwanda cha kutengenezea matofali katika eneobunge lenu. Mwandikie barua Mhariri wa Gazeti la Mzalendo ukitoa maoni yako kuhusu faida na changamoto zinazoweza kutokana na mradi huu.

Andika insha kuhusu umuhimu wa mwanafunzi kujiunga na vyama mbalimbali shuleni.

Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
Papo kwa papo kamba hukata jiwe.

Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:
Sikuupa moyo wangu nafasi ya kujutia niliyoyatenda. Nilikuwa nimeamua kuyajenga maisha yangu upya.

NED

1. UFAHAMU: (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

"Asante baba, asante mama," akasema Bahati jioni moja baada ya chajio, "Sijui ilitokeaje kukawa na watu wanaothamini binadamu wenye mahitaji maalumu katika jamii hii. Sitawauliza mlichofanya kunikinga na hukumu ya ukoo ya kuniangamiza; hayo mtakuja kunihadithia siku moja. Ila nataka mjue kwamba kuishi na ulemavu wa aina yoyote ile kuna dhiki kuu. Niliyokabiliana nayo baada ya uamuzi wenu wa kunipeleka shuleni hayawezi kutoshea hata chapisho la kurasa elfu. Si kudhihakiwa na miale ya jua; ngozi yangu inashindwa kuuhimili ukali wake, si kutengwa na marika, si kulazimika kusoma hati za kawaida hadi pale serikali ilipoanzisha sera ya kuhakikisha kwamba matini zote za kiusomi zimeandikwa pia kwa hati ambazo zinaweza kusomwa na wenye changamoto kama yangu, si kubaguliwa kazini...." Bahati alitua, akawatazama wazazi wake kama anayetaka kuona taathira ya maneno yake kisha akaendalea.

"Msinione kama aliyekosa **hisani**, ila nataka niwaambie kwamba hata uamuzi wenu wa kunitafutia mlinzi kuandamana nami hadi shuleni ulinitia kwenye ngome zaidi. Nilijihisi kama niliyedhulumiwa zaidi katika kule kulindwa! Najua mlikuwa mnachelea kwamba ningekuwa windo rahisi kwa walanguzi wa binadamu ambao wanaamini kwamba viungo vyetu sisi ni dawa ya kutibia ndwele mbalimbali. Hata hivyo, katika kipindi chote hicho nilitamani kwamba mngenifunza mbinu za kujilinda mimi binafsi. Amini usiamini hata nilitamani kwamba ningetekwa nyara, nijadiliane na watesi wangu kuliko kupokwa nafasi ya kubuni mikakati ya kujihakikishia usalama".

"Mwanangu Bahati," alisema mume wangu, "binadamu hawi jagina kwa kuzifuata tamaduni za jamii yake bila kuzichunguza. Haidhuru kwamba ilichukua muda kuyang'amua haya. La muhimu ni kwamba umeweza kuishi kama ndugu zako".

Nilimtazama mume wangu kwa macho yaliyokuwa yamepofushwa na dimbwi la machozi. Moyo uliituma akili yangu kurudi nyuma kule -e-e-e- kwenye miereka ya baada ya kuzaliwa kwa Bahati. Asubuhi hiyo ya kipupwe nilishika ujia ulioelekea kwenye msitu uliokuwa karibu na boma la Mzee Kedi, baba mkwe wangu; mgongoni nimeifungia mbeleko ambayo ilikisitiri kitoto changu. Nilitazama nyuma, nikaiona nyumba ambayo mimi na mume wangu tulikuwa tumechanga bia kuijenga.

"Haya yote nayaacha," nilijiambia, "nayaacha na mengine mengi. Nawaacha mabinti wangu wawili, namwacha mume wangu, naiacha kazi yangu, nayaacha maisha yangu. Wala sijuti kwa kuyaacha haya yote. Sina cha kujutia kwani imebidi kuondoka. Jamii yangu imenitema; mimi na mwanangu. Haina nafasi ya mwanangu, kwa hivyo nami nimeamua kwamba haina nafasi yangu kwa vile imesema huu ni mzigo wangu. Ikiwa ukoo umeamua kuwa hatima ya mwanangu huyu ni kuwa kitoweo cha fisi, basi na tuwe sote karamu ya fisi," nilitamatisha kauli yangu kisha nikayarudisha nyuma tena mawazo yangu.

Nilikumbuka sauti ya muuguzi hospitalini siku ambayo nilijikopoa, "Pongezi Tamasha, Mungu amekutunukia kipusa". Nilikifunua kitoto changu kilichokuwa kimefunikwa gubigubi, nikakitazama viguu, vikono, uso...kisha, 'Mungu wangu!' ikanitoka.

"Dadangu, unastahili kumshukuru Mungu," akasema muuguzi, "wapo wanawake, mimi mwenyewe nikiwemo, ambao hawajawahi kuambulia ujauzito, sikwambii hata kupoteza mimba.

Huyu wako ni kiumbe kamili, kasoro yake i kwenye ngozi tu, na hii ni hali ambayo unaweza kukabiliana nayo. Hapa unionapo nimelazimika kumpa mume wangu talaka, mwenyewe alienda kortini akaiomba. Anadai kwamba hatusikilizani. Ila najua kiini cha haya yote ni kutoshika kizazi".

Nilimtazama huyo muuguzi kana kwamba hajasema lolote. Nilimwona kama anayeuona mzigo wangu kuwa kanda la usufi. Huenda huyu muuguzi hakujua kwamba katika jamii yangu watoto wa aina hii ni kama pacha, huaminiwa kuwa nuksi kwa ukoo mzima, kwa hivyo hutupwa. Muuguzi huyu hakujua pia kwamba tayari nilikuwa na watoto wawili wa kike na huo tayari ulikuwa mzigo mkubwa kwangu kwani ilibidi kumhakikishia mavyaa kila mara kwamba hawa pia walikuwa watoto.

Moyo ulinipa kukumbuka jitimai iliyojiandika usoni mwa mume wangu asubuhi hiyo alipokuja hospitalini. Alikitazama kitoto chetu kana kwamba anaona mzuka. Alinyamaza kwa muda, akashusha pumzi, kisha akanishika kwenye bega na kuondoka kwenye wodi. Machozi yalivunja kingo zake huko yanakohifadhiwa, nikalia kama mfiwa. Mume wangu alirudi tena baada ya siku mbili; anakuja kunipeleka nyumbani.

"Mke wangu, naomba msamaha kwa kutokuja kuwatazama kwa siku mbili. Ilibidi nishauriane na ukoo kuhusu tanzia hii. Inavyoonekana ni kwamba msimamo wa baba na wazee wengine ni ule ule. Wanasema ukoo wa Baulanga haujawahi kupata mtoto wa aina hii, kwamba kumhifadhi mwana huyu kutakuwa **kuupaka masizi** ukoo. Wahenga hawatakubali tendo hili. Sijui nitakutetea vipi. Nimo kwenye njia panda," mume wangu alikamlisha uzungumzi wake na kuelekea kwenye afisi ya mhasibu kukamilisha viviga vya kutuondoa hospitalini.

"Huna haja ya kunitetea. Sijafanya kosa lolote. Nililofanya ni kujaliwa kiumbe ambaye anaonekana kuwa punguani kwa misingi ya jamii yako. Nitakilinda kitoto hiki hata kifoni," nilimwambia mume wangu mawazoni.

(a) "Kufanikiwa kwa watu wenye mahitaji maalumu kunategemea jamii." Thibitisha kwa kutoa hoja **sita** kutoka aya **tatu** za kwanza. (alama 6)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(b) Kwa kurejelea aya ya **nne** hadi ya **saba**, onyesha jinsi unyanyasaji wa kijinsia unavyoendelezwa katika jamii hii. (alama 3)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(c) "Msimulizi anahimiza uwajibikaji." Thibitisha kwa kutoa hoja **nne** kutoka aya **tatu** za mwisho. (alama 4)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(d) (i) Andika kisawe cha, **'hisani'** kwa mujibu wa taarifa. (alama 1)

..............................................................................................................................

(ii) Eleza maana ya, **'kuupaka masizi'** kulingana na taarifa. (alama 1)

..............................................................................................................................

**2. UFUPISHO:** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Moja kati ya mambo ambayo yamerahisisha maisha ya binadamu ni maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia. Siku hizi shughuli nyingi ambazo zilichukua muda mrefu kutekelezwa zinachukua muda mfupi sana. Tuchukue kwa mfano shughuli za usafiri na utendaji kazi. Siku hizi zipo mashine ambazo zinafanya kazi kuwa nyepesi mno. Kwa mfano, katika ukulima, kuna mashine za kulima, kuvuna na hata kupura nafaka. Magari nayo yamerahisisha usafiri na upashanaji habari. Safari ambayo awali ilichukua siku mbili au tatu, siku hizi inachukua siku moja au hata saa chache tu kwa sababu ya kuwepo kwa magari ya kisasa.

Katika sekta ya elimu, maendeleo makubwa yameshuhudiwa. Siku hizi mwalimu anaweza kuhuisha somo lake kwa kutumia tarakilishi. Vipindi mbalimbali vimenaswa na kuhifahiwa kwenye kompyuta. Itokeapo kwamba mwalimu wa darasa atakosa kuhudhuria somo, wanafunzi wanaweza kufunzwa na mwalimu wa kompyuta. Shughuli za utafiti nazo zimefaidika mno kutokana na uvumbuzi wa kiteknolojia. Wasomi na wanafunzi wanaweza kupata matini mbalimbali za rejea kupitia kwenye mtandao. Hili linasaidia kufidia upungufu wa vitabu vya

kikaida. Hali kadhalika, maendeleo ya kiteknolojia yamerahisisha shughuli za usajili vyuoni na hata shuleni. Wanafunzi wanaweza kujisajili na hata kulipia kozi mbalimbali kupitia kwenye mtandao. Hali hii inaokoa muda ambao watahiniwa na wanaafunzi wangepanga foleni vyuoni, na hata katika taasisi zinazotoa mitihani, ili kujisajili. Kadhalika, teknolojia imesaidia katika kuhakikisha usalama wa alama za wanafunzi. Wataalamu wa teknolojia wameweza kuweka mikakati ambayo itahakikisha kwamba mabadiliko yoyote ya alama yanaweza kufuatiliwa kupitia kwenye mtandao.

Upande wa matibabu nao haujaachwa nyuma. Utafiti kuhusu tiba za kukabiliana na magonjwa sugu unafanywa kupitia kwenye mtandao wa intaneti. Pia, kuna mitambo ya kuchunguzia viini vya magonjwa mbalimbali na kutoa matokeo hapo hapo. Hali hii husaidia kumpa mgonjwa matibabu yafaayo wakati ufaao, hivyo kuokoa maisha yake. Madaktari pia wanaweza kufanya udodosi hapo hapo kwa kubofya tu tarakilishi.

Yumkini manufaa zaidi ya maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia yamepatikana kwenye uwanja wa biashara na uchumi kwa jumla. Ni dhahiri kwamba siku hizi ubadilishanaji wa bidhaa na huduma umekuwa rahisi mno. Kwa mfano, mfanyabiashara anaweza kuuza na kununua bidhaa zake kutoka nga'mbo akiwa hapo hapo kiwandani au afisini mwake. Hali hii imefanikishwa hata zaidi na uvumbuzi wa simutamba; kifaa kidogo lakini chenye akili kama ya bindamu. Kifaa hiki huwa na huduma ya intaneti ambayo humwezesha muuzaji kumtumia mnunuzi picha ya bidhaa aitakayo akiwa popote pale. Kifaa hiki pia ni muhimu katika kuendeleza huduma za benki. Je, unajua kwamba unaweza kutoa na kuhifadhi fedha kwenye akaunti yako kwa sekunde mbili au tatu ukiwa hapo hapo sebuleni mwako? Unajua pia unaweza hata kuomba na kupokea mkopo kupitia simu yako ya mkononi? Huduma hii ya simutamba pia humwezesha mtu kuwatumia pesa jamaa zake bila kulazimika kwenda benki au posta kuzituma. Mtu anaweza hata kuhifadhi laki moja kwenye simu na kuzituma pesa hizo kulingana na matilaba yake. Kadhalika mtu anaweza kulipia huduma kama vile za umeme, maji, matibabu na hata karo kupitia kifaa hicho hicho.

Ni dhahiri kwamba uvumbuzi wa kisayansi na kiteknolojia umeiletea jamii natija kubwa. Hata hivyo, hakuna mchele usiokuwa na ndume. Maendeleo haya yameandamana na changamoto anuwai. Kuwepo kwa mtandao wa intaneti kumewafanya baadhi ya wanajamii kutumia muda wao mwingi kwenye mtandao, mara nyingine kwa nia ya kujiburudisha tu au kuzungumza na marafiki. Hili linapalilia kuzorota kwa maadili ya kikazi. Aidha, kuna baadhi ya watu ambao wanatumia mtandao kuwatusi na kuwadhalilisha wengine kwa namna mbalimbali. Wengine huingilia uhuru wa kibinafsi wa wenzao kwa kuangaza mahusiano yao ya kimapenzi. Hali kadhalika, kuna wanajamii ambao hutumia mtandao kuwatisha wengine. Baadhi hutumia mtandao kuwatapeli wengine. Pengine hata wewe umewahi kupigiwa simu ukaambiwa umeshinda milioni moja, ukaanguka kwenye mtego huo, na baadaye hata ukapoteza kiasi fulani cha fedha ukifuata milioni ambayo haipo!

Uvumbuzi wa kiteknolojia umechangia kuendeleza wizi wa kitaaluma. Kuna wasomi katika ngazi mbalimbali ambao hunakili mawazo ya wataalamu moja kwa moja bila hata kutambua mchango wao kwenye marejeleo. Hii ni njia moja ya kudhoofisha fani yenyewe ya utafiti. Kadhalika, mtandao wa intaneti umetumiwa na watu waliopotoka kimaadili kupujua thamani ya mtihani. Baadhi ya watu huchukua sehemu ya mtihani au hata karatasi nzima ya mtihani wakaipiga picha na kuituma kwa wateja wao kupitia kwenye mitandao ya kijamii. Visa vya kigaidi navyo vinaendelezwa kwa ufanifu mkubwa kupitia kwenye mtandao wa intanenti na simu za mkononi. Njama nyingi za ulipuaji wa majengo zimepangwa kupitia simutamba. Vilevile, uvumbuzi wa kiteknolojia unatishia kuteteresha mshikamano wa kifamilia. Siku hizi mzazi anaweza kukaa kwa miezi miwili bila kuonana ana kwa ana na watoto wake, wanazungumza tu kupitia kwenye simu. Hili hutepua ule uhusiano wa kibinafsi kati ya jamaa, na mwishowe huweza kusababisha ukengeushi; watoto na wazazi wakajiona kuwa wageni kwa kila mmoja. Juu

ya hayo, huduma zinazopatikana kwenye mtandao zimewafanya vijana kuwa waraibu kiasi cha kutotenga wakati kuyadurusu masomo yao. Hili linawatia kiwewe wakati wa mtihani na yumkini ni mojawapo ya vyanzo vya udanganyifu katika mitihani.

Maendeleo ya kiteknolojia yamesaidia kuimarisha maisha ya binadamu katika nyanja zote za maisha. Binadamu wameweza hata kupata mafundisho ya kidini moja kwa moja kupitia kwenye simu zao za mkononi. Hata hivyo, binadamu ameweza pia kuhasirika kutokana na uvumbuzi huu. Mashine zimetwaa nafasi ya binadamu katika utendakazi, jambo ambalo linapalilia zaidi uhaba wa nafsi za kazi. Ni muhimu binadamu ajitahidi kutumia teknolojia kwa njia endelevu ili kujifaidi.

(a) Fupisha ujumbe wa aya **nne** za kwanza kwa maneno 90. (alama 8, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Nakala Safi**

NED

(b) Fafanua masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya **tatu** za mwisho. (maneno 70)
(alama 7, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Nakala Safi**

INED

**3. MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)

(a) Andika tofauti moja kati ya sauti zifuatazo: (alama 2)

(i) /ng'/na/gh//

..........................................................................................................................

(ii) /v/ na /f/

..........................................................................................................................

(iii) /r/ na /l/

..........................................................................................................................

(iv) /m/ na /n/

..........................................................................................................................

(b) Andika maneno yenye miundo ifuatayo: (alama 2)

(i) konsonanti, konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu

..........................................................................................................................

(ii) konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu

..........................................................................................................................

(c) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi **mawili** ya kiambishi : **o**. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(d) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo. (alama 2)

(i) Mhalifu <u>alisamehewa</u> kwa sababu <u>alinyenyekea</u>.
(Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino.)

..........................................................................................................................

(ii) Waigizaji wengine wameingia jukwaani.
(Tumia kivumishi cha idadi chenye kuonyesha nafasi katika orodha.)

..........................................................................................................................

(e) Tunga sentensi ukitumia kirai kihusishi kama kielezi. (alama 1)

..........................................................................................................................

(f) Unganisha sentensi zifuatazo kwa viunganishi mwafaka. (alama 2)

(i) Kheri aliweza kutujengea hospitali. Atajenga zahanati pia.

..........................................................................................................................

(ii) Zumari anasomea Uanasheria. Vilevile Maki anasomea Uanasheria.

..........................................................................................................................

(g) Onyesha miundo **miwili** ya nomino katika ngeli ya A – WA. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(h) Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyodhihirika. (alama 1)

..........................................................................................................................

(i) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 1)

Maseremala walilainisha mbao hizo wakatutengenezea meza.

..........................................................................................................................

(j) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo. (alama 4)

(i) Kaumu amewafanya mifugo wangu wanywe maji.
(Anza kwa: Mifugo wangu , usitumie, 'amewafanya'.)

..........................................................................................................................

(ii) Wanakijiji wanaishi karibu na msitu. Wanakijiji hawawavamii wanyama.
(Unganisha kuunda sentensi ambatano.)

..........................................................................................................................

(k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa. (alama 1)
Ngoma hizo zao ziliibwa na wezi wale.

..........................................................................................................................

(l) Tumia 'kwa' katika sentensi kuonyesha:

(i) sehemu ya kitu kizima (alama 1)

..........................................................................................

(ii) namna tendo lilivyofanyika (alama 1)

..........................................................................................

(m) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)
"Kusoma kwa mapana kutapalilia ubunifu wa wanafunzi hawa wenu," mtaalamu akatuambia.

..........................................................................................

(n) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Viwanda vikianzishwa mashambani idadi ya wanaohamia mjini itapunguzwa.

..........................................................................................

(o) Tunga sentensi zenye miundo ifuatayo. (alama 2)

(i) KN (N + RH) + KT (Ts + T)

..........................................................................................

(ii) KN (V + N) + KT (t + v)

..........................................................................................

(p) Ainisha yambwa katika sentensi ifuatayo.
Mhunzi alimfulia mjukuu wake pete ya shaba. (alama 2)

..........................................................................................

(q) Bainisha maana **mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Bedui alimrushia tufe.

..........................................................................................

..........................................................................................

(r) Alama za mtajo hutumiwa kufungia maneno halisi ya msemaji. Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mengine **mawili** ya alama za mtajo. (alama 2)

..........................................................................................

..........................................................................................

(s) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kutumia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari.
Mwanafunzi mkakamavu huzingatia masomo yake. (alama 1)

....................................................................................................

(t) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **rithi** na **ridhi**. (alama 2)

....................................................................................................

(u) Tunatumia simile tunapotaka mtu atupishe,.......................................tunapoomba kitu kinusurike, na kefule............................................... na jambo, (alama 1)

(v) Andika visawe vya maneno yafuatayo: (alama 1)

(i) doa ....................................................................................

(ii) omba ....................................................................................

(w) Andika sentensi ifuatayo upya kulingana na maagizo. (alama 1)

Maeneo haya yana uyoga.
(Anza kwa: Uyoga.)

....................................................................................................

3INED

4. **ISIMUJAMII**: (Alama 10)

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

"Kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa, mahakama hii imethibitisha bila chembe ya shaka kwamba wewe mshtakiwa, Bi Mlachake Chauchau ndiye uliyepika pombe haramu ambayo ilisababisha vifo vya raia hamsini na kupofuka kwa wengine mia moja. Unahukumiwa kwa kosa la mauaji."

(a) Bainisha sajili ya makala haya kwa kutoa mifano **miwili** kutoka kwenye makala. (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(b) Fafanua sifa nyingine **nane** za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya. (alama 8)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1. Lazima** (20 marks)

*Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

Walikuja mahasidi, ah, walikuja
Nyayo zao zikirindima, ah rindima
Kwa ghamidha ya uadui, oo uadui
Wali wakibeba sime
Wali wakibeba mata
Wali wakibeba mienge
ya moto kutangazia
kwao kuwasili

Walikuja kwa ndimi
zilohimili cheche
matusi kutumwaiya.
Hawakujua ya kwamba
mbele ya mhimili huno wetu
wao wali vipora.
Kwenye Mlima wa Sugu, walituvamia.
Aliwakabili Mbwene
Mwana wa Ngwamba, ee Mbwene
Aliwakabili Mbwene kwa kitali kikali.
Wali wametuteka ja samaki kwenye dema
Wali wamewapukutisha
wetu mabarobaro
Aliwakabili Mbwene
Ee Mbwene, Mwana wa Ngwamba
Aliwakabili
kwa hamasa za ujana
kwa uchungu wa kuumbuliwa
wa wetu wana.

Aliwakabili Mbwene
Nao wakalipiza shambulizi
kwa kujidai majagina
walijibwaga uwanjani
Laiti wangalijua wanajikabidhi
viganjani mwa Mbwene.
Aliwakabili Mbwene, ee
Mwana wa Ngwamba, shujaa asoshindwa
alipigana kitali

cha kufa na kupona
kuiopoa jamii yetu,
kuirejesha hadhi yetu.
kuirejesha mifugo yetu
kuwarejeshea wakulima vikataa vyao
kuwaokoa vipusa wetu
nyara waliotekwa, ati walipiza kisasi.

Aliwakabili Mwana wa Ngwamba
Aliwakabili Upepo wa Kusi
Hata kikomo cha mapambano kilipofika
Wagundi walijua kwamba
Walikuwa na Mwana, ee Mwana
Mbwene, ee Mwana wa Ngwamba
Hakuwa na kifani, ee kifani
Alipigana nao, ee Mwana wa Ngwamba
Kwa siku kumi bila tonge wala tone la maji
Kwetu kukenda kicheko cha wokovu
Kwao kukenda kilio.

(a) "Huu ni wimbo wa sifa." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano **mitatu** kutoka kwenye utungo huu. (alama 3)

(b) Andika sifa **tatu** za jamii ya nafsineni katika utungo huu. (alama 3)

(c) Huku ukitoa mifano, bainisha vipengele **vinane** vya kimtindo ambapo nafsineni imetumiwa kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama 8)

(d) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii yako. Fafanua hoja **sita** utakazotumia kuishawishi jamii yako kukinga dhidi ya hali hii. (alama 6)

## SEHEMU B: RIWAYA

### K. Walibora: *Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

**2.** "Lakini waliogopa...Waliogopa hata kuwa na uoga."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha tamathali **moja** ya usemi ambayo imetumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

(c) Kwa kurejelea hoja **kumi na nne** kutoka kwenye riwaya hii, thibitisha kwamba raia wa Tomoko walistahili kuogopa hata kuwa na uoga. (alama 14)

3. (a) "Usinivue nguo kwa macho yako wee!"
Kwa kurejelea hoja **kumi na mbili** kutoka kwenye riwaya hii, thibitisha kwamba mzungumzaji anastahili kuvuliwa nguo. (alama 12)

(b) Tathmini umuhimu wa barua ya Ben Bella kwa Mashaka katika kuijenga riwaya hii. (alama 8)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**T. Arege:** *Mstahiki Meya*

*Jibu swali la 4 au la 5.*

4. "Tuyashughulikie ya leo. Kesho, keshokutwa na mtondo hatutakuwepo. Wayatakia nini ya mtondogoo?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha sifa ya mzungumzaji inayodokezwa na kauli iliyopigiwa mstari. (alama 1)

(c) Eleza sifa **tano** za anayeambiwa maneno haya. (alama 5)

(d) Kwa kurejelea hoja **kumi** kutoka kwenye tamthilia, onyesha jinsi kutoyataka ya mtondogoo kulivyozorotesha hali ya maisha Cheneo. (alama 10)

5. "Ni mgao wa wakubwa kula kwanza na sisi wengine kupigania makombo yanayoanguka chini."

(a) Fafanua sifa **tano** za mzungumzaji. (alama 5)

(b) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hoja **kumi na tano** kutoka kwenye tamthilia. (alama 15)

## SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au la 7.*

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Mwanangu, wenye dhambi vishawishi, vikejeli
Mwanangu, katu wasikushawishi, binkuli
Mwanangu, aushi nayo uishi, kama mwali
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, sherati sikuperembe, kakubali
Mwanangu, usiwache wakubembe, kwa sali,
Mwanangu, mithili yao mapembe, ya fahali

Mwanangu sikubali!
Mwanangu, wajeuri siwe nao, ni shubili
Mwanangu usifwate njia zao, pita mbali
Mwanangu, ujeuri sera yao, mazohali,
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, waongo usiwasifu, kulihali
Mwanangu, uongo ubatilifu, si amali
Mwanangu, ndimi zao hazikifu, si manzili
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, wafisadi siwe nao, kemikali
Mwanangu, tamaa ndo utu wao, si Injili
Mwanangu, wahepe kila uchao, kiakili
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, wote walio wabaya, wanadhili
Mwanangu, usije ukawapeya, ikibali
Mwanangu, katika hino duniya, kaa mbali
Mwanangu sikubali!
(J. Kiponda)

(a) Fafanua mambo **sita** ambayo yanaweza kuzorotesha maadili ya anayelengwa na shairi hili. (alama 6)

(b) Bainisha tamathali **mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(c) Andika aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(d) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama 4)

(i) idadi ya vipande katika mishororo.

(ii) mpangilio wa maneno katika mishororo

(iii) idadi ya mizani katika mishororo.

(iv) mpangilio wa vina katika beti.

(e) Andika aina **mbili** za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(f) Andika ubeti wa **tano** kwa lugha ya nathari. (alama 4)

7. *Soma Shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Walo nacho hawachi
mshangao kunitia
Moyoni watakutia
pindi waonapo
we u chambo cha

Hawa ni wa kuajabiwa
Watakupa yao kazi
Mpangilio wa kazi
wakukabidhi wao
na malengo wakupe
La! Hawakupi!
Wanakuhusisha
katika kuyavyaza na
muda wa kuyafikia
nao mwaafikiana
ati kuna makubaliano bayana
ambayo ubatizo wayo ni
kandarasi ya utendakazi.
Ela we nao mnajua
ndo kigezo cha kupimia
wako uwajibikaji
wako mchango chunguni
yako thamani
Na usidhani una hiari ya
kuamua tapofika
Watakusukuma
kufikia yao shabaha
bila kuwazia
ujira wanokupa.
Watakuhimiza
kutumia chako kipawa
kuikoza nundu yao mafuta
Viumbe hawa!
Mabepari - waajiri.

(a) Eleza mikakati **sita** inayotumiwa na waajiri kujikuza kiuchumi. (alama 6)

(b) Bainisha tamathali **tatu** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)

(c) Huku ukitoa mifano, bainisha aina **mbili** za uhuru wa kishairi aliotumia mshairi. (alama 2)

(d) Andika mifano **miwili** ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 2)

(e) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 1)

(f) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)

(g) Andika ubeti wa **tatu** kwa lugha ya nathari. (alama 4)

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

**K. Walibora na S. A. Mohamed** (Wah): *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

**8.** (a) Tathmini umuhimu wa Lucy katika kuijenga hadithi, "Tazamana na Mauti." (alama 10)

"Mizizi ya Matawi" (Ali A. Ali)

(b) "Aaa, bibi yangu namuomba Mungu anisamehe dhambi zangu ..."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) "Jamii ya," Mizizi na Matawi inastahili kusamehewa." Fafanua kwa kutoa hoja **sita** kutoka kwenye hadithi. (alama 6)

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education

# 102/1 – KISWAHILI – Karatasi ya 1
## INSHA
## Nov. 2018 – Muda: Saa 1¾

---

**Jina** .................................................. **Nambari ya Mtahiniwa** ..........................................

**Sahihi** .............................................. **Tarehe** ..........................................................

---

**Maagizo**

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima****.*
(d) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
(e) *Kila insha isipungue maneno* ***400****.*
(f) *Kila insha ina alama 20.*
(g) *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
(h) *Insha zote* ***sharti*** *ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
(i) ***Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.***
(j) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

---

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**1.** **Lazima**

Wewe ni katibu wa chama cha Walinda Mazingira Wasio na Mipaka shuleni mwenu. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika kujadili suala la uharibifu wa mazingira katika eneo lenu.

**2.** "Udanganyifu katika mitihani haumwathiri mwanafunzi tu, bali pia jamii yake." Fafanua.

**3.** Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
Mti mkuu ukigwa, wana wa ndege huyumba.

**4.** Tunga kisa kinachoanza kwa kauli ifuatayo:
"Waja husema kuwa subira huvuta heri: hii yangu inazidi kuvuta machungu kila kuchapo. Hii heri itapatikana lini?" Tuama alijisemea kwa masikitiko.

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education

# 102/2 – KISWAHILI – Karatasi ya 2

## LUGHA

## Nov. 2018 – Muda: Saa 2½

---

**Jina** .................................................. **Nambari ya Mtahiniwa** ........................................

**Sahihi ya Mtahiniwa** .......................... **Tarehe** ..............................................................

---

**Maagizo**

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Jibu maswali **yote**.*
(d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
(e) *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
(f) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
(g) ***Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.***
(h) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

---

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

**1. UFAHAMU** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

"Mabibi na mabwana, ndugu wapenzi, alianza Bi. Mkesha, "huu ni mwaka wa tano tangu tufanye uchaguzi mkuu uliowapa vigoda wenzetu hawa. Katika kipindi hiki kumetokea mengi ya kujipigia kidari, pametokea pia mengi, mengi mabaya ya kuitia jamii ya Tungama izara. Tumejipa mkono wa tahania kwa uteuzi wetu mzuri. Vilevile tumejisuta kwa uteuzi usio wa kuridhisha.

Ndugu wapenzi, sina haja ya kuwakumbusha yote ambayo tumepitia; mmeyashuhudia yote. Ila ninayotaka kusema ni kwamba **malengo yetu ya kuwateua viongozi yamesalitiwa**. Ndugu zangu, itakumbukwa kwamba watangulizi wetu walianza safari ya kurejesha utu wa Mwafrika wakiwa na nia thabiti ya kuwabwaga maadui watatu wa maendeleo. Je, mnawajua maadui hao? Ni ujinga, magonjwa na umaskini. Waanzilishi wa taifa hili, pamoja na viongozi waliowafuata walipigania huduma za bure za afya, na elimu ya bure na ya lazima kwa wote. Vijana wetu walijitoma ugani kuzamia lulu ya elimu; wakavidhihaki vitabu hadi kufikia kilelecha cha elimu. La kusikitisha ni kwamba elimu hii imekuwa laana kwao. Mnajua kisa na maana ya hali hii? Natija iliyotarajwa haikupatikana. Na haya si mageni kwetu. Mnajua wapo vijana humu vijijini ambao wamepiga lami kwa miaka na mikaka bila kuambulia kazi za hadhi ambazo waliahidiwa huko vyuoni. Hatimaye hawa hawa wenye shahada mbili, na wengine hata tatu, ndio wanaokuwa matarishi wa wale ambao walichechemea masomoni. Vijana wengine, kwa kukosa hata huo utarishi, wameamua kuanzisha biashara rejareja ili kujikimu; wamekosa la mama, wanaamwa la mbwa. Sina haja ya kuwafafanulia kiini cha hali hii ya kutamausha.

Ni dhahiri kwamba uthabiti wa taifa lolote lile hutegemea uthabiti wa uongozi, na uaminifu wa raia wake katika kuuwajibisha huo uongozi. Hata hivyo, inasikitisha kwamba wengi wetu tumejipoka uwezo wa kuuwajibisha uongozi kwa kuwa mawindo rahisi ya uzungukaji mbuyu. Huu ndio uwele ambao umeufisidi utu wetu na kutusahaulisha thamani za kitaifa. Hebu niambie ewe mama mwenzangu, kuna faida gani kuuza kura yako kwa kibaba cha unga na noti ya shilingi mia moja, ati kwa kuwa unaambiwa, 'Ukinichagua nitahakikisha kwamba ile *Affirmative Action* imezingatiwa? Ipo haja gani kuchomwa na jua ukiwafuata hawa hawa viongozi, ukiwaimbia nyimbo za kuwatia raia kichaa cha shangwe ili kuwapembeja wawapigie kura? Je, faida kwako imekuwa gani? Hujangojea kwa kipindi chote hiki kusakafiwa kwa hiyo barabara uliyoahidiwa siku ulipouza kura yako? Na ile ahadi ya 'mwenzetu' ya kuwaajiri vijana wetu kwenye Jeshi la Wanamaji imetimia? Hatujashuhudia watu wa akraba moja wakisombwa kutoka humu kijijini kwenda kuchukua nyadhifa katika mashirika ya umma?"

"Kweli waso haya wana mji wao, Bi. Mkesha **amejikosha** kweliweli," Bi. Kuli alimwambia mwenzake Bi. Kengemeka kisha akaendelea." Anatuambia yepi mageni ambayo masikio haya yangu yaliyokula chumvi ya miongo sita ushei ya miaka hayajasikia?"

"Anasema tumpe nafasi ajitome kwenye uwanja wa majogoo," akajibu Bi. Kengemeka, "atakuwaje tofauti na hao wanaume?" Hata hao wanawake tumewahi kuwapa nafasi, wakatutenda zaidi ya wanaume. Usinikumbushe kura yangu niliyoipoteza kwa kumkweza Bi. Shali kwenye usukani. Siwezi kusahau namna ile ahadi ya maji ya mabomba na kuchimbwa kwa visima ilivyoishia kwenye kauli yake tu."

Tumetendwa sote mwenzangu," alisema Bi. Kuli, "inasikitisha kwamba dau la masomo ya wanangu limeenda mrama huku nikikimlilia huyo huyo Bi. Shali. Kila mara tunasikia kupitia

vyombo vya habari kwamba serikali imeanzisha Hazina ya Eneobunge kuyafadhili masomo ya watoto kutoka familia maskini. Lengo kuu, nasikia, ni kuhakikisha kwamba asilimia kubwa ya watoto haipati fursa ya kujiunga na shule tu, bali pia inakamilisha masomo . 'Hata hivyo, huu ni mwaka wa tatu tangu wanangu watatu waache masomo kutokana na ukosefu wa karo. Na usidhani ni karo ya shule ya kitaifa, la, hasha! Ni karo ya shule za kutwa ambapo niliwapeleka baada ya huyu huyu Bi.Shali kunitilia huku akinitolea huko kuhusiana na ufadhili wa masomo."

"Usinikumbushe yaliyomfika mwanangu Neema," alisema Bi. Kengemeka huku akitwaa ukingo wa kanga yake kujipangusa machozi. "Mwana huyu alikaa nyumbani kwa muhula mzima," akaendelea Bi. Kengemeka," dhiki ya kuwaona wenzake wakienda shuleni huku yeye anabaki nyumbani ikamfanya kuwa windo rahisi la mmoja wa hao wabunge, akaambulia uja uzito ambao hakuulalia wala kuuamkia. Mwenyewe mbunge ameshika hamsini zake kana kwamba hakufanya lolote. Mwanangu Jabali naye amehiari kuwa kibarua katika shamba la mbunge wa sasa. Mwenyewe anasema anataka kudunduiza pesa ili arudi shuleni kukamilisha mwaka wake wa mwisho. Na usidhani ni hao wangu tu waliofikwa na ya kuwafika. Tumewaona wana wa wenzetu tuliopiga foleni pamoja kuwateua hao hao wabunge, wakitumiwa kama masoko ya dawa za kulevya. Wengine wamegeuzwa walanguzi wa dawa hizi," Bi. Kengemeka alikamilisha uzungumzi wake na kushusha pumzi kana kwamba ameutua mzigo mzito.

Hata hotuba ya Bi. Mkesha ilipofikia ukingoni, Bi. Kuli alimwambia mwenzake, "Ninavyoona ni kwamba wanasiasa wote wamefinyangwa kutoka aina sawa ya udongo. Ikitokea kwamba tutampa huyu Bi. Mkesha kura, tumpe kwa kulazimika kikatiba kupiga kura; tusiwe na matarajio makuu. Inasikitisha kwamba vijana wetu waadilifu hawataki kujitia najisi kwa kuingilia siasa. Yule kijana wetu Angaza angekubali rai ya wazee kujitoma ulingoni tungemuunga mkono.

(a) "**Malengo yetu ya kuwateua viongozi yamesalitiwa**." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hoja sita kutoka kwenye taarifa. (alama 6)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(b) Eleza mchango wa wanyonge katika hali ya uongozi nchini Tungama. (alama 3)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(c) Bainisha mbinu **nne** ambazo Bi. Mkesha anatumia kuishawishi hadhira yake. (alama 4)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(d) (i) Andika kisawe cha, 'kuwapembeja' kwa mujibu wa taarifa. (alama 1)

..........................................................................................................................

(ii) Andika maana ya, 'amejikosha' kulingana na taarifa. (alama 1)

..........................................................................................................................

717

0465

2. **UFUPISHO** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Tangu jadi, jamii za Kiafrika zilikuwa na majukumu bayana ya kijinsia. Kila jamii ilipania kuyarithisha majukumu haya kwa vijana wa vizazi tofautitofauti. Katika jamii nyingi, vikao maalumu viliandaliwa ili kuwaelekeza vijana kuhusu namna ya kukabiliana na majukumu yao ya kijamii. Nyakati nyingine mafunzo haya yalitolewa katika vipindi vya burudani kama vile utambaji wa ngano. Kadhalika, maarifa mengi kuhusu namna ya kukabaliana na majukumu na changamoto za jinsia mahususi yalitolewa kupitia sherehe maalumu za kitamaduni almaarufu miviga. Mifano ya sherehe hizi ni kama vile upashaji tohara, arusi, na hata matanga.

Jamii za zamani, kama zilivyo za kisasa, zilikuwa na matarajio mahususi kwa watu wa jinsia zote. Mathalani, katika jamii nyingine za Kiafrika, mwanamume ndiye aliyetarajiwa kuikimu aila yake. Katika kipindi cha Usasi na Kuhemera kwa mfano, mwanamume ndiye aliyekuwa na jukumu la kwenda kichakani kuwinda. Hali kadhalika, mwanamume ndiye aliyetarajiwa kufanya kazi zilizohitaji nguvu kama vile kufyeka misitu kwa ajili ya kutengeneza mashamba, kuchimba migodi, kuchonga mawe, kufua vyombo vya dhahabu na fedha, kuchonga vinyago,

na kazi nyingine zilizohitaji nguvu. Mke naye alitengewa jukumu la ulezi, si wa watoto wake tu, bali pia wa mume wake, na hata jamii pana. Ilikuwa jukumu la mwanamke kubaki nyumbani kumpikia mumewe na watoto, kufua nguo na kunadhifisha mazingira. Wakati mwingine waume wao walipojitoma msituni kupigania uhuru, wanawake ndio waliowapikia chakula na kutafuta mbinu za kuwafikishia huko huko msituni.

Watoto wa kike walifunzwa kuzilinda jamii zao, si kwa mali tu, bali pia kwa hali. Walifunzwa kwamba furaha na afya ya familia zao, kimwili, kihisia na kisaikolojia ilimtegemea mama. Ndiye aliyehakikisha kwamba familia yake imepata lishe bora, ndiye aliyekuwa mwalimu wa kwanza wa watoto wake; akawafunza namna ya kujithamini na kuwathamini wenzao; akawafunza pia namna ya kutatua migogoro yao kwa njia ifaayo. Kwa upande mwingine, watoto wa kiume walifunzwa umuhimu wa kuwa watu wa kutegemewa na jamaa zao, pamoja na kubuni mikakati ya kuzihakikishia familia zao usalama.

Jamii ya kisasa inazidi kukua na kutwaa uchangamano, nayo mitazamo ya binadamu kuhusu masuala na hali mbalimbali inaendelea kubadilika. Siku hizi kwa mfano, si ibra kupata kwamba majukumu ambayo awali yalikuwa yametengewa jinsia mahususi sasa yametwaliwa na jinsia zote. Imedhihirika kwamba kupanda kwa gharama ya maisha kumezua haja ya waume kwa wake kushirikiana bega kwa bega kuchumia vyungu vya familia zao. Asilimia ya wanawake ambao wanafanya kazi za ajira katika mashirika ya umma na ya kibinafsi imepanda. Kadhalika, kinyume na zamani, idadi kubwa ya wanawake imesoma. Hakika wapo wanawake wengi ambao wameibuka kuwa magwiji katika taaluma kama vile uhandisi, udaktari na usoroveya ambazo awali zilikuwa milki ya wanaume pekee. Ulingo wa siasa nao umetwaa sura mpya. Idadi ya wabunge wanawake inaendelea kupanda kila kuchapo. Wapo pia wanawake ambao wamejiunga na vikosi vya kulinda usalama; jambo ambalo halikuwa la kawaida katika jamii nyingi hapo awali. Wanaume nao wametwaa kazi ambazo awali zilitengewa wanawake pekee. Katika baadhi ya jamii za Kiafrika, mwanamume ambaye alipatikana jikoni alichukuliwa kuwa anaufedhehesha ukoo. Siku hizi si ajabu kuwapata akina baba wengine wakiziandalia familia zao vyakula. Vilevile idadi ya wanaume wanaosomea kazi ya uuguzi inazidi kuongezeka. Pia wapo wanaume ambao wanafanya kazi ya ususi na kuwarembesha wanawake. Hali hii ya mwingiliano wa majukumu haisaidii tu kukabiliana na changamoto ya tofauti za kijinsia, bali pia hupalilia mshikamano wa kijamii. Watu wanapobadilishana zamu katika kutekeleza majukumu ya kijamii huthaminiana. Hujiona kama wanaotegemeana kwa hali zote, na kwa njia hii utangamano hujengeka zaidi. Kadhalika, kubadilishana majukumu ni njia bora ya kufidia udhaifu wa wenzetu.

Ni dhahiri kwamba kumekuwa na mwingiliano mkubwa wa kimajukumu, hali ambayo imeziwezesha jamii nyingi kufikia ufanisi mkubwa. Hata hivyo, imebainika kwamba hali hii inaelekea kumomonyoa faida ambazo jamii nyingi zimepata kwa wanaume na wanawake kushirikiana kutekeleza majukumu anuwai. Mathalani, wazazi wengi siku hizi wamo mbioni kutafuta elimu, ama kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kikazi, au kwa kukamia malipo zaidi. Kuna baadhi ya wazazi ambao hujisajili kwa kazi mbalimbali, si kwa sababu wanahitaji maarifa fulani, bali kwa sababu wanataka kuwapiku wenzao katika ndoa. Matokeo ni kwamba mume na mke wanajipoka muda wa kukaa pamoja na kufahamiana, pengo la kimahusiano nalo linajengeka, hali ambayo imesababisha kusambaratika kwa baadhi ya ndoa. Hali kadhalika imebainika kwamba, kwa sababu ya mume na mke kuwa mbioni kujiendeleza kitaaluma na kielimu, malezi ya watoto yameanza kutetereka. Jukumu la kuwalea watoto na vijana limetelekezewa vijakazi, vitwana na hata vibonzo!

Ibainike kwamba kila jambo sharti liwekewe mipaka. Yapo majukumu ambayo sharti yatekelezwe na jinsia maalum, yumkini kwa sababu za kimaumbile. Yapo majukumu kama vile malezi ya watoto ambayo sharti yachangiwe na kila jinsia.

(a) Fupisha ujumbe wa aya **tatu** za kwanza kwa maneno 80. (alama 7, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

**Nakala Safi**

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

ED

(b) Eleza masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya **nne** za mwisho. (maneno 90)
(alama 8, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

**Nakala Safi**

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

**3. MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 40)

(a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) kipasuo ghuna cha midomoni

..............................................................................................................

(ii) irabu ya kati, chini

..............................................................................................................

(iii) kikwamizo sighuna cha kaakaa gumu

..............................................................................................................

(iv) nazali ya ufizi

..............................................................................................................

(b) Bainisha silabi zilizowekewa shadda katika maneno yafuatayo: (alama 1)

(i) miambakofi

..............................................................................................................

(ii) yatazoleka

..............................................................................................................

(c) Andika neno lenye muundo ufuatao: (alama 2)

(i) kiambishi ngeli, wakati uliopita, mzizi, kauli tendwa, kauli tenda (kiishio)

..............................................................................................................

(ii) kiambishi cha wingi, mzizi

..............................................................................................................

(d) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo. (alama 4)

(i) Uaminifu wa mtu humfanya aheshimiwe.
(Badilisha nomino iliyopigiwa mstari kuwa kivumishi.)

..........................................................................................................

(ii) Shama,Tegea na Koru ndio walioibuka washindi.
(Tumia kiwakilishi nafsi badala ya maneno yaliyopigiwa mstari.)

..........................................................................................................

(iii) Mchuuzi alinunua mboga zilizofungwa pamoja.
(Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari.)

..........................................................................................................

(iv) Seluwa ni mtiifu. Maria ni mtiifu pia.
(Unganisha kuwa sentensi moja yenye kihusishi cha kulinganisha.)

..........................................................................................................

(e) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 1)

(i) ugwe ..........................................................................................

(ii) limau ..........................................................................................

(f) Unganisha sentensi zifuatazo kuunda sentensi ya masharti. (alama 2)
Moto ulidhibitiwa. Kulikuwa na vifaa vya kutosha.

..........................................................................................................

(g) Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 1)

Nahodha alilikwepa jabali hilo, chombo kikafika ufuoni salama.

..........................................................................................................

(h) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)
nomino, kishazi kitegemezi, kitenzi, nomino, kivumishi, kielezi

..........................................................................................................

(i) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya mazoea. (alama 1)

Barabara nyingi zimesakafiwa.

..........................................................................................................................................

(j) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kuanza kwa neno: Wanafunzi. (alama 2)

Wageni wamefika.Wanafunzi wamefurahi.

..........................................................................................................................................

(k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.

Nguo ambazo zinauzwa kwenye duka hilo zinavutia. (alama 1)

..........................................................................................................................................

(l) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo. (alama 4)

(i) Muutu aliwalea watoto wa Maki.
(Anza kwa: Watoto wa Maki.)

..........................................................................................................................

(ii) Maji yalijaa. Maji yalimwagika.
(Unganisha kuunda sentensi changamano.)

..........................................................................................................................

(m) Tumia kielezi cha kiasi badala ya kile kilichopigiwa mstari. ( alama 1)

Sewe alituelezea jambo hilo <u>kinaganaga</u>.

..........................................................................................................................................

(n) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Viongozi wengi walikuwa waadilifu mno kabla ya Uchaguzi Mkuu.

..........................................................................................................................................

(o) Changanua sentensi zifuatazo kwa kielelezo cha mstari.

(i) Hili lake lilikuwa limeiva lakini hatukujua. (alama 2)

........................................................................................................................

........................................................................................................................

(ii) Mkufu wa Umu unapendeza mno. (alama 1)

........................................................................................................................

(p) Andika maana **mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo.
Medi anasema atawarithisha nyumba yake. (alama 2)

........................................................................................................................

(q) Akifisha sentensi ifuatayo.
jihadhari akasema kulei uamuzi wako unaweza kukuathiri vibaya. (alama 2)

........................................................................................................................

(r) Kanusha sentensi ifuatayo.
Mkulima anahitaji magunia haya. (alama 1)

........................................................................................................................

(s) (i) Karimu ni kwa choyo ........................... ni kwa kukashifu na ........................... ni kwa tele. (alama 2)

(ii) Maarufu ni kwa mashuhuri, ukoo ni kwa ...........................ilhali faida ni

kwa ........................... ( alama 2)

(t) Tunga sentensi **moja** kubainisha maana **mbili** za neno: kata. (alama 2)

........................................................................................................................

4. **ISIMUJAMII** (Alama 10)

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Ndugu wapenzi, waumini wenzangu, mbazi hii haionyeshi huruma ya Mwenyezi Mungu kwetu wakosefu tu, bali pia inatufunza umuhimu wa unyenyekevu na msamaha.

(a) Bainisha sifa **tatu** za sajili ya kidini zinazojitokeza katika makala haya. (alama 3)

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

(b) Fafanua vipengele vingine **saba** vya kimtindo ambavyo mhubiri huyu angetumia kufanikisha mazungumzo yake. (alama 7)

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education

**102/3 – KISWAHILI – Karatasi ya 3**

**FASIHI**

**Nov. 2018 – Muda: Saa 2½**

Jina ............................................ Nambari ya Mtahiniwa ............................................

Sahihi ............................................ Tarehe ............................................

**Maagizo**

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
(d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima****.*
(e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
(f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*
(g) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
(h) *Majibu yote* ***sharti*** *yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
(i) ***Karatasi hii ina kurasa 24 zilizopigwa chapa.***
(j) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

954
0397

## SEHEMU A : USHAIRI

**1. Lazima**

A. Mazrui: *Chembe Cha Moyo*
*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Nimeyaandika maneno haya
    Kwa niaba ya:
    Mamilioni wasio malazi
    wabebao vifurushi vilivyo wazi
    wazungukao barabarani bila mavazi
    ...milki yao ya maisha.
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki
wiki baada ya wiki
    leo sumu au spaki
    leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
wale mayatima wa maskini
wazungukao mapipani
kila pembe mjini
kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza
walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
polepole wakijiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana watazama
wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
bila ya mtu kuona
    kama kwanba sote tu vipofu,

"Kifo ni shujaa,
Ikiwa mimi Gunge mwili wangu huu mtukufu
kwa tambo na nemsi
nitaukubalia
kuwa lengo la dua za kuonewa imani
kuwa karamu ya macho ya mahasimu
kuvikwa suti na mwosha
kufunikwa kwa udongo uliolaaniwa
Mimi Gunge,
Niliruhusu jabali kubwa
Likibinye changu kichwa
Likidhibiti changu kidari
Linizibe zangu pumzi
Gunge niache kutawala."

(i) Huu ni wimbo wa aina gani? (alama 1)

(ii) Andika sababu **mbili** kuthibitisha jibu lako la a(i). (alama 1)

(iii) Ni nani anayeimbiwa na nafsineni? (alama 1)

(iv) Bainisha matatizo **mawili** yanayoikumba jamii inayosawiriwa na utungo huu. (alama 2)

(v) Bainisha mbinu zifuatazo katika wimbo huu. (alama 3)

I. ritifaa

II. mbinu rejeshi

III. taashira

(vi) Unanuia kutumia mbinu ya kutazama na kushiriki kufanya utafiti kuhusu nyimbo za aina hii. Eleza sababu **sita** za kuchagua mbinu hii. (alama 6)

(b) Fafanua mikakati **sita** ambayo jamii inaweza kutumia ili kuudumisha utanzu wa semi. (alama 6)

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

FOR ANSWERS SMS OR WHATSAPP 0723981225